
# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TAARIFA YA SERIKALI KUHUSU UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015 -2020 KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA, 2015 HADI DESEMBA, 2017



**MWENYEKITI WA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI**

**Imetayarishwa na :**
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Reli,
S.L.P. 980,
**40480 – DODOMA,**

Desemba, 2017.

# YALIYOMO Ukurasa

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

Utangulizi .......... 1

**SURA YA PILI** .......... **4**

Hali ya Uchumi .......... 4
Kilimo na Ushirika .......... 8
Mifugo na Uvuvi .......... 14
Maliasili na Utalii .......... 19
Viwanda na Biashara .......... 24
Madini .......... 26
Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi .......... 32
Usafirishaji na Uchukuzi .......... 41
*Madaraja* .......... *56*
*Vivuko* .......... *61*
*Usafiri wa Anga* .......... *62*
*Huduma za Hali ya Hewa* .......... *65*
*Miundombinu ya Huduma za Reli* .......... *65*
*Usafiri wa Majini* .......... *67*
Nishati .......... 70
Mawasiliano .......... 75
Huduma ya Afya .......... 78
Elimu, Sayansi na Teknolojia .......... 91
Maji .......... 102
*Majitaka* .......... *110*
*Umwagiliaji* .......... *111*
Kuimarisha Muungano .......... 113
Utawala Bora na Demokrasia .......... 117
Vyombo vya Ulinzi na Usalama .......... 120
*Jeshi la Zimamoto na Uokoaji* .......... *121*
*Jeshi la Polisi* .......... *122*
*Jeshi la Magereza* .......... *124*
*Idara ya Uhamiaji* .......... *126*
*Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa* .......... *127*
Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki .......... 130
Kuhamia Makao Makuu Dodoma .......... 132
Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Majanga .......... 134
Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI .......... 135
Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya .......... 138
Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo .......... 139
Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi .......... 143
Kuendeleza Makundi Maalumu .......... 146

Watu Wenye Ulemavu ........................................................................................................................148
*Wafanyakazi.........................................................................................................................150*
*Kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii.......................................................................................151*

**SURA YA TATU........................................................................................................................ 152**

Matarajio ..................................................................................................................................152

**SURA YA NNE ......................................................................................................................... 154**

Hitimisho ..................................................................................................................................154

## ORODHA YA BANGOKITITA ZINAZOONESHA UTEKELEZAJI WA ILANI KATIKA KILA SEKTA

**Bangokitita Na. 1: Kuimarika kwa Hali ya Uchumi Nchini…………………………………………………………………………….4**

# SURA YA KWANZA

## *1.0 Utangulizi*

Serikali ya Awamu ya Tano iliingia madarakani Novemba, 2015 baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015. Katika uchaguzi huo, Wananchi walikipa Chama cha Mapinduzi ridhaa ya kuongoza Dola katika kipindi kingine cha miaka mitano (5) hadi mwaka 2020.

Katika Kipindi cha miaka mitano (5) ya utekelezaji wa Ilani, Chama cha Mapinduzi kimeielekeza Serikali ya Awamu ya Tano kuendelea kukabiliana na changamoto zinazowakabili wananchi kwa kuweka Sera madhubuti zitakazokuza uchumi kwa kasi kubwa; kupunguza tatizo la ajira hususan kwa vijana; kuondoa umasikini; kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya Umma; na kuendelea kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi na mali zao.

Aidha, Ilani hii inatekelezwa kwa kuzingatia mwelekeo alioutoa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015 Mjini Dodoma. Wakati wa uzinduzi huo, Mhe.Rais alizitaja baadhi ya kero zinazowakabili wananchi ambazo Serikali yake iliahidi kuzishughulikia kwa haraka kuwa ni:-

i. Upotevu wa mapato, kushindwa kukusanya kodi, ubadhirifu, matumizi mabaya ya fedha za Umma na utekelezaji wa baadhi ya miradi chini ya kiwango;

ii. Kupambana na ujangili uliokithiri wa nyara za Serikali na migogoro ya mipaka kati ya Vijiji na Hifadhi za Taifa;

iii. Uhaba wa pembejeo za Mifugo na Kilimo, tatizo la masoko, wakulima kukopwa mazao yao na ukosefu wa Wataalam wa ugani;

iv. Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuwepo kwa michango mingi isiyo ya lazima, malalamiko ya walimu yasiyoisha, mazingira ya kusomea ikiwa ni pamoja na majengo, madawati na ukosefu wa nyumba za walimu na;

v. Kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika wa reli, upungufu wa bandari kavu na mizigo mingi kusafirishwa kwa barabara.

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani imechukua hatua madhubuti katika kukabiliana na changamoto hizo na mafanikio ya dhahiri yameanza kuonekana katika kipindi hiki kifupi.

Mafaniko yaliyopatikana kutokana na hatua hizo za Serikali ya Awamu ya Tano ni pamoja na uchumi kuendelea kuimarika na kukua kwa wastani wa asilimia 7 mwaka 2016; kuongezeka kwa Pato la kila Mtu kutoka Shilingi 1,918,897 mwaka 2015 hadi Shilingi 2,131,299 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 11.1; kupungua kwa Mfumuko wa Bei kutoka wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2015 hadi asilimia 5.2 mwaka 2016. Mapato ya ndani yameongezeka kutoka wastani wa Shilingi bilioni 850 kwa mwezi hadi wastani wa Shilingi trilioni 1.3 kwa mwezi. Kuendelea kuimarika kwa hali ya uchumi na utoaji wa huduma za Jamii, kumewezesha maisha ya wananchi wa kawaida kuboreka kama inavyothibitishwa na taarifa ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo ya Watu kwa mwaka 2016. Kwa kigezo cha Fahirisi ya Maendeleo ya Watu (HDI) ambacho kimetumika katika taarifa hiyo, ustawi wa Watanzania umeimarika kutoka alama 0.521 mwaka 2014 hadi alama 0.531 mwaka 2015. Kigezo hiki huzingatia viashiria kadhaa vya maendeleo na ustawi, hususan muda wa kuishi baada ya kuzaliwa, elimu na wastani wa kipato cha mwananchi. Kigezo hiki kinaifanya Tanzania kuwa nchi ya pili kwa ustawi wa wananchi wake katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali za kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii kama vile elimu bila malipo, maji, afya na umeme katika maeneo ya vijijini na mijini.

Mafanikio mengine ni kusainiwa kwa Mkataba wa Kusanifu na Kujenga Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kati ya Kisasa kutoka Dar es Salaam - Morogoro (KM 300) utakaogharimu Shilingi Trilioni 2.74. Ujenzi wa kipande hicho ikiwemo ujenzi wa Kambi, ofisi na kiwanda cha kukarabati mataruma umeanza. Vilevie, ujenzi na ukarabati wa barabara mbalimbali nchini unafanyika ikiwemo barabara ya juu eneo la TAZARA, *Interchange* Ubungo, barabara nyingine Kuu na za Mikoa, ujenzi wa miradi ya Miundombinu ya umeme, maji na ununuzi wa meli mpya kwa ajili ya usafiri kwenye Maziwa makubwa. Aidha, Shirika la Ndege Tanzania limefufuliwa kwa kununua ndege sita mpya. Ndege mbili kati ya hizo ambazo zina uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja zimewasili nchini na zinaendelea kutoa huduma. Ndege nyingine zilizobakia zimelipiwa na zitaingia nchini katika kipindi kifupi kijacho.

Serikali pia imefanya mazungumzo na Serikali ya Uganda na kuridhia mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima – Uganda hadi Bandari ya Tanga. Aidha, mafanikio makubwa yamepatikana katika Sekta ya Madini baada ya makubaliano mapya na Kampuni zinazochimba madini nchini na marekebisho ya Sheria ya Madini. Hatua hizi zitaiwezesha Tanzania kupata faida kubwa tofauti na ilivyokuwa awali.

Kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi kifupi tangu Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani na kufuatia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea, Wananchi wana matumaini makubwa kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo Tanzania itakuwa na uchumi unaokua kwa kasi na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo.

Taarifa hii jumuishi imebainisha baadhi tu ya mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha Novemba, 2015 hadi Desemba, 2017 katika sekta mbalimbali. Taarifa ina Sura Nne. Sura hii ya Kwanza ambayo ni utangulizi inatoa picha ya jumla ya mafanikio yaliyopatikana. Sura ya Pili inabainisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 kisekta, ambapo sekta zimebainisha yale yaliyotekelezwa. Sura ya Tatu inaeleza kwa ufupi matarajio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi cha miaka mitatu iliyobakia ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Sura ya Nne ni Hitimisho.

# SURA YA PILI

## *2.0 Hali ya Uchumi*

Mwenendo wa viashiria vya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa mwaka 2016 na 2017 vinaonesha kuwa uchumi wetu unakua na kuimarika. Maelezo ya kina juu hali ya uchumi ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 1.

**Bangokitita Na. 1: Kuimarika kwa Hali ya Hali ya Uchumi Nchini**

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 20 (a) | Uchumi unaendelea kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 8 au zaidi na kuinua ustawi wa Watanzania kwa kuongeza mapato ya wananchi kufikia kiwango cha wastani wa nchi ya uchumi wa kati na hivyo, kuongeza fursa za ajira na kupunguza umasikini. | (i) Hali ya uchumi imeendelea kuimarika kwa ukuaji wa asilimia 7 mwaka 2015 na 2016. Sekta zenye ukuaji mkubwa ni pamoja na Habari na Mawasiliano asilimia 13.0, uchimbaji wa madini na mawe asilimia 11.5; na usafirishaji na uhifadhi mizigo asilimia 11.8. Nchi yetu inashika nafasi ya tatu kwa ukuaji wa uchumi Barani Afrika.<br>(ii) Katika mwaka 2016, wastani wa Pato la kila Mtanzania ulifikia Shilingi 2,131,299 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 1,918,897 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11. Mwenendo wa ukuaji wa uchumi utaiwezesha Tanzania kufikia kundi la nchi zenye Uchumi wa Kati lenye wastani wa Dola za Marekani 1,043 sawa na Shilingi 2,398,900. |
| 20 (b) (i) | Kudhibiti Mfumuko wa Bei ili uendelee kubaki kwenye tarakimu moja na hivyo kuzuia kasi ya kupanda kwa gharama za maisha. | Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, Mfumuko wa Bei umeendelea kubakia kwenye tarakimu moja. Mwezi Julai, 2017 Mfumuko wa Bei ulikuwa asilimia 5.2, na mwezi Agosti ulishuka hadi kufikia asilimia 5.0. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 20(b) (ii) | Kudhibiti nakisi ya bajeti ili iendelee kushuka na kufikia kiwango kisichozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa ili pamoja na mambo mengine, Tanzania iendelee kuwa kivutio kwa wawekezaji na kupunguza gharama za kukopa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. | Nakisi ya bajeti ya Serikali ilikuwa asilimia 1.8 mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2015/2016. Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kudhibiti matumizi kwa lengo la kupunguza nakisi ya Bajeti. |
| 20(b) (iii) | Kusimamia Deni la Taifa liendelee kuwa himilivu ili lisiwe mzigo kwa uchumi wetu bali liendelee kuwa fursa na kichocheo cha maendeleo ya nchi yetu. | (i) Viashiria vya uhimilivu wa Deni la Taifa vinaonesha kwamba uwiano kati ya deni na Pato la Taifa umefikia asilimia 31.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56. Vilevile, uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa Pato la Taifa ilikuwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 50.<br>(ii) Viashiria vya uwiano kati ya ulipaji wa deni la nje na uuzaji wa bidhaa nje ilikuwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Serikali imeendelea kulipa madeni yote yanayoiva kwa wakati. Viashiria hivi vinabainisha kwamba Deni la Taifa halina athari kwa uchumi wa Nchi yetu. |
| 20(b)(iv) | Kuhakikisha thamani ya Shilingi yetu inatengamaa ili kujenga imani ya uchumi wetu kwa lengo la kuongeza shughuli za uwekezaji, uzalishaji na biashara. | Thamani ya Dola ya Marekani ikipimwa kwa shilingi ya Tanzania ilipanda kwa asilimia 1.78 hadi Juni 2017 ikilinganishwa na Kenya iliyopanda kwa asilimia 2.27, Yuan ya China (asilimia 3.43), Faranga ya Rwanda (asilimia 5.38), Yen ya Japan (asilimia 6.69) na Shilingi ya Uganda (asilimia 6.93). |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 20(b) (v) | Kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni na kuepuka kuagiza bidhaa zisizo za lazima kutoka nje ya nchi. | Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 4.1 kufikia Dola za Marekani milioni 9,285.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola milioni 8,918.1 mwaka 2015. Aidha, uagizaji wa bidhaa na huduma nje ulipungua kwa asilimia 14 kwa mwaka 2016 kutoka Dola milioni 12,528.2 kwa mwaka 2015 kufikia Dola milioni 10,772.3. |
| 20(b)(vi) | Kuendelea kuwa na mikakati itakayowezesha kuwa na akiba ya fedha za kigeni zinazotosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje bila ya matatizo. | Hadi kufikia Desemba 2016, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani 4,325.6 ikilinganishwa na Dola milioni 4,093.7 Desemba 2015. Kiasi hicho kinaweza kulipia gharama za kununua bidhaa na huduma kwa miezi 4.2. Hadi Juni 2017, Serikali ilikuwa na akiba ya fedha za kigeni zenye uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa kipindi cha miezi 5.8. |
| 20(c) | Kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza vyanzo vipya vya mapato na kupanua wigo wa walipa kodi ili kuongeza uwezo wa Serikali wa kugharimia huduma za kijamii na kiuchumi. | Mapato ya Serikali yameongezeka kutoka wastani wa Shilingi bilioni 850 mwaka 2014 kwa mwezi hadi kufikia Shilingi trilioni 1.3 kwa mwezi Mwaka 2017. Aidha, Mapato ya Kodi yameongezeka kutoka Shilingi trilioni 9.908 mwaka 2014/15 hadi trilioni 14.266 mwaka 2016/2017. |
| 20(e)(i) | Kuendelea kupanua huduma za fedha hadi vijijini kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi. | Sera mpya ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 iliyotafsiriwa kwa Kiswahili imekamilika na kuzinduliwa rasmi Oktoba, 2017. Idadi ya wananchi waliosajiliwa na kutumia simu za kiganjani imeongezeka na kufikia milioni 17.7 mwaka, 2017 na kuwezesha wananchi kutumia simu hizo kupata bidhaa na huduma mbalimbali kwa urahisi na kwa wakati mijini na vijijini. Benki 36 zinatoa huduma ya uwakala wa kibenki |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | kwa waweka akiba na wakopaji wadogo kupitia Mfumo wa Huduma za Simu za Kiganjani. Mawakala waliosajiliwa wamefikia 398,094 na wana amana ya Shilingi milioni 1,180,440.8. |
| 20(e) (iii) | Kuweka mazingira yatakayo wezesha kushuka kwa riba ya mikopo katika Taasisi za Fedha ili kutoa fursa kwa wananchi kupata mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa riba nafuu. | Serikali imechukua hatua za kuongeza ukwasi katika uchumi na hivyo kudhibiti riba za mikopo. Hatua hizo ni pamoja na:<br>(i) Kupunguza riba ambayo inayotumika kukopeshea benki kutoka asilimia 16.0 hadi asilimia 12.0 Machi 2017 ili kuwezesha benki za biashara kupata fedha,<br>(ii) Kupunguza asilimia ya amana inayotakiwa kubaki Benki Kuu kwa amana kutoka Sekta Binafsi kutoka asilimia 10 hadi 8.0 ili kuziwezesha benki kuwa na kiwango cha kutosha cha ukwasi.<br><br>Matokeo ya hatua hizo ni pamoja na:<br>(i) Kupungua kwa riba za amana za muda maalum kutoka wastani wa asilimia 9.3 hadi wastani wa asilimia 8.7;<br>(ii) Viwango vya riba za amana za mwaka mmoja (1) vilipungua kutoka wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2015 hadi wastani wa asilimia 11 mwaka 2016. |
| 20(f) | Kutekeleza Sera na Sheria za kusimamia mapato yanayotokana na gesi asilia na mafuta ili kuhakikisha | Mwaka 2016, Serikali ilikamilisha maandalizi ya Kanuni zinazotoa mwongozo wa ukokotoaji wa bei ya gesi asilia na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | fedha zinatumika kwa manufaa ya Wananchi wa kizazi hiki na kijacho. | 285). |
| 20(g)(i) | Kuongeza ufanisi wa shughuli za minada kwa njia ya simu na mtandao wa intaneti. | Serikali iliweka mwongozo wa kusimamia kampuni zinazotoa huduma za kielektroniki kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wa wananchi katika kununua na kuuza hisa kupitia simu za mikononi. Hadi kufikia Julai 2017, idadi ya wawekezaji katika masoko ya hisa ilifikia 510,965, sawa na ongezeko la wawekezaji 91,437 ikilinganishwa na wawekezaji 419,528 mwaka 2016. |

## *2.1 Kilimo na Ushirika*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akilijaribu trekta mojawapo katika kiwanda cha kutengeneza matrekta aina ya URSUS kilichopo Kibaha mkoani Pwani.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akiongoza zoezi la upandaji miwa katika mradi wa Mkulazi II katika shamba la Gereza la Mbigiri, Morogoro*

Katika kutekeleza maelekezo ya Ilani kwenye sekta ya Kilimo, Serikali imeimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, huduma za ugani, umwagiliaji, upatikanaji wa masoko na kuhamasisha sekta binafsi na vyama vya ushirika kanzisha viwanda vya

kusindika mazao ya kilimo. Maelezo ya kina juu ya utekelezaji huo ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 2.

***Bangokitita 2: Mafanikio Katika Sekta za Kilimo na Ushirika***

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 22 (a) | Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa hususan katika kuboresha mifumo ya utoaji wa ruzuku na pembejeo pamoja na kuwaunganisha wakulima na Benki ya Maendeleo ya Kilimo na taasisi nyingine za fedha. | **Pembejeo za Kilimo**<br>(i) Serikali imewezesha Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agricultural Seed Agency-ASA) kuzalisha mbegu bora za Nafaka na Mikunde tani 2,804 mwaka 2015/2016 na tani 2,884 mwaka 2016/2017.<br>(ii) ASA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imezalisha tani 2,456 za mbegu za mahindi katika shamba la Mbozi mwaka 2015/2016 na tani 1,141 mwaka 2016/2017.<br>(iii) Mwaka 2015/2016, ASA kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza ilizalisha miche bora ya matunda 25,341 na vipando bora vya muhogo 10,525,210 na mwaka 2016/2017 miche bora ya matunda 20,435 na vipando bora vya muhogo 12,772,210 ilizalishwa.<br>(iv) Upatikanaji wa mbolea kwa wakulima ulifikia tani 302,450 mwaka 2015/2016 sawa na asilimia 62.3 na tani 297,000 mwaka 2016/2017 sawa na asilimia 61.2 ya mahitaji ya mbolea ya tani 485,000 kwa mwaka.<br>**Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo**<br>(i) Mwaka 2015/16, Serikali ilitoa ruzuku ya mbegu bora za mahindi na mpunga tani 10,270.86 na mbolea tani 99,993 na kunufaisha kaya za wakulima 999,926 kwa utaratibu wa |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | vocha. Serikali iliingia makubaliano na kampuni za mbegu na kuuza mbegu bora za mahindi na mpunga tani 3,731.5 kwa kaya 378,900.<br><br>(ii) Ruzuku ya kuzalisha miche bora ya chai na miche bora ya kahawa imeongezeka kutoka miche ya chai 1,600,000 na kahawa miche 2,106,510 mwaka 2015/16 hadi miche bora ya chai 7,100,000 na kahawa 2,412,805 mwaka 2016/2017.<br><br>(iii) Ruzuku ya viuatilifu vya zao la korosho tani 8,011 na vya pamba ekapaki 1,244,075 vimetolewa mwaka 2015/2016 na kwa mwaka 2016/2017, viuatilifu vya pamba ekapaki 1,803,586 na vya korosho tani 19,414.54 vimetolewa<br><br>**Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja**<br>Kanuni za Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja za mwaka 2017 na mwongozo wa utekelezaji zimeandaliwa kwa madhumuni ya kuongeza upatikanaji na kupunguza bei za mbolea kwa asilimia 30. Mfumo huo umeanza kutumika katika msimu 2017/2018 ambapo hadi Septemba 2017 jumla ya tani 55,000 zimeingizwa nchini.<br><br>**Udhibiti wa ubora wa pembejeo**<br>Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) imekagua Hekta 15,106 za mashamba ya kuzalisha mbegu, sampuli 3,863 za mbegu zilichukuliwa na kupimwa na maduka 380 ya wafanyabiashara wa mbegu yalikaguliwa. Aidha, tani 588,943 zilizoingizwa na tani 158,159 za mbolea zilizosafirishwa nje zilikaguliwa na |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | wafanyabiashara wa mbolea 400 na mawakala 1,648 kusajiliwa.<br><br>**Kuimarisha upatikanaji wa zana za kilimo.**<br>Kipindi cha Novemba 2015 na Septemba 2017 jumla ya matrekta makubwa 1,894 na matrekta ya mkono 336 yaliingizwa nchini na sekta binafsi. Pia, Serikali imenunua mashine za kisasa 14 za kusindika mpunga zenye uwezo wa kukoboa kati ya tani 5 hadi 30 kwa siku kwa skimu 13 za umwagiliaji nchini. |
| 22(b) | Kutoa elimu kwa wakulima juu ya Kanuni Bora za Kilimo kwa kuongeza idadi ya maafisa ugani kutoka 9,558 waliopo sasa hadi kufikia 15,082 mwaka 2020. | (i) Idadi ya Maafisa Ugani imeongezeka kutoka 9,558 mwaka 2015 hadi 13, 532 mwaka 2017. Kati ya hao, 8,232 ni Maafisa Ugani wa Sekta ya Kilimo, 4,283 Mifugo, 493 Uvuvi na 524 ni Maafisa Ushirika.<br><br>(ii) Vituo vya Mafunzo ya Kilimo na Mifugo vya Kata vimeongezeka kutoka 147 mwaka 2015 hadi 322 kufikia Juni, 2017, sawa na ongezeko la asilimia 54.3. |
| 22(d) | Kuboresha Mfumo wa Utafiti wa Kilimo nchini ili matokeo ya tafiti hizo yawafikie wakulima. | Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) imepitishwa na Bunge, kusainiwa na Rais na kutangazwa katika gazeti la Serikali. Taasisi hiyo itasaidia kuboresha mfumo wa utafiti wa kilimo nchini. |
| 22(d)(i) | Kugundua na kutathmini aina za mbegu bora za mazao mbalimbali zenye sifa ya kutoa mavuno mengi, zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi na zenye viinilishe vingi. | Vituo vya Utafiti wa Mbegu vya Serikali na Taasisi Binafsi za kilimo vimegundua na kuidhinisha mbegu bora 35 zinazotoa mazao mengi na kustahimili ukame (21 kutoka vituo vya utafiti na 14 kutoka Taasisi Binafsi) za mazao ya Mahindi tisa, Mpunga mbili, Karanga tatu, Korosho 16; Maharage mbili; na Viazi vitamu tatu. |
| 22(d)(ii) | Kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali kwa kushirikiana | Mbegu Mama na za Awali zimezalishwa kwa mazao ya Pamba tani 23.2; Viazi |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | na Taasisi za Umma na Binafsi ili kutosheleza mahitaji ya uzalishaji wa mbegu bora nchini. | mviringo miche 60,000; na tani 5.1 za nafaka (Mpunga, Mahindi na Ngano) tani 15.8. Mikunde (Soya na Maharage) tani 45.8; Migomba miche 1,830; na Parachichi miche 3,390. |
| 22(d)(v) | Kuboresha miundombinu ya utafiti na kuwajengea uwezo watafiti ili kuongeza ufanisi wa utafiti nchini. | (i) Maabara nne za kupima udongo katika vituo vya utafiti vya Selian, Mlingano, Uyole na Ukiliguru vimeboreshwa kwa kupatiwa Mashine zinazoweza kupima udongo kwa haraka na kwa bei nafuu.<br>(ii) Jumla ya watafiti 74 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ya shahada za kwanza, uzamili na uzamivu. Kati ya hao 27 ni wa shahada ya uzamivu (PhD). |
| 22(g)(ii) | Kuanzisha Soko la Bidhaa kwa mujibu wa Sheria ya Soko la Bidhaa (Commodity Exchange Act) Namba 15 ya mwaka 2015; | Soko la Mazao na Bidhaa *(Commodity Exchange)* limeanzishwa kwa mujibu wa sheria na Ofisi na Jukwaa la soko hilo zimefunguliwa katika jengo la LAPF lililoko Kijitonyama, Dar es Salaam. Kazi za uwekaji wa vifaa muhimu katika Ofisi na Jukwaa imekamilika. |
| 22(g)(iii) | Kujenga masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuwapa wakulima fursa ya kuuza mazao yao nje ya nchi | Ujenzi wa masoko na maghala ya kimkakati yanaendelea kujengwa katika mipaka ya Mulongo, Sirari, Kabanga, Kahama na Kyerwa – Nkwenda ili kudhibiti wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kuingia moja kwa moja mashambani na kununua mazao ya wakulima kwa bei ndogo.<br><br>Mfumo wa Stakabadhi za zao la Korosho Ghalani umeainishwa.<br>Aidha, Serikali imeongeza ushindani kwa wanunuzi wa ndani na nje wa Korosho jambo ambalo limeongezabei ya Korosho hadi kufikia **Shilingi 3,500** kwa kilo moja ikilinganishwa na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma. |
| 22(g)(iv) | Kuviimarisha na kuviwezesha vyama vya ushirika kuwa na uwezo wa kutafuta | (i) Vyama Vikuu vya Ushirika wa Korosho vya TANECU, MAMCU, RUNALI, Lindi Mwambao, TAMCU |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | masoko ya mazao ya wakulima ya ndani na nje kwa kuweka mfumo madhubuti wa ukusanyaji, uchambuzi na uenezaji wa taarifa za masoko na kutoa elimu juu ya uongezaji thamani na biashara. | na CORECU vimesimamiwa kupata masoko na bei nzuri ya korosho kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Katika msimu wa 2017/18, viliuza korosho na kuwalipa wakulima jumla ya **Shilingi bilioni 809.18**.<br>(ii) Vyama 10 vya Ushirika vya Wabanguaji Wadogo wa Korosho katika mkoa wa Tanga vimesimamiwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na kuuza korosho Tani 791 katika nchi za nje.. |
| 22(h) | Kuhamasisha Sekta Binafsi na Vyama vya ushirika wa mazao kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo hususan kwenye maeneo ya uzalishaji wa mazao hayo kwa lengo la kuongeza thamani na kuongeza ajira. Aidha, kuwawezesha wakulima kupata majokofu ili kuhifadhi matunda na mazao ya mboga mboga yanayoharibika haraka pamoja na vifungashio. | (i) Vyama 20 vya Ushirika wa Wafugaji Tanga, wanachama wa Chama Kikuu (TDCU) kupitia umiliki wa hisa asilimia 42.5 ya kiwanda cha Tanga Fresh Ltd imenunua Mtambo wa usindikaji wa maziwa kwa teknolojia ya muda mrefu UHT. Kupitia mtambo huo usindikaji wa maziwa unatarajiwa kuongezeka na kufikia lita 40,000 kwa siku.<br>(ii) Chama cha Ushirika wa Masoko na Mazao Chato AMCOS cha Mkoani Geita kimekabidhiwa kiwanda cha kuchakata na Kuzalisha Mafuta ya Alizeti chenye uwezo wa kuzalisha lita 700 za mafuta kwa siku. |

## 2.2 Mifugo na Uvuvi



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (wa nne kushoto), akiangalia ndama wakinywa maziwa kwenye shamba la mifugo la Kitulo, wilayani Makete, Njombe.*



*Serikali kupitia Mradi wa kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria awamu ya pili (LVEMP II) imeendelea kudhibiti magugu maji na kuboresha mazingira. Wavuvi wakiwa na mitumbwi yao kwenye mwalo wa Nyamirembe, wilayani Chato ambao unasimamiwa na mradi huu*

Sekta ya mifugo na uvuvi imeimarishwa ili kuwaongezea wafugaji na wavuvi kipato na kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 3.

Bangokitita Na. 3: Mafanikio Katika Sekta za Mifugo na Uvuvi

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 25 (a) | Kuongeza uzalishaji wa mitamba kwenye mashamba inakozalishwa na kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuendelea kuzalisha mitamba ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa. | Jumla ya Mitamba 1,280 imezalishwa katika kipindi cha 2015/2016 hadi 2016/2017. |
| 25(b) | Kutenga, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji nchini ili kuongeza maeneo ya ufugaji yaliyopimwa kutoka hekta milioni 1.4 za sasa hadi hekta milioni 5.0 mwaka 2020. | Serikali imetenga Hekta 519,918.38 kuwa maeneo ya ufugaji kwenye vijiji 80 katika Wilaya 17 za mikoa 11 na kufanya jumla ya eneo lililotengwa hadi sasa kufikia hekta milioni 2.535 katika vijiji 728. Jumla ya hati za kumiliki ardhi kimila 44 zimetolewa kwa wafugaji katika Wilaya za |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Monduli, Ngorongoro, Hanang, Simanjiro na Karatu. |
| 25 (c) | Kujenga miundombinu ya mifugo kwa kuongeza idadi ya malambo kutoka 1,378 yaliyopo sasa hadi 2,000 na kujenga mabwawa katika mikoa yenye mifugo mingi. Aidha, vitajengwa visima virefu 300, majosho 50 na kuanzisha minada 164 ya mifugo katika maeneo yote yatakayotengwa kwa ajili ya ufugaji ili kuzuia kuhamahama kwa wafugaji kunakosababisha migogoro. | Serikali imekamilisha ujenzi wa mabwawa **matatu** (**3**) ya Masusu (Ngorongoro), Olyapasei (Kiteto) na Kwamaligwa (Kilindi). Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakamilisha ujenzi wa malambo **1,381** na visima virefu **101** katika maeneo mbalimbali nchini. |
| 25 (e) | Kuanzisha mashamba darasa ya malisho katika kila Halmashauri ya Wilaya ili wafugaji wa asili wajifunze jinsi ya kuboresha na kuhifadhi malisho (feed banks) hususan wakati wa kiangazi na ukame. | Mashamba darasa **mawili** ya uzalishaji malisho yamenzishwa katika Halmashauri za Bunda na shamba **moja** katika Halmashauri za Busega, Kiteto na Igunga ambapo kila shamba darasa lina ukubwa wa Hekta **10**. |
| 25(h) | Kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji katika kuboresha ukosefu za mifugo nchini kwa kutoa huduma za uhimilishaji kwa wafugaji kwa gharama nafuu kupitia ruzuku itakayowekwa katika mbegu za uhimilishaji. | Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kilichoko Usa River Arusha kimetoa mafunzo kwa wahimilishaji **264** kuhusu teknolojia ya uhimilishaji katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017. Katika mwaka 2016/2017, Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa kimezalisha dozi **100,000** za mbegu bora za mifugo. |
| 25(i) | Kuboresha huduma za uhimilishaji kwa kuimarisha vituo vya uhimilishaji vya Taifa vya NAIC- Usa River (Arusha) na Sao Hill (Iringa); na vituo vya Kanda vya Kibaha (Mashariki), Lindi (Kusini), | Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji- NAIC kimepatiwa vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na "*Chiller*" kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha hewa baridi ya Nitrojeni. Ng'ombe waliohimilishwa Katika kituo cha NAIC wameongezeka kutoka **221,390** mwaka |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | Mbeya (Nyanda za Juu Kusini), Dodoma (Kati), Mwanza (Ziwa) na Mpanda (Kusini Magharibi) ili kusogeza karibu huduma ya uhimilishaji kwa wafugaji na kujenga vituo vipya vya uhimilishaji vya Kanda vya Tabora (Magharibi) na Tanga (Mashariki). | 2015/2016 hadi ng'ombe **457,557** mwaka 2016/2017. Vituo vingine vya Kanda vimepatiwa vitendea kazi na ukarabati wa miundombinu na mitambo ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya uhimilishaji wakati wote. |
| 25 (j) | Kuendelea kukuza na kuendeleza masoko ya mifugo na mazao yake yanayozalishwa na wafugaji na kujenga viwanda viwili (2) vya ngozi katika mikoa ya Singida na Dodoma. | Serikali imeanzisha minada 12 ya upili ambapo, minada 11 kati ya hiyo ni ya mipakani (border livestock markets) na Halmashauri za Serikali za Mitaa zimeanzisha minada ya awali 445. |
| 25(k) | Kuendelea kutoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo kiasi cha lita milioni 1.0 ili kuhakikisha kuwa majosho 2,428 yaliyopo nchini yanatumika kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo hususan ugonjwa hatari wa Ndigana kali. Aidha, Serikali itatoa ruzuku ya Chanjo ya Ndigana kali (ECF) na kushirikisha Sekta Binafsi na wadau wengine kufufua majosho 150 na kujenga majosho mapya 200 katika mikoa yenye mifugo mingi. | Serikali imefanya Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku za dawa za kuogesha mifugo kwa lengo la kufanyia kazi upungufu uliojitokeza ili kuboresha huduma. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 25(l) | Kuendelea kununua na kutoa chanjo za magonjwa ya mlipuko yanayoathiri afya ya mifugo na binadamu na kuwezesha biashara ya mifugo katika soko la kimataifa, hususan Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Homa ya Bonde la Ufa (RVF) na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR). | Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na Serikali imenunua dozi 200,000 za chanjo ya CBPP na dozi 400,000 za chanjo ya PPR. Aidha, chanjo ya RVF imeendelea kufanyiwa majaribio na wataalam wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa chanjo hiyo hapa nchini. Vilevile, Wakala wa Maabara ya Veterinari (TVLA) ilitengeneza jumla ya dozi 118,000,000 za chanjo ya Mdondo wa kuku inayostamili joto ambazo zimesambazwa kwa wafugaji wa kuku katika mikoa yote ya Tanzania Bara. |
| | **Sekta ya Uvuvi:** | |
| **27(l)** | Kushirikiana na wadau wa ufugaji wa samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kujenga mabwawa ya kufugia samaki na kuongeza uzalishaji kutoka tani 10,000 hadi 50,000 kwa mwaka na kupanua wigo wa ajira kwa vijana. | (i) Mabwawa ya kufugia samaki yameongezeka kutoka **21,300** mwaka 2015 hadi **22,545** Juni, 2017;<br>(ii) Vitotoleshi (incubators) **15** vya samaki aina ya perege vyenye uwezo wa kuzalisha vifaranga **11,520,000** kwa mwaka vimewekwa katika kituo cha Kingolwira;<br>(iii) Jumla ya vifaranga vya samaki na Kambamiti **14,119,272** vimezalishwa na vituo vya Serikali na sekta binafsi;<br>(iv) Wafugaji wa samaki **15,000** wenye mabwawa **7,672** wamepata elimu juu ya uzalishaji samaki, utunzaji bora wa mabwawa na usalama wa mazingira ya ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa;<br>(v) Vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji vimeongezeka kutoka nane (8) hadi **13** Juni, 2017; |
| **27(n)** | Kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kupata vifaa vya uvuvi kwa bei nafuu. | Serikali imeongeza boti za uvuvi kutoka **10,507** mwaka 2015 hadi **11,284** Juni, 2017. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **27(p)** | Kuendelea kupambana na uvuvi haramu ili uvuvi uwe endelevu na wenye tija. | (i) Vikundi 25 vya Jamii vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (*Beach Management Units-BMUs*) vimeundwa;<br><br>(ii) Vituo **25** vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vimeimarishwa kwa kuvipatia vitendea kazi na kufanya ukarabati wa miundombinu katika vituo vya Kasanga (Rukwa), Buhingu (Kigoma), Mbambabay (Ruvuma) Kipili (Rukwa) ili viweze kufanya doria na kuendesha operesheni za kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi katika maeneo ya mipakani;<br><br>(iii) Operesheni zilizofanyika zimewezesha kukamatwa kwa zana haramu zikiwemo kokoro **695**, kamba za kokoro mita **100,920**, nyavu ndogo za makila **6,592**, nyavu ndogo za dagaa chini ya mm **8, 5,145**, nyavu za utali **3,865**, vyandarua **10**, mitungi ya gesi **74**, baruti **59**, detonators **105**, compressors **3**, kilo **41** za Urea, regulators **9**, jozi **44** za viatu vya kuogelea, na boti **232**. Pia, kilo **16,478** za sangara wachanga, kilo **16,557** za dagaa, kilo **140** za kaa, kilo **9** za majongoo bahari, na makombe 104 zilikamatwa.<br><br>(iv) Jumla ya watuhumiwa **241** walikamatwa na kesi zimefunguliwa mahakamani. |

## 2.3 Maliasili na Utalii





*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli, akiangalia meno ya tembo yaliyokamatwa na vyombo vya dola.*

*Mbuga ya wanyama Serengeti ni miongoni mwa mbuga kubwa hapa nchini ambayo ina samba wengi na ni kivutio kikubwa cha watalii.*

Maliasili na Utalii ni moja ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa na ajira kwa wananchi. Kwa kutambua umuhimu wa sekta hiyo, Serikali imetekeleza mikakati ya kulinda maliasili na kukuza utalii nchini. Maelezo ya kina juu ya utekelezaji huo ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 4.

Bangokitita Na. 4: Mafanikio Katika Sekta za Maliasili na Utalii

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 29(a) | Kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini kutoka 1,102,026 mwaka 2015 hadi 2,000,000 mwaka 2020 kwa kuwezesha Sekta Binafsi kuwekeza katika huduma za miundombinu ya utalii pamoja na kuendeleza Mkakati wa Kimataifa wa Utangazaji wa | (i) Idadi ya watalii imeongezeka kutoka 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,284,279 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 12 na kuliingizia Taifa Dola za Marekani bilioni 2. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali za kuboresha miundombinu ya utalii ikiwemo kukarabati kilometa 2,571.2 za |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | Utalii ili kuwavutia watalii wengi zaidi. | barabara zilizopo ndani ya hifadhi; njia za miguu zenye urefu wa kilometa 143.5 na kuweka makaravati 27 kwenye Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Udzungwa na Arusha. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro imekamilisha ujenzi wa Kituo cha doria cha Masamburai, Jengo la Makumbusho katika Bonde la Olduvai; ukarabati wa Kambi ya Mary Leakey. Ujenzi wa vituo vya Mang'ola Juu, Bonde la Faru na Engaruka unaendelea.<br>(ii) Serikali kupitia Bodi ya Utalii imeshiriki na kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania katika maonesho 11 ya WTM (Uingereza), ITB (Ujerumani) MITT (Urusi), COTTM (China), INDABA na WTM – Africa (Afrika Kusini), Dutch Expo (Uholanzi), OTM (India), ATM na MICE ARABICA (Dubai) na The Pearl of Africa Expo (Uganda). |
| 29(b) | Kuongeza msukumo katika utalii wa kihistoria kwa kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya malikale na kuyatangaza maeneo hayo. | Serikali imekarabati Boma la Mikindani, Gofu la kihistoria lililotumika kutoza ushuru wakati wa Utawala wa Mjerumani na nyumba aliloishi Dkt. Livingstone lililopo Mikindani na kuweka mipaka katika mji wa Mikindani. Aidha, Tembe la Dkt. Livingstone lililopo Kwihara, Tabora limeboreshwa. Vilevile, kambi na Makumbusho iliyokuwa ikitumiwa na Dkt Leakey katika kituo cha Olduvai imeboreshwa na kufanywa kituo cha utalii na miradi 66 ya kuendeleza utalii wa utamaduni imeanzishwa. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 29(c) | Kuongeza bajeti ya Sekta ya Utalii ili kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi. | Katika mwaka wa fedha 2017/18, bajeti imeongezeka na kufikia Shilingi 6,607,062,566 ikilinganishwa na Shilingi 4,157,908,000 zilizotengwa mwaka 2016/2017 na Shilingi 4,331,494,000 mwaka 2015/16. |
| 29(g) | Kuendelea kujenga mazingira bora ya kuwawezesha vijana kuanzisha kampuni za kutembeza watalii katika maeneo mbalimbali ya utalii. | Serikali imetenga baadhi ya shughuli za utalii kwa ajili ya wazawa pekee. Shughuli hizo ni pamoja na kupandisha watalii kwenye milima (*mountain climbing*), ukodishaji magari ya kitalii, ukatishaji tiketi za ndege na uongozaji wa watalii. |
| 29(h) | Kuhifadhi malikale kwa kuishirikisha jamii kutumia Malikale kama chanzo cha kujipatia kipato kwa kutoa elimu ya ujasiriamali, kutenga maeneo ya biashara, kuishirikisha sekta binafsi na kutoa elimu ya uhifadhi kwa umma. | Serikali imefanya ukarabati wa Boma la Mjerumani lililopo Mkoani Iringa lililojengwa mwaka 1900 na kulifanya kuwa Makumbusho ya Mkoa wa Iringa na Kituo cha Utamaduni ambapo shughuli mbalimbali za utalii na biashara za vitu asili zinaendelea. |
| 31(a) | Kuendelea kujenga mahusiano mema baina ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo kwa namna ambayo wananchi hao watanufaika na uwepo wa hifadhi hizo. | Serikali imejenga maktaba mbili (2), maabara tano (5), madarasa 12, ofisi tisa (9), mabweni mawili (2), nyumba za walimu tatu (3) na kununua madawati 13,250 katika vijiji mbalimbali vilivyopo karibu na hifadhi. Pia, imejenga nyumba tatu (3) za wauguzi, zahanati mbili (2), kuchimba malambo mawili na kisima kimoja kirefu pamoja na ununuzi wa mtambo wa kusukuma maji na kuwezesha vikundi 20 vya wavuvi kupata taa 200 zinazotumia nishati ya jua. |
| 31(b) | Kutatua migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo ya jirani na hifadhi kwa | Serikali imehakiki mipaka yote ya maeneo ya hifadhi na kuweka alama za kudumu na mabango ya tahadhari. Hadi mwezi Mei, |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kushirikisha wadau katika kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za kudumu; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi; na kuzingatia utawala wa Sheria katika kusimamia rasilimali za maliasili. | 2017 vigingi 14,755 vimesimikwa, sawa na aslimia 62.4 ya vigingi 23,638 vinavyohitajika katika Hifadhi za Misitu, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro. Aidha, vijiji 48 vilivyopo karibu na hifadhi na mapori ya akiba vimewezeshwa kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Vijiji hivyo vipo katika Wilaya za Ludewa, Madaba, Makete, Mufindi, Njombe Mjini, Njombe Vijijini, Kilolo na Nyasa. |
| 31(c ) | Kuboresha miundombinu ndani ya Mapori ya Akiba na Vikosi dhidi ya ujangili na kuongeza vitendea kazi vya kisasa kwa ajili ya doria na upelelezi nje na ndani ya maeneo ya hifadhi. | Serikali imeimarisha vikosi vya kupambana na ujangili kwenye Kanda 8, kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro na mapori ya akiba nchini ikiwa ni pamoja na kuvipatia magari 58 ya doria. Pia imewezesha matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo ndege zisizo na rubani (*drones*) na mbwa wa kunusa ambao wamewekwa katika mipaka ya nchi na kwenye viwanja vya ndege na bandari ili kudhibiti utoroshaji wa nyara. |
| 31(e) | Kuendelea kuimarisha doria za ulinzi wa wananchi dhidi ya wanyamapori kwa kuboresha mfumo wa utoaji taarifa za wanyamapori waharibifu. Aidha, Serikali itaboresha na kutoa kwa wakati kifuta machozi kwa watu au familia zitakazoathirika kwa kiwango kinacholingana na athari zitakazotokea. | Serikali imefanya siku-doria 8,924 kwenye Wilaya 55 kwa ajili ya kuwalinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyama wakali na waharibifu. Hadi Mei 2017, jumla ya Shilingi 923,798,350 zimelipwa kwa wananchi katika wilaya 55 kwa ajili ya kifuta jasho (Shilingi 797,138,350) na kifuta machozi (Shilingi 126,600,000). |
| 31(f) | Kuongeza eneo la kupanda miti kutoka hekta 60,000 mwaka 2015 hadi hekta 130,000 | Jumla ya Hekta 24, 241 zimepandwa miti sawa na asilimia 58 ya lengo la Hekta 42,000 hadi kufikia Mei, 2017. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | mwaka 2020 na kuhakikisha kwamba mbao zinazovunwa zinatumiwa kwa ajili ya kutengeneza samani na matumizi mengine hapa nchini badala ya kusafirisha magogo nje ya nchi. | |
| 31(g) | Kuweka utaratibu wa wazi utakaowawezesha wananchi wanaoishi jirani na hifadhi kufaidika na rasilimali hizo. | Jumla ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori WMAs 38 zimeanzishwa na uhamasishaji unaendelea. Aidha, kupitia uwezeshaji wa Mfuko wa Misitu Tanzania, miradi 254 ya kuboresha kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu imetekelezwa. Miradi hiyo ni ya ufugaji nyuki ambapo vikundi vya ufugaji nyuki 399 na watu binafsi 27 wamewezeshwa kupata mizinga ipatayo 11,730. |
| 31(i) | Kupambana na ujangili wa wanyama pori wakiwemo Tembo na Faru. | Doria-siku 660,486 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 7,085 kwa makosa mbalimbali yakiweno kukutwa na meno ya tembo 129 na vipande 95 vyenye uzito wa jumla ya kilo 810.03; silaha za kivita 48, silaha za kiraia 150, risasi 1,058, magobore 406, silaha za jadi 22,307 na roda 120,538; pikipiki 189, baiskeli 214, magari 20; ng'ombe 79,831 na kilo 4,043 za samaki. Kutokana na doria hizo, kesi 2,097 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali ambapo kesi 802 zilimalizika; kesi 262 zenye watuhumiwa 472 zilimalizika kwa wahusika kufungwa jela; kesi 43 zenye watuhumiwa 79 kuachiwa huru, kesi 276 zenye watuhumiwa 469 kulipa faini ya jumla ya Shilingi 452,141,862 na kesi 966 zinaendelea katika Mahakama mbalimbali nchini. |

## 2.4 *Viwanda na Biashara*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akifungua kiwanda cha madawa cha Prince Pharmaceuticals kilichopo Buhongwa nje kidogo ya Jiji la Mwanza.*



*Waziri wa Nchi (OWM) Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, na Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango, wakiangalia viatu vilivyotegenezwa na kiwanda cha Gereza la Karanga, Moshi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Anna Mghwira. Kiwanda hicho ni miongoni mwa uwekezaji unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika sekta hii.*

Azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha uchumi unakua kwa kasi na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda. Katika kujenga uchumi wa viwanda, Serikali imehamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Maelezo ya kina juu ya mafanikio hayo ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 5.

Bangokitita Na. 5: Mafanikio Katika Sekta za Viwanda na Biashara

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 22 (h) | Kuhamasisha Sekta Binafsi na Vyama vya ushirika wa mazao kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo hususan kwenye maeneo ya uzalishaji wa mazao hayo kwa lengo la kuongeza thamani na kuongeza ajira. Aidha, kuwawezesha wakulima kupata majokofu ili kuhifadhi | (i) Kiwanda cha *Vegeta Padravka Limited* kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani kimewekeza katika ukaushaji wa mbogamboga kwa ajili ya kutengeneza vionjo vya chakula (*food seasoning)*. Uzinduzi wa kiwanda hicho ulifanyika Machi, 2017 na kinatarajia kuwekeza **Shilingi bilioni 9.9** na kutoa **ajira 63** za moja kwa moja. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | matunda na mazao ya mboga mboga yanayoharibika haraka pamoja na vifungashio. | (ii) Viwanda vya kuzalisha vifungashio vimejengwa kikiwemo Kiwanda cha *Lakairo Polybag* Jijini Mwanza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 4** chenye uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi (polypropylene bags) milioni 10 kwa mwaka na kuajiri watu 85; Kiwanda cha *Global Packaging* kilichopo Kibaha kimewekeza **Shilingi bilioni 8** na uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi **milioni 11.75** kwa mwaka na ajira ya watu 110. |
| 25 (p) | Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya nyama na mazao mengine yatokanayo na mifugo ikiwemo jibini na ngozi hususan katika maeneo yenye mifugo mingi ili kuongeza thamani. | (i) Kampuni ya *Watercom Ltd* imejenga Kiwanda cha Kusindika Maziwa eneo la Kigamboni, Mkoa wa Dar-es-Salaam ambacho kitatumia teknolojia ya *Ultra Heat Treatment* (UHT) ambayo huzalisha maziwa yenye ubora wa hali ya juu. Kiwanda hicho kimewekeza Dola za Marekani milioni 20 sawa na Shilingi bilioni 44 na kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 67.5 za maziwa kwa mwaka na kutoa ajira 500.<br><br>(ii) Eneo la ekari 6,000 limepatikana kwa ajili ya kuanzisha Kiwanda cha Nyama cha *Nguru Hills Ranch* eneo la Makunganya Wilaya ya Mvomero Mkoa wa Morogoro. Shilingi bilioni 30.23 zimekwishawekezwa. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kusindika nyama ya ng'ombe 50,000 na mbuzi 60,000 kwa |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | mwaka, kutoa ajira za moja kwa moja 350 na kutoa fursa ya ajira zisizo za moja kwa moja ikiwemo kilimo cha nafaka na majani maalum kwa ajili ya kulishia mifugo.<br>(iii) Kiwanda cha Nyama cha *Meat King Limited* kilichopo eneo la Moshono, Mkoa wa Arusha kimewekeza Shilingi bilioni 5.5 kwa ajili kusindika nyama ya ng'ombe, kuku na kondoo. Kiwanda hicho kinatoa ajira 45 za moja kwa moja na 500 zisizo za moja kwa moja.<br>Kwa ujumla, idadi ya viwanda vya nyama imeongezeka kutoka 25 mwaka 2015 hadi viwanda 33 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 32. |

## *2.5 Madini*





*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akipokea Taarifa ya Tume ya Uchunguzi wa mchanga wa madini (Makinikia) kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume hiyo Prof. Abdulkarim Hamis Mruma, Ikulu Jijini Dar es Salaam.*

*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akipokea Taarifa ya Kamati Maalum ya Bunge ya Kuchunguza Biashara ya Tanzanite na Almasi kutoka kwa Spika wa Bunge, Mhe. Job Ndugai, mjini Dodoma.*

Serikali imeweka na kusimamia mfumo thabiti wa kukagua shughuli za migodi, kuhamasisha uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya madini na kukomesha vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje pamoja na kuwawezesha wachimbaji wadogo.

Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 6.

Bangokitita Na. 6: Mafanikio Katika Sekta ya Madini

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 35 (a) | Kuweka na kusimamia mfumo thabiti wa kukagua shughuli za migodi, kukusanya takwimu za madini na kufuatilia maduhuli yatokanayo na madini kwa malengo mapana ya kuongeza mapato ya Serikali. | (i) **Ukaguzi wa Uzalishaji wa Mauzo ya Madini kutoka Migodi Mikubwa Nchini**<br><br>Kwa kipindi cha kuanzia Novemba 2015 hadi Julai 2017, jumla ya sampuli 8,497 za mikuo ya dhahabu na makinikia ya shaba (*copper concentrat*e) kutoka kwenye migodi mikubwa zilifanyiwa uchunguzi kwenye Maabara ili kujua kiasi na thamani ya madini yaliyozalishwa na kuuzwa nje. Ukaguzi ulifanywa katika Migodi ya TanzaniteOne na Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka. Kaguzi zimeiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa jumla ya **Dola za Marekani 6,994,696.01**.<br><br>(ii) **Ukaguzi wa Madini ya Kimkakati *(Strategic Auditing)***<br><br>Serikali imekagua uzalishaji na mauzo ya madini ya ujenzi na viwandani katika Mikoa mingi nchini na kuwezesha malipo ya mrabaha wa **Shilingi bilioni 9.97.** Mrabaha huo unatokana na uzalishaji na mauzo ya Tani milioni 20.69 za madini ya ujenzi na viwandani yenye thamani ya **Shilingi bilioni 324.28.**<br><br>Ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na mauzo ya dhahabu kutoka kwa wazalishaji wanaotumia teknolojia ya "*vat leaching*" kuchenjua marudio katika Mikoa ya Mbeya, Mwanza, Geita, Shinyanga na Tabora umefanyika. Jumla ya **kilo 2,500.7** za dhahabu |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | zenye thamani ya **Shilingi bilioni 182.45** zilizalishwa na wamiliki halali wa leseni katika maeneo hayo. Ukaguzi huo umewezesha malipo ya mrabaha wa kiasi cha **Shilingi bilioni 7.30.** Ukaguzi umefanyika pia kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu katika Wilaya za Chunya, Geita na Mpanda ambapo jumla ya **Kilogramu 48.68** za dhahabu na **mifuko 100,287** ya mawe yenye madini ya dhahabu yenye thamani ya **Shilingi bilioni 6.02** ilizalishwa na wachimbaji hao na fedha **Shilingi milioni 244.02** zilikusanywa kama mrabaha. |
| 35(e) | Kuboresha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini, na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wadau kuhusu Sekta ya Madini. | Mfumo wa *Online Mining Cadastre Transactional Portal* (OMCTP) ambao unaruhusu kuomba leseni za madini na kufanya malipo kwa njia ya mtandao, hivyo kuongeza uwazi na kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wadau wa Sekta ya Madini kwa wakati umeanzishwa. |
| 35(g) | Kuendelea kuliimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na utoaji huduma katika Sekta ya Madini kwa niaba ya Serikali na Watanzania wote. | Serikali imeliimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa kulipatia rasilimali watu, fedha na vifaa na imeanza kutekeleza yafuatayo:-<br><br>(i) Uchimbaji wa Makaa ya Mawe katika Kilima cha Kabulo – Kiwira ambapo hadi sasa Jumla ya **tani 6,197** zimechimbwa.<br><br>(ii) Wakia **30,699.50** zilizalishwa kwenye mgodi wa STAMIGOLD na kuuzwa na jumla ya **Shilingi bilioni 37.2** zimepatikana.<br><br>(iii) Kupitia Mgodi wa Ubia wa Tanzaniteone, jumla ya **kilo 569.53** za madini ya Tanzanite zilizalishwa na |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | mauzo kufikia jumla ya **Shilingi bilioni 32.**<br><br>(iv) Kufanya utafutaji wa awali wa madini ya *rare earth elements* katika eneo la Sengeri, Songwe.<br><br>(v) Kuendelea kufanya utafutaji wa awali wa madini ya Phosphate katika eneo la Mvomero.<br><br>(vi) STAMICO kwa kushirikiana na GST imefanya utafiti wa kijiosayansi katika maeneo ya Katente, Mgusu, Kyerwa, Buhemba, Mafurungu, Ibindi/D-reef ambayo yatatumika kwa kujenga vituo vya mfano kwa ajili ya wachimbaji wadogo *(centre of excellences).* |
| 35(h) | Kuendelea kuujengea uwezo wa kifedha na rasilimali watu Wakala wa Jiolojia Tanzania ili uweze kufikia kiwango bora zaidi katika ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu za kijiolojia na kijiofizikia zitakazosaidia katika kuchochea kasi ya utafutaji na upatikanaji wa mashapo ya madini hapa nchini yanayoweza kuchimbwa kwa faida. | Mwaka 2016/17, Serikali iliipatia Wakala wa Joilojia shilingi **4,831,204,000** ikiwa ni ongezeko la asilimia **8** ikilinganishwa na shilingi **4,433,482,000** zilitolewa mwaka 2015/16. Kutokana na bajeti hiyo Wakala ulitekeleza yafuatayo:<br><br>(i) Kufanya utafiti wa kina wa Jiosayansi ulioainisha wingi wa mashapo ya madini kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo, katika maeneo ya Katente-Geita; Itumbi –Chunya; D-reef na Kapanda- Mpanda; Kyerwa; Buhemba-Musoma na Tanga;<br><br>(ii) Kununua vifaa vya kisasa vinavyowezesha utengenezaji wa vyungu vya kuchomea dhahabu - |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (*crucibles*) 17,286 na *cupels* 12,261;<br><br>(iii) Kuchapisha ramani ya jiolojia inayoonesha uwepo wa madini mbalimbali katika maeneo ya Nachingwea, Tunduru na Masasi (ISBN 978-9987-765-19-5). Ramani hiyo inalenga kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini;<br><br>(iv) Kufanya utafiti wa jiolojia, jiokemia na visawe vya mbali (*remote sensing)* kwenye Wilaya za Mpwapwa na Kongwa ili kubaini maeneo mapya yenye madini ya metali *(base metal);* na<br><br>(v) Kufanya utafiti wa jotoardhi unaolenga kupata vyanzo vya nishati ya joto ardhi kwa ajili ya maeneo ambayo yako mbali na gridi ya taifa katika maeneo ya Takwa na Gonga wilayani Chemba. |
| 35(j) | Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ili kukuza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa. | Katika kipindi cha Novemba, 2015 hadi Julai, 2017 jumla ya leseni 55 za uchenjuaji madini zimetolewa. Serikali imesitisha usafirishaji wa madini ghafi na mbale ya madini nje ya nchi na imetangaza *Expression of Interest* ya kuwataka wawekezaji wa *smelter* na *refinery* kujitokeza kwa ajili ya kujenga mitambo hiyo hapa nchini. Jumla ya kampuni 25 zimeonesha nia na Serikali inaendelea na utaratibu wa kutafuta kampuni zitakazofaa kwa ajili ya ujenzi wa mitambo hiyo. |
| 35(k) | Kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi itakayowezesha | (i) Serikali imeanzisha madawati maalum ya ukaguzi wa vifurushi vya madini |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini. | vinavyosafirishwa nje ya nchi katika viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza, Songwe na Arusha; Bandari ya Dar es Salaam na Zanzibar, Mipaka ya Holili na Namanga.<br>(ii) Ukaguzi uliofanyika umewezesha kukamatwa kwa watoroshaji wa madini yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 1.3 na Shilingi Milioni 151.5 katika matukio 22 yaliyoripotiwa. |
| 35(l) | Kuweka na kutekeleza mikakati maalum itakayowezesha soko la Tanzanite hapa nchini kuimarika zaidi na hivyo kuongeza manufaa yatokanayo na madini hayo yanayopatikana Tanzania pekee. | Serikali imeandaa minada ya Tanzanite na Maonesho ya madini ya vito ikiwemo tanzanite ili kuwapatia soko la ushindani na la uhakika wachimbaji na wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite. Pia, Serikali imeanza ujenzi wa jengo la kudumu la kuendeshea biashara, maonesho pamoja na minada ya madini katika eneo la EPZ lililopo Mererani pamoja na ujenzi wa ukuta wa kuzunguka eneo lote la uchimbaji ili kudhibiti utoroshaji wa madini ya Tanzanite. |
| 35(m)(i) | Kuwatambua, kuwarasimisha na kuwapatia maeneo ya uchimbaji madini wachimbaji wadogo. | Jumla ya leseni 4,207 zenye ukubwa wa kilomita za mraba 74.10 zimetolewa kwa wachimbaji wadogo wa madini kote nchini. Aidha, jumla ya maeneo 11 yenye ukubwa wa hekta 38,951.88 yenye uwezo wa kutoa leseni za uchimbaji 3,895 yalitengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika Mikoa ya Kagera, Singida, Katavi, Ruvuma, Lindi, Tabora na Geita. |
| 35(m)(ii) | Kuwapatia wachimbaji wadogo ruzuku, mafunzo, teknolijia na maarifa ya kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji. | Jumla ya wachimbaji wadogo 2,000 walipatiwa mafuzo na semina kuhusu teknolojia mbadala za uchenjuaji dhahabu, usalama migodini, ujasiriamali, utunzaji kumbukumbu na utunzaji wa mazingira. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| 35(m)(iii) | Serikali kupitia STAMICO kwa kushirikiana na wachimbaji wakubwa kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mikopo na masoko. | (i) Mfumo wa Utoaji wa Taarifa za Masoko na Bei kwa wachimbaji wadogo *(Small scale mining Portal)* umeanzishwa na elimu ya utumiaji wa mfumo huo imetolewa kwa wachimbaji wadogo.<br><br>(ii) Serikali kupitia STAMICO imenunua madini ya bati yenye thamani ya Shilingi **Milion 327** kutoka kwa Wachimbaji wadogo wa madini hayo waliopo Wilayani Kyerwa, Mkoani Kagera.<br><br>(iii) Serikali kupitia STAMICO inawasaidia wachimbaji wadogo kwa kuwafanyia uchorongaji na utafiti wa madini na kuwaandalia taarifa za kijiolojia ambazo hutumika katika kuomba mikopo kwenye Taasisi za fedha. |

## 2.6 Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akisalimiana na wananchi baada ya kukagua eneo la ujenzi wa nyumba za makazi eneo la Magomeni Kota, Jijini Dar es Salaam*



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe.Wiliam Lukuvi akiwa na baadhi ya wakazi wa kijiji cha Nyange Wilaya ya Kilombero - Morogoro, baada ya kuwakabidhi Hatimiliki za kimila.*

Serikali inaendelea kutekeleza mipango ya kuendeleza ardhi ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo utakaorahisisha umilikishaji wa ardhi na uhifadhi wa kumbukumbu za ardhi kwa kukamilisha ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za

Ardhi, kuendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, kumamilisha uandaaji wa Mipango Kabambe kwa miji mikuu yote ya mikoa na kuzijengea uwezo Halmashauri katika kupima ardhi. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 7.

Bangokitita Na. 7: Mafanikio Katika Sekta za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 37(a)(i) | Kujenga mfumo utakaorahisisha umilikishaji wa ardhi na uhifadhi wa kumbukumbu za ardhi kwa kukamilisha ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System*). | Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi kumbukumbu za Ardhi Serikali umeanza kujengwa. Yafuatayo yamefanyika:-<br><br>(i) Mfumo unganishi umeanza kufungwa katika Halmashauri za Manispaa za Kinondoni na Ubungo Jijini Dar es Salaam. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika Juni, 2018 na baadaye Mfumo huo utafungwa katika Halmashauri zote nchini;<br><br>(ii) Kukamilisha ukarabati wa Jengo la Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (National Land Information Centre-NLIC) na hivyo kuanza kwa zoezi la “data conversion” ya nyaraka mbalimbali za Sekta ya Ardhi;<br><br>(iii) Kuimarisha Mfumo wa Kutunza Kumbukumbu za Ardhi (Management of Land Information System – MOLIS) na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Kanda kuhusu matumizi ya mfumo huo pamoja na uhakiki wa kumbukumbu za ardhi katika mfumo huo; na<br><br>(iv) Kusimika Mfumo wa Ukusanyaji |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | wa Kodi ya Pango la Ardhi (Government e-payment Gateway System) katika Halmashauri 31 nchini na hivyo kuwezesha kufanyika kwa malipo ya kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali kwa njia ya kielektroniki ikiwemo simu za mkononi; |
| 37(a)(ii) | Kuimarisha huduma za ardhi katika Kanda kwa kujenga majengo manane (8) katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Ziwa (Mwanza), Kaskazini (Moshi), Magharibi (Tabora), Kati (Dodoma), Kusini (Mtwara), Kanda ya Mashariki na Kanda ya Dar es Salaam inayohudumia mkoa wa Dar es Salaam. | Michoro ya ujenzi wa Ofisi za kanda saba (7) imeshaandaliwa na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea. |
| 37(a)(iii) | Kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi katika Kanda nane (8) za ardhi nchini kwa lengo la kuongeza kasi ya utoaji wa Hatimiliki za Kimila nchini. | Serikali imeendelea kuimarisha Ofisi za Kanda kwa kupeleka Wataalam wa kada mbalimbali ambapo kanda 5 za Mwanza, Dodoma, Mtwara, Tabora na Moshi zilipata jumla ya watumishi 21. Aidha, kila kanda imepatiwa gari jipya. |
| 37(a)(iv) | Kuzijengea uwezo Halmashauri za Miji na Wilaya kwa kuzipatia mafunzo, vifaa, rasilimali fedha na wataalam ili ziweze kupima viwanja na mashamba nchini. | Serikali imepeleka jumla ya Shilingi 2,283,332,800 katika Halmashauri hadi Agosti, 2017 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ardhi. |
| 37(a)(v) | Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi ili uweze kufidia ardhi | Serikali imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia ya Ardhi yenye jukumu la kufuatilia na kuratibu malipo yote ya fidia |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | itakayotwaliwa kwa matumizi ya umma na uwekezaji. | yatakayofanywa na Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Halmashauri. Aidha, Mwongozo wa namna shughuli za Mfuko wa Fidia ya Ardhi zitakavyofanyika umeandaliwa na kusambaza kwa wadau . |
| 37(a)(vi) | Kufanya uhakiki wa mashamba pori yasiyoendelezwa kwa kipindi kirefu na kugawa upya kwa wananchi. | Serikali imefanya ukaguzi wa mashamba ya uwekezaji **121** yenye ukubwa wa ekari **552,139.21** katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Njombe na Kagera na kuingiza taarifa zake katika kanzidata ya Serikali ambapo mashamba 58 yalibainika kutoendelezwa. Mashamba hayo pamoja na mengine yenye ukubwa wa ekari **429,654.16** yaliyopo katika mikoa ya Tanga, Pwani, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa na Dar es Salaam yamefutiwa umiliki na kurudishwa kwa halmashauri husika kwa ajili ya kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi na kuigawa kwa kuzingatia mahitaji ya ardhi yaliyopo katika eneo husika. Aidha, Serikali imepata ardhi ya ekari **5,288.49** kwa ajili ya uwekezaji kutokana na mashamba hayo yaliyofutwa umiliki. |
| 37(a)(ix) | Kuimarisha huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kuanzisha Mabaraza mapya 100 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi. | (i) Serikali imefungua Maabaraza ya Ardhi na Nyumba matatu (3) katika Wilaya za Kilindi, Lushoto na Kiteto na kufanya jumla ya Mabaraza yanayofanya kazi kufikia **53** kwa nchi nzima. Aidha, uteuzi wa Wenyeviti 18 na wajumbe 38 wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba umefanyika.<br><br>(ii) Nakala za Vitabu vya Mwongozo wa Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi zimegawiwa kwa Mabaraza ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Kata **108** katika mikoa 6 nchini. Vilevile, uamuzi kwa mashauri **32,123** kati ya mashauri **59,229** yaliyokuwa yanashughulikiwa umetolewa. |
| 37(a)(x) | Kuhakikisha maafisa ardhi wasio waaminifu wanashughulikiwa. | Serikali imewasimamisha kazi watumishi wanne, watumishi **16** walifukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali ya kiutendaji na watumishi **19** waliandikiwa barua za onyo na kutakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wa umma. |
| 37(a)(xi) | Kuanzisha akiba ya ardhi (*Land Bank).* | Mashamba **178** yaliyopo katika mikoa ya Arusha na Morogoro yameainishwa na kuingizwa kwenye akiba ya ardhi. Aidha, eneo lenye ukubwa wa ekari **83,080** limetengwa katika maeneo ya mipango kabambe katika halmashauri **14** nchini kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. |
| 37(b)(i) | Kuendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. | Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Ukanda wa SAGCOT na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji umefanyika ambapo **vijiji 1,731** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kati ya **vijiji 12,545** nchi nzima. |
| 37(b)(ii) | Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 7,500 na mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya 25. | Mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya tatu za Kilombero, Ulanga na Malinyi chini ya Mradi wa *Land Tenure Support Programme* na mipango ya **vijiji 154** katika **Wilaya 35** imeandaliwa na taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi ya **vijiji 56** ilipokelewa na kuhakikiwa. |
| 37(b)(iii) | Kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vyote nchini. | Vijiji **11,000** vimekwishapimwa nchini kati ya vijiji **12,545** nchi nzima hadi kufikia Agosti, 2017. |
| 37(b)(iv) | Kuwapatia wananchi hatimiliki | Jumla ya Hatimilki za kimila **69,208** |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | za **kimila 2,500,000** pamoja na kujenga masjala za **ardhi 250** katika ngazi za Wilaya na Vijiji. | zilikuwa zimeandaliwa na kutolewa kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini hadi Agosti, 2017. Aidha, ukarabati wa masjala za ardhi za vijiji **79** na tatu (**3**) za wilaya umekamilika na ujenzi wa masjala za ardhi ya kijiji za vijiji **42** vya Wilaya tatu (3) upo katika hatua za mwisho za ujenzi. |
| 37(b)(v) | Kuwapatia wananchi hati miliki **2,000,000** pamoja na kusajili nyaraka nyingine za kisheria. | Jumla ya Hatimiliki za **viwanja 82,633** na nyaraka za **kisheria 122,106** zilikuwa zimesajiliwa na kutolewa kufikia Agosti,2017 kwa wananchi. Aidha, jumla ya **makazi 240,000** ya mijini yametambuliwa na taratibu za urasimishaji zinaendelea. |
| 37(c)(i) | Kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kwa masharti nafuu. | Kufikia Agosti 2017, mikopo ya **Shilingi bilioni 416.94** imetolewa kwa wananchi **3,519** na muda wa kurejesha wa hadi miaka **20.** Aidha, Mfuko wa Mikopo Midogo Midogo ya Nyumba (*Housing Micro Finance Fund*) uliopo chini ya Benki Kuu ya Tanzania umeongezewa mtaji wa dola za Marekani milioni **18** ambapo benki za biashara tatu (**3**) zimechukua mtaji wa **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya kukopesha wananchi wa kipato cha chini kwa masharti nafuu. |
| 37(c)(iv) | Asasi za Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi zitajenga nyumba za gharama nafuu zisizopungua 50,000. | Jumla ya miradi ya nyumba za gharama **nafuu 14** yenye **nyumba 492** imekamilika na miradi **mingine 14** ya nyumba za gharama nafuu yenye **nyumba 1,002** inaendelea. Aidha, **Wadau 127** wa Sekta Binafsi wamejenga **nyumba 17,813.** |
| 37(c)(v) | Kuwawezesha wanavijiji kujiunga kwenye vikundi vya ujenzi vitakavyopatiwa elimu ya jinsi ya kujenga nyumba | Taarifa za Vyama vya Ushirika wa nyumba **32** zimeingizwa katika Kanzidata ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba. Vyama vinane kati ya 32 vimejenga |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | bora vijijini. | nyumba **655** katika maeneo mbalimbali nchini. |
| 37(c)(vi) | Kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwa Mwendelezaji Milki Mkuu (*Master Estate Developer*). | Shirika la Nyumba la Taifa limepewa dhamana ya kupanga na kuendeleza maeneo ya Kunduchi Rifle Range; Songwe; Ruvu; Pembamnazi; Chato na Kibondo; Shirika la Nyumba la Taifa linaendelea na ujenzi wa miji kadhaa ya kisasa nchini ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Kisasa Kawe (*Kawe Satellite City);* Mradi wa Safari City ulioko Mateves, Arusha; na Ujenzi wa nyumba 300 katika eneo la Iyumbu, Manispaa ya Dodoma upo katika hatua za mwisho za ujenzi. |
| 37(c)(x) | Kujenga nyumba za watumishi wa umma na majengo ya Serikali yenye kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu kwa:-.<br>Kuanza ujenzi wa majengo yatakayotumika kama Ofisi kwa taasisi za Serikali ili kuipunguzia Serikali gharama ya kodi kubwa ya pango katika soko huria. | (i) Ujenzi wa majengo ya Serikali unaofanywa na wakandarasi mbalimbali pamoja na taasisi za ujenzi za serikali (TBA, WHC, NHC pamoja na mifuko ya Hifadhi ya Jamii) unazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.<br><br>(ii) Serikali imetenga **Shilingi bilioni 200** katika mwaka wa fedha 2017/2018, kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali Dodoma ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa mzigo wa kodi ya pango kwa Serikali. |
| 37(c)(xii) | Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti na Uendelezaji wa Miliki (*Real Estate Regulatory Authority*) ambayo pamoja na majukumu mengine itasimamia udhibiti wa kodi za pango kwa nyumba za makazi na biashara. | Rasimu ya muswada wa kutunga sheria ya kuratibu na kusimamia sekta ya milki (*The Real Estate Bill, 2017*) imeandaliwa na inaendelea kujadiliwa katika ngazi mbalimbali za Serikali. |
| 37(d)(i) | Kukamilisha uandaaji wa | Mipango Kabambe ya Miji Mikuu ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Mipango Kabambe (*Master Plans*) kwa miji mikuu yote ya mikoa. | Mikoa minne ya Iringa, Mara, Mtwara na Singida imekamilika na kuidhinishwa. Aidha, Mipango Kabambe ya Miji Mikuu ya Mikoa ya Arusha, Mwanza, Pwani na Simiyu ipo katika hatua za mwisho za kuidhinishwa wakati ile ya Miji Mikuu ya Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Ruvuma ipo katika hatua za kukamilishwa. |
| 37(d)(ii) | Kuhimiza ujenzi wa miji ya pembezoni (*Satelite Cities*) katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na miji mingine ili kufanya miji hiyo ikue kwa kuzingatia Mipangomiji. | Mji wa pembezoni wa Luguruni katika Jiji la Dar es Salaam ambao umekabidhiwa kwa Shirika la Nyumba la Taifa umeanza kujengwa. Aidha, Halmashauri 35 zimetambua na kutenga maeneo kwa ajili ya miji ya pembezoni. |
| 37(d)(iv) | Kuendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi yaliyopo katika maeneo ambayo hayajapimwa kwa lengo la kuyapanga na kuyapima viwanja katika Miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Morogoro na Mbeya. Programu hii itatoa hatimilki za Makazi. | Kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na:<br>(i) Kupima viwanja 12,419 katika Jiji la Dar es Salaam ambapo hatua za umilikishaji zinaendelea;<br>(ii) Kupima viwanja 16,958 katika Jiji la Mwanza na kutoa hati kwa viwanja 6,958;<br>(iii) Kurasimisha viwanja 57,380 kwa nchi nzima;<br>(iv) Kubainisha viwanja 50,200 vitakavyo rasimishwa katika mwaka wa fedha 2017/18 katika halmashauri za Manispaa za Musoma, Kigoma Ujiji, Tabora, Singida, Sumbawanga na Lindi. |
| 37(d)(v) | Kuendeleza maeneo yaliyoiva (*re-development scheme*) ya Kipawa, Namanga, | Programu ya uendelezaji upya maeneo ya Kipawa, Buguruni, Msasani, Bonde la Mpunga na Kawe katika Jiji la Dar es |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Vingunguti, Manzese, Buguruni, Msasani Bonde la Mpunga na Kawe, Jijini Dar es Salaam. | Salaam imeandaliwa ambapo hadi Agosti, 2017 Mpango wa eneo la Buguruni ulikuwa umeidhinishwa na unatumika. |
| 37(e)(ii) | Kuimarisha alama za mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani za Kenya, Burundi, Zambia, Malawi, Uganda, Rwanda, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. | Utekelezaji ni kama ifuatavyo:-<br><br>(i) Tanzania na Kenya - upigaji picha za anga wa mpaka wenye urefu wa kilometa **756** umekamilika na picha hizo zitatumika kuandaa ramani za msingi;<br><br>(ii) Tanzania na Uganda – Mpaka wake una urefu wa kilometa **391.** Eneo la nchi kavu lenye urefu wa kilometa **149** limeainishwa;<br><br>(iii) Tanzania, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi katika Ziwa Tanganyika – Pande zote zimekubaliana namna ya kupima mipaka yao ndani ya maji;<br><br>(iv) Tanzania na Zambia - Mikutano miwili (2) ya kuimarisha mpaka wa nchi kavu wenye urefu wa kilomita **289** imeshafanyika katika ngazi ya Makatibu Wakuu;<br><br>(v) Tanzania na Malawi – Vikao vya usuluhishi chini ya usuluhishi wa Marais Wastaafu *Joackim Chisano, Rais Thabo Mbeki na Rais Festus Mogae* katika sehemu inayopita katika Ziwa Nyasa yenye |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | urefu wa kilometa **248 bado** vinaendelea;<br>(vi) Tanzania na Msumbiji - Alama za msingi 26 za mpaka zimekarabatiwa pamoja na kusimikwa alama **54** za kati ya mpaka. |

## *2.7 Ujenzi na Uchukuzi*



*Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Joseph Magufuli, akipeana mkono na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano mara baada ya kufungua barabara ya Biharamulo–Kagoma-Lusahunga yenye urefu wa kilometa 154, wilayani Biharamulo Mkoani Kagera, tarehe 19 Julai 2017.*



*Barabara ya Bagamoyo-Makofia-Msata yenye urefu wa kilometa 64 katika eneo la Daraja la Ruvu chini, Bagamoyo mkoani Pwani.*

Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara, madaraja, madaraja ya juu (flyovers), vivuko, ununuzi meli pamoja na kuanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini –TARURA. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa viwanja vya Ndege na ununuzi wa ndege pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na 8.

Bangokitita Na.8: Mafanikio Katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| **39(a)(i)** | **Kuimarisha Mfuko wa Barabara (Road Fund)**<br>Kubuni vyanzo vipya na kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya sasa ili kuongeza mapato. | Bodi ya Mfuko wa Barabara inafanya utafiti wa vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko unaotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2017. |
| **39(a)(ii)** | Kubuni/Kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kwamba thamani na ubora wa kazi unaendana na fedha zilizotumika (*value for money*) | Ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa kazi umeongezeka kutoka ukaguzi wa Halmashauri na Ofisi za Mikoa za Wakala wa Barabara 157 hadi ukaguzi wa Halmashauri na Ofisi za Mikoa za Wakala wa barabara 191. Aidha, thamani na ubora wa kazi umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 50.5 kwa mwaka 2014/2015 hadi asilimia 63.7 mwaka 2015/2016. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **39(a)(iii)** | Kuanzisha wakala/taasisi itakayosimamia kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara za miji na majiji na Halmashauri ambazo ziko chini yaTAMISEMI. | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Road Agency-TARURA) ulianzishwa. kwa tangazo la Serikali namba 211 lililotolewa katika gazeti la Serikali la tarehe 12/05/2017. |
| **39(b)(i)** | Kuunganisha makao makuu ya mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami na kujenga barabara kuu zote zinazounganisha Tanzania na nchi jirani kwa kiwango cha lami. | Mikoa ifuatayo imeunganishwa:<br>(i) **Mikoa ya Kigoma na Kagera**. Ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kidahwe – Kasulu (Km. 50) na Nyakanazi - Kibondo (Km. 50) unaendelea. Aidha, mapitio ya usanifu wa kina yanaendelea kwa sehemu iliyobaki ya Kibondo – Kasulu (Km. 258).<br>(ii) **Mikoa ya Kigoma na Tabora:** Ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kigoma – Kidahwe – Uvinza; Daraja la Kikwete (Malagarasi) ikiwa ni pamoja na barabara unganishi, barabara ya Tabora - Ndono – |

| | | |
|---|---|---|
| | | Urambo (Km. 94) na barabara ya Kaliua – Kazilambwa (Km. 58.9) umekamilika.<br><br>(iii) **Mikoa ya Tabora na Katavi:** Ujenzi wa barabara ya lami kwa sehemu ya Tabora - Sikonge (Usesula) Km. 30 unaendelea. Aidha, taratibu za kuwapata makandarasi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu iliyobaki ya Sikonge (Uselula) – Ipole – Koga - Mpanda (Km. 340).<br><br>(iv) **Mikoa ya Kigoma na Katavi:** Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Mpanda – Mishamo (Vikonge) Km. 35 amepatikana na ameanza kazi. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Uvinza – Magunga (Km. 65.5) ziko hatua za mwisho.<br><br>(v) **Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mwanza na Mara:** Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Bariadi – Lamadi Km. 71 umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea kwa sehemu ya Mwigumbi – Maswa (Km. 50.3). Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Maswa – Bariadi (Km. 49.7) amepatikana.<br><br>(vi) **Mikoa ya Mara na Arusha:** |

| | | |
|---|---|---|
| | | Ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Natta (sehemu ya Makutano – Sanzate Km. 50) unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Wasso (Loliondo) – Sale Junction (Km. 49) umeanza. Vilevile, Serikali inakamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Natta – Mugumu (Km. 43.2).<br><br>(vii) **Mikoa ya Rukwa na Katavi:** Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Sitalike – Mpanda (Km. 36.9) na Sumbawanga – Kanazi (Km. 75) na Kanazi – Kizi – Kibaoni (76.6) umekamilika. Pia Usanifu umekamilika kwa sehemu ya Sitalike – Kibaoni.<br><br>(viii) **Mikoa ya Mbeya na Tabora/Singida:** Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo – Chunya (Km. 72) umekamilika. Mkataba kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Chunya – Makongolosi (Km. 43) umesainiwa. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Makongolosi - Rungwa - Itigi – Mkiwa (sehemu ya Mkiwa - Itigi - Noranga Km. 57) zinaendelea.<br><br>(ix) **Mikoa ya Njombe na Mbeya:** Serikali imesaini mikataba na makandarasi wa ujenzi wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete Km. 107.4).<br><br>(x) **Mikoa ya Ruvuma na Morogoro:** Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (Km. 396) umekamilika. Aidha, mkataba na Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara (Km. 68) umesainiwa.<br><br>(xi) **Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Singida, Arusha na Manyara:** Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Matala – Oldean *Junction* (Km. 328). Aidha, upembuzi yakinifu unaendelea kwa barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom - Sibiti – Lalago-Maswa (km 389).<br><br>(xii) **Mikoa ya Dodoma na Manyara:** Sehemu ya Dodoma – Mayamaya (Km. 43.65) ujenzi umekamilika, sehemu ya Mayamaya - Mela (Km. 99.35) ujenzi umekamilika kwa asilimia 98 na sehemu ya Mela - Bonga (Km. 88.8) ujenzi umekamilika kwa asilimia 95. |
| **39(b)(iii)** | Kupunguza umaskini kwa kushirikisha kikamilifu vikundi vya wananchi katika kazi za matengenezo madogo madogo ya barabara kama vile kazi za | TANROADS imetenga fungu maalum kwa ajili ya kazi za matengenezo madogo zinazotekelezwa na wananchi na vikundi vya akinamama. |

| | | |
|---|---|---|
| | kufyeka nyasi, kuzibua mifereji na kufanya usafi wa barabara zinazopita katika maeneo yao. | |
| **39(b)(iv)** | Makandarasi wazalendo wanaoonesha nia ya kushiriki katika kazi kubwa za ujenzi wa barabara watapatiwa dhamana na Serikali ili kujenga uwezo na kuwapatia fursa za kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za sekta ya ujenzi. | Makandarasi Wazawa wanawezeshwa kupata dhamana ya mikopo kupitia Mfuko wa Kuwasaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund – CAF) unaosimamiwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB). Hadi Juni, 2017 Mfuko ulikuwa na mtaji wa Shilingi Bilioni 3.4 na wanachama 1,095. Katika mwaka 2016/17, dhamana zenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.8 zilitolewa kwa Makandarasi wanachama wa Mfuko huu. |
| **39(c)** | **Kukamilisha ukarabati wa barabara unaoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa. Kukamilisha ujenzi (km 2,439.35)** | |
| | (i) Sumbawanga – Matai – Kasanga (Km. 56 kati ya km 112) | Hatua ya utekelezaji ni asilimia 75, ambapo Km. 76 zimekamilika. |
| | (ii) Mziha – Turiani – Magole (Km. 75 kati ya Km. 84.6) | Ujenzi wa Km. 43 kati ya Km. 48.8 kutoka Magole hadi Turiani kwa kiwango cha lami umekamilika. |
| | (iii) Dumila – Kilosa (Km. 18 kati ya Km. 63) | Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Rudewa – Kilosa (Km. 18) uko katika hatua ya ununuzi. |
| | (iv) Dumila – Turiani - Handeni Km. 174) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Turiani – Mziha – Handeni, imekamilika. |
| | (v) Bariadi – Lamadi (Km. 13 kati ya km 71.8) | Ujenzi wa barabara ya Bariadi - Lamadi yenye urefu wa Km. 71.8 umekamilika. |
| | (vi) Mbeya – Chunya - Makongolosi (Km. 56 kati ya Km. 115) | Mbeya - Lwanjilo – Chunya (Km. 72) ujenzi imekamilika. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (Km. 43) umesainiwa. |
| | (vii) Bagamoyo – Makofia – Msata (Km. 7 kati ya Km. 64) | Ujenzi kwa kiwango cha lami (Km. 64) pamoja na daraja la Ruvu Chini umekamilika. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (viii) | Kisarawe – Mwaneromango (Km. 48 kati ya Km. 54) | Ujenzi wa kilometa 6.5 umekamilika. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga sehemu ya km 4 zinaendelea. |
| | (ix) | Kibosho Shine- Kwa Raphael- International School (Km. 24 kati ya Km. 43) | Ujenzi wa kilometa 17 kwa kiwango cha lami umekamilika. |
| | (x) | Kirua Nduoni – Mtoni (km 16 kati ya km 31.5) | Ujenzi umekamilika. |
| | (xi) | Nyamuswa – Bunda – Kisorya - Nansio (Km. 117 kati ya Km. 117.5) | Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 24. |
| | (xii) | Babati – Dodoma (Km. 195.15 kati ya Km. 251) | Ujenzi wa sehemu ya Dodoma - Mayamaya umekamilika na Mayamaya - Mela ujenzi umefikia asilimia 98 na sehemu ya Mela-Bonga asilimia 95. |
| | (xiii) | Sumbawanga – Kanyani – Nyakanazi (Km. 483.7 kati ya Km. 562) | (i) Ujenzi umekamilika kwa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (Km. 75); Kanazi – Kizi – Kibaoni (76.6:); na Sitalike - Mpanda (Km. 36.9).<br>(ii) Ujenzi unaendelea kwenye sehemu ya Mpanda - Usimbili: Ifukutwa - Vikonge (Km. 35) na kazi zimekamilika kwa asilimia 6.<br>(iii) Kidahwe - Kasulu (km 63): Ujenzi unaendelea na umekamilika kwa asilimia 37.50<br>(iv) Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (Km. 50): Ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea na umekamilika kwa asilimia 35.20. |

| | | |
|---|---|---|
| | (xiv) Nzega – Puge (Tabora) (Km. 20.5 kati ya Km. 116) | Kazi ya ujenzi wa mradi wote kilometa 116 imekamilika. |
| | (xv) Manyoni – Itigi – Tabora (Km. 113 kati ya Km. 264) | (i) Ujenzi wa barabara Manyoni – Itigi - Chaya (Km. 89.3) na Nyahua – Tabora (Km. 85) umekamilika.<br>(ii) Chaya – Nyahua (Km. 85.4): Mkataba wa ujenzi umesainiwa. |
| | (xvi) Mangaka – Mtambaswala (Km. 65) | Ujenzi umekamilika kwa asilimia 100 Agosti, 2016. |
| | (xvii) Makutano – Natta – Mugumu (Km. 125) | Kazi imekamilika kwa asilimia 45. |
| | (xviii) Kyaka – Bugene (Km. 59.16) | Mradi umekamilika kwa asilimia 100. |
| | (xix) Tunduru – Namtumbo (Km. 194) | Mradi umekamilika kwa asilimia 100. |
| | (xx) Tunduru – Mangaka (Km. 137) | Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zimekamilika asilimia 100. |
| | (xxi) Mwigumbi – Maswa – Bariadi (Km. 100) | Ujenzi wa kipande cha Mwigumbi - Maswa yenye urefu wa km 50.3 kazi za ujenzi zimefikia asilimia 76. Aidha, mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Maswa – Bariadi (Km. 49.7) umesainiwa. |
| | (xxii) Tabora – Urambo (Km. 8.8 kati ya km 90) | Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zimekamilika kwa asilimia 100. |
| | (xxiii) Uyovu – Bwanga - Biharamulo (Km. 112) | Ujenzi wa barabara ya Uyovu - Bwanga (Km. 45) umefikia asilimia 75 na wa barabara Bwanga - Biharamulo (Km. 67) umefikia asilimia 55. |
| | (xxiv) Kisesa – Usagara (Km. 17) | Ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 82. |
| | (xxv) Katumba – Mbambo – Tukuyu (Km. 80) | Ujenzi wa sehemu yenye urefu wa kilometa 10 unaendelea na umefikia asilimia 75. Usanifu wa sehemu ya kilometa 15 unaendelea. |
| | (xxvi) Kidahwe – Kasulu (Kanyani) (Km. 50) | Ujenzi wa barabara unaendelea na umefikia asilimia 37.50. |

| | | |
|---|---|---|
| | (xxvii) Katumba – Mbambo – Tukuyu (Km. 80) | Ujenzi wa sehemu yenye urefu wa kilometa 10 unaendelea na umefikia asilimia 75. Usanifu wa sehemu ya kilometa 15 unaendelea. |
| | (xxviii) Kidahwe – Kasulu (Kanyani) (Km. 50) | Ujenzi wa barabara unaendelea na umefikia asilimia 37.50. |
| | (xxix) Kikusya - Ipinda – Matema Beach (Km. 39.5) | Ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 32. |
| | (xxx) KIA-Mererani (Km. 26) | Mradi umekamilika. |
| | (xxxi) Mwanga - Kikweni – Lomwe | Hatua za ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa km 9.6 kwa kiwango cha lami zipo katika hatua za mwisho. |
| | (xxxii) Kaliua – Kazilambwa (Km. 42 kati ya Km. 56) | Mradi umekamilika. |
| | (xxxiii) Dodoma University Road (Km. 12) | Utekelezaji wa mradi huu unaendelea na umefikia asilimia 77. |
| 39 (c) (ii) | **Kukamilisha ukarabati (Km. 517.2)** | |
| | (i) Ushirombo – Lusahunga (Km. 67 kati ya 110) | Kazi za ukarabati wa kilometa 56 zimekamilika kwa kiwango cha lami. |
| | (ii) Morocco – Mwenge (Km. 4.3) | Mradi umekamilika. |
| | (iii) Segera – Same – Himo (Km. 131 kati ya Km. 285) | Ukarabati umekamilika. |
| | (iv) Nyagunge – Musoma – Sirari (km 177 kati ya Km. 262) | Ukarabati wa eneo la Simiyu/Mara Border- Musoma (Km. 85.5) umekamilika. |
| | (v) Mafinga – Igawa (Km. 137.9) | Kazi za ukarabati kipande cha **Mafinga – Nyigo Section (Km. 74.1)** imefikia asilimia 73 na **Nyigo – Igawa Section (Km. 63.8)** imefikia asilimia 52. |

| | | |
|---|---|---|
| 39 (d) | **Kuanza Ujenzi mpya na ukarabati kwa Kiwango cha Lami Barabara Zifuatazo:** | |
| | **Kuanza ujenzi (Km. 5,427.0)** | |
| | (i) Njombe – Ndulamo - Makete (Km. 109) | Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami umesainisa Juni, 2017 kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha Njombe - Moronga (Km. 53.9) na Moronga - Makete (Km. 53.5). |
| | (ii) Nata – Fort Ikoma (Km. 30) | Mradi upo katika hatua za ununuzi. |
| | (iii) Mto wa Mbu – Loliondo (Km. 213) | Ujenzi wa sehemu ya Wasso (Loliondo) – Sale Junction (Km. 49) umeanza. |
| | (iv) Sanya Juu – Boman'gombe (Km. 25) | Ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Alerai (Km. 32.2) umefikia asilimia 24 |
| | (v) Tabora – Ipole - Koga – Mpanda (Km. 359) | Makandarasi kwa ujenzi wa vipande vya Uselula – Komanga (108 Km.) pamoja na sehemu ya barabara ya Sikonge (Sikonge Spur Road - 7.5 Km.); Komanga - Kasinde (Km. 108) barabara ya Inyonga (Inyonga Spur Road – Km. 4.8) wamealikwa.<br>Kwa barabara ya Kasinde - Mpanda Section (Km. 108) pamoja na sehemu ya barabara ya Urwira (Urwira Spur Road – Km. 3.7), AfDB taratibu za kualika Makandarasi zinaendelea. |
| **39 (d)** | **Kuanza Ujenzi mpya na ukarabati kwa Kiwango cha Lami Barabara Zifuatazo:** | |
| | (i) Matai - Kasesya (Km. 50) | Taratibu za kusaini Mkataba ziko katika hatua za mwisho. |
| | (ii) Sanya Juu – Kamwanga (Km. 75) | Ujenzi wa kipande cha Sanya Juu – Alerai (Km. 32.2) umekamilika kwa asilimia 24. |
| | (iii) Rujewa - Madibira – Mafinga (Km. 151) | Ipo katika hatua ya ununuzi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (iv) | Makurunge – Saadan – Pangani - Tanga (Km. 178) | Usanifu wa kina umekamilika. |
| | (v) | Mbinga – Mbamba bay (Km. 66) | Taratibu za kualika Makandarasi zinaendelea. |
| | | | |
| **39 (d)** | | **Kuanza Ujenzi mpya na ukarabati kwa Kiwango cha Lami Barabara Zifuatazo:** | |
| | (vi) | Matai - Kasesya (Km. 50) | Taratibu za kusaini Mkataba ziko katika hatua za mwisho. |
| | (vii) | Sanya Juu – Kamwanga (Km. 75) | Ujenzi wa kipande cha Sanya Juu – Alerai (Km. 32.2) umekamilika kwa asilimia 24. |
| | (viii) | Rujewa - Madibira – Mafinga (Km. 151) | Ipo katika hatua ya ununuzi. |
| | (ix) | Makurunge – Saadan – Pangani - Tanga (Km. 178) | Usanifu wa kina umekamilika. |
| | (x) | Mbinga – Mbamba bay (Km. 66) | Taratibu za kualika Makandarasi zinaendelea. |
| | (xi) | Mtwara – Mingoyo - Masasi (Km. 200) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (xii) | Mpemba – Isongole (Tanzania/Malawi) (Km. 49) | Mkandarasi yuko katika hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi (mobilization). |
| | (xiii) | Makongolosi – Rungwa - Mkiwa (Km. 412) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. |
| | (xiv) | Mtwara – Newala – Masasi (Km. 209) | Mkandarasi wa sehemu ya Mtwara – Mnivata (Km. 50) yuko katika maandalizi ya kuanza ujenzi (mobilization). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (xv) | Kibaha – Mapinga (Km. 23) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika na ujenzi unaendelea ambapo kilomita moja imekamilika hadi sasa. |
| | (xvi) | Geita - Bukoli – Kahama (Km.107) | Upembuzi na usanifu wa kina umekamilika. Kazi ya kuandaa nyaraka za zabuni zinaendelea. |
| | (xvii) | Mbande – Kongwa Jct – Mpwapwa (Km. 50) | Kilometa 8 kwa kiwango cha lami zimejengwa, kilometa 6 zimejengwa Kongwa na kilometa 2 Mpwapwa. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 5 anaendelea na kazi. |
| | (xviii) | Ipole – Rungwa (Km. 172) | Mradi unahusisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea. |
| | (xix) | Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeka (Mfuji) – Morogoro/Njombe Boarder (km 125) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. |
| | (xx) | Itoni – Ludewa – Manda (Km. 211) | Ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda Road (Km. 211) kwa kiwango cha zege (Cement Concrete) sehemu ya Lusitu – Mawengi (Km. 50) unaendelea na umefikia asilimia 1.8. |
| | (xxi) | Dar es salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (Km.190) | Mtaalam Mwelekezi (Transaction Adviser) amekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na hatua za kumpata Mwekezaji/Mbia zinaendelea. |
| | (xxii) | Musoma – Makojo - Busekela (Km. 92) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (xxiii) | Tabora – Mambali – Bukene – Itobo – Kahama (Km. 149) | Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami. |
| | (xxiv) | Lupilo – Malinyi - Kilosa kwa Mpepo – Londo – Kitanda (Km. 396) | Kazi za upembuzi yakinifu zinaendelea na Mhandisi Mshauri amewasilisha ripoti ya mwisho ya upembuzi yakinifu. |

| | | |
|---|---|---|
| | (xxv) Itoni – Ludewa – Manda (Km. 211) | Ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi (Km. 50) unaendelea na umefikia asilimia 1.8. |
| | (xxvi) Ifakara – Mahenge (Km. 67) | Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. |
| | (xxvii) Kibondo – Mabamba (Km. 35) | Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. |
| | (xxviii) Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldeani Jct (Km. 328) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (xxix) Omugakorongo – Kigarama –Murongo (Km. 111) | Kazi za upembuzi yakinifu zinaendelea. |
| | (xxx) Soni – Bumbuli – Dindira- Korogwe (Km. 74) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira (Km. 74) inaendelea. |
| | (xxxi) Makofia – Mlandizi - Vikumburu (Km 148) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kipande cha barabara cha Makofia – Mlandizi -Maneromango (Km.100.35) umekamilika. Na zoezi la utathimini wa fidia kwa wananchi linaendelea. |
| | (xxxii) Handeni – Kiberashi – Kondoa – Singida (Km. 433) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (xxxiii) Pugu – Kifuru - Mbezi Mwisho - Mpiji Magoe - Bunju (Km. 34) | Kipande cha kilomita 12 kimeshajengwa. |
| | (xxxiv) Kisarawe – Mlandizi (Km. 52) | Kilometa 6.5 za sehemu ya Kisarawe – Maneromango, zimejengwa kwa kiwango cha lami. |
| | (xxxv) Kiboroloni – Tsuduni – Kidia (Km. 10.8) | Usanifu wa kina umekamilika. Zabuni za kumpata Mkandarasi zimetangazwa. |
| | (xxxvi) Nyamirembe Port – Katoke (Km. 50) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea. |
| | (xxxvii) Handeni – Kiberashi – Kondoa – Singida (Km. 460) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (xxxviii) Iringa – Ruaha National Park (Km. 104) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. Mradi umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2017/18. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (xxxix) | Njombe (Ramadhani) – Iyayi (Km. 74). | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. |
| | | | |
| 39 (d)(ii) | **Kuanza ukarabati (Km. 1,055.12)** | | |
| | (xl) | Arusha – Moshi – Himo – Holili (Km. 140). | Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Tengeru – Sakina (Km. 14.1) imekamilika. Kwa sehemu ya njia ya Mchepuo (Km. 42.4) kazi zimekamilika kwa asilimia 55.65. |
| | (xli) | Makambako – Songea (Km. 295) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikamilika Agosti. |
| | (xlii) | Mtwara – Mingoyo – Masasi (Km. 200) | Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. |
| | (xliii) | Lusahunga – Rusumo (Km. 92) | Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. |
| | (xliv) | Nyakasanza – Kobero (Km. 60) | Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. |
| 39 (e) | **Kuzifanyia Upembuzi na Usanifu wa kina km 6,530.7 Barabara Zifuatazo:-** | | |
| | (i) | Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (Km. 428) | Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu zinaendelea. |
| | (ii) | Arusha - Kibaya – Kongwa (Km. 430) | Mkataba wa Mhandisi Mshauri kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa. |
| | (iii) | Bugene – Kasulo /BENACO)(Km. 124) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (iv) | Mbeya – Tunduma (Km. 104) | Kazi za upembuzi yakinifu zimekamilika na usanifu wa kina unaendelea. |
| | (v) | Morogoro – Dodoma (Km. 263) | Utekelezaji wa mradi huu haujaanza. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (vi) | Mwanza – Mwanza/Shinyanga (Km. 102) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea. |
| | (vii) | Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (Km. 149) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi huu umekamilika. |
| | (viii) | Magu – Bukwimba - Ngudu – Jojiro (Km. 64) | Mradi upo katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. |
| | (ix) | Tarime – Mugumu ( Km. 87) | Kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea. |
| | (x) | Amani – Muheza (Km. 34) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. |
| | (xi) | Nyehunge – Sengerema (Km. 68) | Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. |
| | (xii) | Mugakorongo – Rwambaizi – Murongo (Km. 125) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ipo katika hatua za mwisho. |
| | (xiii) | Morogoro (Bigwa) – Mvuha (Km. 78) | Usanifu wa kina unaendelea na upo katika hatua za mwisho. |
| | (xiv) | Morogoro Border – Kibena – Lupembe – Mfuji (Morogoro/Njombe Boarder) (Km.125) | Usanifu wa kina umekamilika. |
| | (xv) | Kamanga – Katunguru - Sengerema (Km. 35) | Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu zinaendelea. |
| | (xvi) | Geita – Nzera – Nkome (Km. 54)(Geita) | Ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza fedha zikipatikana |
| | (xvii) | Upanuzi wa Tegeta – Bagamoyo (Km. 57) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. |
| | (xviii) | Kibada – Kimbiji (Km. 29.2) | Mradi upo kwenye hatua ya ununuzi. |
| | (xix) | Murugarama – Rulenge – Nyakahura (Km. 85) | Mradi upo kwenye hatua ya ununuzi. |
| | (xx) | Karatu – Mbulu –Haydom – Singida (Km. 190) | Upembuzi yakinifu unaendelea. |
| | (xxi) | Bariadi – Kisesa –Mwandoya – Ngoboko –Mwanhuzi – Sibiti – Mkalama – Iguguno (Km. 289) | Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami |
| | (xxii) | Mika – Utegi – Shirati (Km. 44) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea. |

| | | |
|---|---|---|
| | (xxiii) Chimala – Matamba – Kitulo (Km. 51) | Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami |
| | (xxiv) Upanuzi wa Kitonga Escarpment (Km. 10) | Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. |
| | (xxv) Babati – Orkesmet – Kibaya (Km. 225) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea. |
| | (xxvi) Kongwa – Mbuyuni NARCO JCT – Kibaya – Orkesmet (Km. 340) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeanza. |
| | (xxvii) Madaba – Mundindi (Liganga) – Mkiu (Km. 46) Ruvuma. | Mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa tarehe 14/7/2017 na kazi inaendelea. |
| | (xxviii) Muhutwe – Kamachumu – Muleba (Km. 53) | Ujenzi wa Km. 8.7 kwa kiwango cha lami umekamilika. |
| | (xxix) Mto wa Mbu – Loliondo – Karatu – Ngorongoro (Km. 300) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. Mkandarasi wa sehemu ya Wasso (Loliondo) – Sale Junction (Km. 49) anaendelea na kazi ya ujenzi. |
| | (xxx) Likuyufusi – Mkenda (Km. 124) | Upembuzi yakinifu na usanifu umekamilika |

### 2.7.2 Madaraja



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, na Rais wa Benki ya Dunia, Dkt. Jim Yong Kim, wakikata utepe kuashiria ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya Barabara za Morogoro na Sam Nujoma (Ubungo Interchange) katika eneo la Ubungo Jijini Dar es Salaam.*



*Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja. Pichani ni daraja la waenda kwa miguu katika eneo la Furahisha, mkoani Mwanza, lililojengwa kwa mapato ya ndani ya Serikali.*




*Daraja la juu (flyover) inayoendelea kujengwa na Serikali ili kupunguza msongamano wa magari katika makutano ya barabara ya Nyerere na Nelson Mandela, eneo la TAZARA, jijini Dar es Salaam.*

| | | | |
|---|---|---|---|
| **39(f)(i)** | **Kukamilisha ujenzi wa madaraja sita (6) yafuatayo:-** | | |
| | (xxxi) | Kilombero na barabara za maingilio Km. 9 | Ujenzi wa Daraja na barabara za maingilio umekamilika |
| | (xxxii) | Kigamboni na barabara za maingiliano Km. 10 | Ujenzi wa daraja umekamilika na kuanza kutumika Mei 2016. |
| | (xxxiii) | Kavuu (Katavi) | Ujenzi wa daraja umekamilika. |
| | (xxxiv) | Sibiti (Singida) | Ujenzi wa daraja hili umefikia asilimia 55. |
| | (xxxv) | Lukuledi II (Lindi) | Ujenzi wa daraja umekamilika asilimia 100. |
| | (xxxvi) | Ruvu Chini (Pwani) | Ujenzi wa daraja hili umekamilika asilimia 100. |
| 39(f)(ii) | **Kuanza ujenzi/ukarabati wa Madaraja saba (7) yafuatayo:-** | | |
| | (xxxvii) | Ruhuhu (Ruvuma) | Ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 35. |
| | (xxxviii) | Momba (Rukwa) | Mkandarasi amepatikana na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea |
| | (xxxix) | Kirumi (Mara) | Taratibu za awali zimekamilika. |
| | (xl) | Selander (Daraja jipya) (DSM) | Zabuni za kumpata Mkandarasi imetangazwa Oktoba, 2017. |
| | (xli) | Magara (Manyara) | Mradi uko kwenye hatua ya ununuzi. |
| | (xlii) | Wami Chini (daraja jipya) (Pwani) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. |
| | | Pangani (Tanga) | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja hili umekamilika. |

| | | |
|---|---|---|
| | (xliii) Lukuledi II (Lindi) | Ujenzi wa daraja umekamilika asilimia 100. |
| | (xliv) Ruvu Chini (Pwani) | Ujenzi wa daraja hili umekamilika asilimia 100. |
| 39(f)(iii) | **Kuanza usanifu wa madaraja matatu (3) yafuatayo:-** | |
| | (xlv) Daraja la Simiyu (Mwanza) | Mkandarasi amepatikana na yuko kwenye maandalizi ya kuanza kazi ya ujenzi |
| | (xlvi) Mzinga (DSM) | Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni zinaendelea. |
| | (xlvii) Mlalakuwa (DSM) | Ujenzi wa daraja hili unaendelea na umefikia asilimia 10. |
| **39(g)** | **Kuanza ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) kwenye makutano ya barabara maeneo yafuatayo :-** | |
| | TAZARA | Hatua ya utekelezaji kwa mradi wa TAZARA *flyover* imefikia asilimia 50. |
| | Ubungo | Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Ubungo *flyover* ulisainiwa Februari 2017. |
| | Chang'ombe | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwezi Juni 2017. |
| | Uhasibu | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwezi Juni 2017. |
| | KAMATA | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwezi Juni 2017. |
| | Morocco | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwezi Juni 2017. |
| | Mwenge | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwezi Juni 2017. |
| | Magomeni | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu |

| | | |
|---|---|---|
| | | wa kina mwezi Juni 2017. |
| | Tabata | Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwezi Juni 2017. |
| **39(g)** | **Kuanza na kukamilisha ujenzi wa barabara na reli ili kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam:-** | |
| **39(g)(i)** | **Kukamilisha ujenzi (Km. 80.1)** | |
| | (i) Mbezi – Marambamawili – Kinyerezi - Banana (Km. 14.0) | Ujenzi wa kipande cha barabara kuanzia Kifuru hadi Kinyerezi, chenye urefu wa Km. 4 ambayo ilikamilika Agosti, 2016 na ujenzi wa Km. 4 kati ya Km. 6.1 kutoka Mbezi Mwisho hadi Kifuru unaendelea na umefikia asilimia 50. |
| | (ii) Tangi Bovu - Goba (Km. 5.2 kati ya Km. 9.0); | Barabara ilikamilika Agosti, 2016. |
| | (iii) Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (Km. 2 kati ya Km. 2.6) | Ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 43. |
| | (iv) Kimara Kilungule - External Mandela road (Km. 8.8 kati ya Km. 9.0); | Ujenzi umekamilika kwa Km. 3. |
| | (v) Kigogo Round About – Bonde la Msimbazi - Twiga/Msimbazi Jct ( Km. 0.5 kati ya Km. 2.7) | Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekamilika. |
| | (vi) Tabata Dampo – Kigogo (Km. 1.6 kati ya Km. 2.25) | Barabara hii imekamilika. |

| | | |
|---|---|---|
| | (vii) Kibamba – Mlonganzila (Km. 8 kati ya Km. 12.0) | Ujenzi wa Km. 4 za lami umekamilika. Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa Km. 8 zilizobaki kulingana na upatikanaji wa fedha |
| 39(g)(ii) | **Kuanza ujenzi (km 58.8)** | |
| | (i) Upanuzi wa Barabara ya Mwai Kibaki (Morocco – Kawe Round. about) na Garden Road (Km. 9.1). | Ujenzi wa daraja la Mlalakuwa unaendelea. Upanuzi wa barabara uko katika hatua ya kumpata Mkandarasi |
| | (ii) Banana - Kitunda - Kivule | Kazi za ujenzi zinaendelea kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | – Msongola (Km. 14.7). | sehemu yenye urefu wa Km. 3.2. |
| | (iii) Ardhi - Makongo – Goba (Km. 9). | Ujenzi wa barabara hii (sehemu ya Goba – Makongo Km. 4) umefikia asilimia 20. |
| | (iv) Upanuzi wa barabara ya Uwanja wa Ndege (JNIA) – Pugu (Km. 8). | Mradi utatekelezwa chini ya BRT II. |
| | (v) Upanuzi wa barabara ya Mbagala – Kongowe – Mwandege (Km. 4). | Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zimeanza. |
| | (vi) Banana - Kitunda - Kivule – Msongola (Km. 14.7). | Kazi za ujenzi zinaendelea kwa sehemu yenye urefu wa Km. 3.2. |
| | (vii) Ardhi - Makongo – Goba (Km. 9). | Ujenzi wa barabara hii (sehemu ya Goba – Makongo Km. 4) umefikia asilimia 20. |
| | (viii) Upanuzi wa barabara ya Mbagala – Kongowe – Mwandege (Km. 4). | Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zimeanza. |
| | (ix) Upanuzi wa barabara ya DSM Port – TAZARA – Uwanja wa Ndege (JNIA) – Pugu (Km. 14). | Mradi utatekelezwa chini ya BRT II. |
| | **Kuanza ujenzi wa miundombinu ya mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT) Awamu ya Pili (II) na Tatu (III) :-** | |
| | (x) Awamu ya II: Barabara ya Kilwa na Kawawa (19.3) | Mradi huu uko katika hatua ya ununuzi. |
| | (xi) Awamu ya III: Barabara za Nyerere, Uhuru, Bibi Titi Mohamedi na Azikiwe (23.6) | Mradi huu uko katika hatua ya ununuzi. |
| 39 (h) | **Miradi ya Kupunguza Msongamano katika Majiji na miji mingine yenye jumla ya km 102 kama ifuatavyo:-** | |
| | (xii) Usagara – Kisesa (Km. 17), Mwanza | Utekelezaji wa barabara hii ni asilimia 82. |
| | (xiii) Shabiby Arusha road Round about (Km.1.6) (Dodoma) | Mradi uko katika hatua ya ununuzi. |

| | | |
|---|---|---|
| | (xiv) Uyole – Songwe (Km. 40)(Mbeya) | Usanifu wa kina umekamilika. |
| | **2.7.2 Vivuko** | |
| | (xv) Kuanza ujenzi wa kivuko kipya cha Rugezi – Kisorya Mkoani Mwanza | Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi wa kivuko kipya cha Rugenzi – Kisorya. |
| | (xvi) Kuanza ujenzi wa kivuko kipya cha Pangani – Bweni Mkoani Tanga | Serikali imekamilisha ujenzi wa kivuko kipya cha Pangani (MV Tanga) chenye uwezo wa kubeba Tani 50, magari madogo 6 na abiria 100 mwezi Septemba, 2016. |
| | (xvii) Upanuzi wa Jengo la abiri wa kivuko cha Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni; | Mkandarasi kwa kazi ya upanuzi wa jengo la abiria upande wa Kigamboni ameshapatikana na mkataba umesainiwa. |
| | (xviii) Kuanza ujenzi wa kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni | Ujenzi wa kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni (MV Kazi) chenye uwezo wa kubeba Tani 170 sawa na magari 22 na abiria 800 umekamilika mwezi Juni, 2017 na kimeanza kufanya kazi. |

## 2.7.3 Usafiri wa Anga




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akizindua ndege mpya aina ya Bombadier Q400 katika uwanja wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere, Jijini Dar es Salaam*

| | | |
|---|---|---|
| 41(a) | Kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Jengo la Tatu Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na kuanza ujenzi wa awamu ya Pili ya Jengo la Tatu Abiria la JNIA | Ujenzi wa jengo umekamilika kwa asilimia 66. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa jengo (Superstructure) na ujenzi wa kuta za ndani (Partition walls) pamoja na ujenzi wa paa awamu ya kwanza. Kazi zinazoendelea nyingine zinaendelea |
| 41(c) | Kuanza na kukamilisha ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Shinyanga na Sumbawanga kwa kukarabati barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha lami. | Mikataba ya Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na mkataba wa Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi wa viwanja hivi imekwishasainiwa. |
| 41(d) | Kujenga na kukamilisha awamu ya pili ya Viwanja vya Ndege vya Tabora na Kigoma | Ujenzi wa barabara ya pili ya kurukia na kutua ndege (runway), barabara ya maungio (taxiway) na maegesho (apron) ya ndege, ujenzi wa mifumo wa taa za kuongozea ndege (AGL) pamoja na mifumo ya mawasiliano ya kuongozea ndege (NavAids) vimekamilika kwa uwanja wa Tabora. Kwa uwanja wa ndege wa Kigoma, ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | kumpata mkandarasi kutokana na kurudiwa kwa mchakato wa ununuzi inaendelea. |
| 41(e) | Kuanza ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Msalato kwa kiwango cha Kimataifa | Mkataba wa Mradi kwa ajili ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Kiwanja Cha Ndege cha Msalato umesainiwa tarehe 29 Juni, 2017. Aidha, katika mwaka 2017/2018, Shilingi bilioni 3.5 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia. |
| | Kukamilisha upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Mwanza hususan Jengo la abiria na kufikia kiwango cha kimataifa. | Kazi zilizofanyika ni kurefusha njia ya kurukia ndege kwa asilimia 95; ujenzi wa jengo la waongoza ndege kwa asilimia 70; ujenzi wa jengo la kituo cha umeme kwa asilimia 80; ujenzi wa jengo la kupokea na kuhifadhi mizigo kwa asilimia 55; ujenzi wa eneo la maegesho ya ndege za mizigo pamoja na kiunganishi kwa asilimia 75; na umaliziaji wa uwekaji wa matabaka ya lami kwenye maegesho ya ndege za abiria umekamilika kwa asilimia 99. |
| 41(g) | Kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa kuanza awamu ya pili ya mradi wa ujenzi, ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege kumi na moja (11) vya mikoa vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina vya Lindi, Kilwa Masoko, Songea, Singida, Lake Manyara, Tanga, Iringa, Njombe, Simiyu, Musoma na Moshi. | Katika mwaka 2017/18, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza kazi za ukarabati na upanuzi katika viwanja vya ndege vya Iringa (bilioni 3.76), Musoma (bilioni 3.85) na Songea (bilioni 3.66). Vilevile, Shilingi bilioni 2 zimetengwa kwa ajili ya kazi za maandalizi ya viwanja vinane vilivyobaki. |
| 41(h) | Kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa kuhamasisha uwekezaji wa | Katika mwaka 2016/17, Serikali iliingia mkataba wa ununuzi wa ndege mpya 6 ambapo ndege mbili (2) aina ya *Bombardier Dash 8 Q 400* ziliwasili |

| | | |
|---|---|---|
| | Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) ili kuimarisha huduma za Shirika la Ndege la Taifa. | nchini Septemba, 2016 na zinaendelea kutoa huduma. Ndege 1 aina ya *Bombardier Dash 8 Q 400* imekamilika na itawasili nchini wakati wowote. Ndege mbili (2) aina ya C -*series* na *Boeing 787-8 Dreamliner* 1 zitakuwa zimeingia zote nchini ifikapo Juni, 2018. |

| 2.7.4 Huduma za Hali ya Hewa | | |
|---|---|---|
| 41(a) | Huduma za Hali ya Hewa kuendelea kuboreshwa kwa kuanza ujenzi wa kituo kikuu cha utabiri wa hali ya hewa nchini. | Kazi ya usanifu wa awali ilikamilika Mei, 2017. Ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mjini Dodoma. |
| 41(b) | Huduma za Hali ya Hewa kuendelea kuboreshwa kwa kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa nchini ili kufikia kiwango cha kimataifa kwa kununua rada za hali ya hewa zisizopungua tano. | Katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga Shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya ununuzi wa Rada ya Hali ya Hewa na vifaa mbalimbali vya hali ya hewa. |

## 2.7.5 Miundombinu ya Huduma za Reli




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akipita katika mfano wa reli ya Standard Gauge inayojengwa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.*



*Mafundi wa Kampuni ya Yapi Merkezi inayojenga Reli ya Kisasa (Standard Gauge), wakiendelea na kazi ya kujaza zege kwenye moja ya kalvati katika eneo la Kisarawe mkoani Pwani.*

| | | |
|---|---|---|
| 39(g) (iv) | Kuanza ujenzi wa reli ya usafirishaji wa abiria katika Jiji la Dar es Salaam. | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia mpya za reli kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na |

| | | |
|---|---|---|
| | | Bunju/Kerege ilianza Machi, 2015 na inatarajiwa kukamilika Julai, 2018. |
| 41(a)(i) | Kwa kushirikiana na Sekta Binafisi kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa kiwango cha *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam – Tabora – Kigoma/Mwanza. | Ujenzi wa kipande cha Km. 300 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro utakaogharimu **Shilingi trilioni 2.74** umeanza na Mkataba wa kuanza ujenzi wa kipande cha Km. 412 kutoka Morogoro hadi Dodoma (Makutopora) wenye thamani ya **Shilingi trilioni 4.328** umesainiwa. |
| 41(a)(ii) | Kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa *standard gauge* kutoka Uvinza – Msongati (Burundi) na Isaka – Kigali (Rwanda). | Kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza – Musongati imekamilika. Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi zinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kugharamia mradi huo. |
| 41(a)(iii) | Kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa *standard gauge* kutoka Mtwara – Songea – Mbamba Bay na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga. | Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea –Amerlia Bay (Manda) na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga (Km. 1,000) kwa *Standard Gauge* ilikamilika Juni, 2016. |
| 41 (a)(iv) | Kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa *Standard Gauge* kutoka Tanga – Arusha – Musoma | Kazi ya usanifu wa kina wa njia ya Reli ya Tanga – Arusha imekamilika Mei, 2015 na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Arusha hadi Musoma (Km. 600) na matawi ya Engaruka (Km. 53), Minjingu (Km. 35) na tawi kuelekea Dutwa (Km. 2.8) pamoja na reli ya Tabora – Mwanza (Km. 120) unaendelea. |
| 41(a)(v) | Kwa kushirikiana na sekta binafisi kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa *Standard Gauge* kutoka Kaliua – Mpanda – Karema. | Kazi za Usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Mpanda – Karema (Km.150) na Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Kaliua – Mpanda zinatarajiwa kukamilika Juni, 2018. |

### 2.7.6 Usafiri wa Majini



*Meli mpya iliyonunuliwa na Serikali ili iwahudumie wananchi katika Ziwa Nyasa*



*Serikali iliahidi kuboresha huduma za usafiri wa majini. Wananchi wakiingia ndani ya kivuko cha MV Mafanikio mkoani Mtwara.*

| | | |
|---|---|---|
| 41(b) | Kushirikiana na Sekta Binafsi, kuendelea kuboresha huduma za uchukuzi katika Bandari za mwambao kwa kukamilisha uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 ili kuimarisha utoaji wa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam. | Kazi ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na uongezaji wa kina katika gati Na. 1 hadi 7, ujenzi wa gati jipya la kushushia magari eneo la Gerezani *Creek*, kupanua na kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli inaendelea. Mkataba wa ujenzi wa mradi ulisainiwa Juni, 2017 na Jiwe la Msingi la Upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam ambao utagharimu **Shilingi bilioni 926.2** liliwekwa Julai 2017 |
| 41(d) | Kushirikiana na Sekta Binafsi, kuendelea kuboresha huduma za uchukuzi katika bandari za mwambao kwa kuanza ujenzi wa bandari mpya za Bagamoyo na Mwambani Tanga. | Serikali imepokea mapendekezo ya Kampuni ya *China Merchants Port Limited (CMPort)* ikishirikiana na *State General Reserve Fund* (Oman) kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Hatua itakayofuata ni makubaliano kati ya Serikali na wawekezaji hao kuhusu utafutaji wa fedha za ujenzi wa bandari na miundombinu wezeshi. Aidha, taratibu |

| | | |
|---|---|---|
| | | za kutafuta mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa Bandari ya Tanga ambao utagharimu Shilingi bilioni 16 unaendelea. |
| 41(e) | Kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea kuboresha huduma za uchukuzi katika bandari za mwambao kwa kuanza na kukamilisha ujenzi wa magati manne ya ziada katika Bandari ya Mtwara. | Mkataba wa ujenzi wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 350 kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko ulisainiwa tarehe 4 Machi, 2017. Mkandarasi alikabidhiwa rasmi mradi tarehe 26 Mei 2017 na ujenzi unatarajiwa kukamilika Februari, 2019. Upanuzi huo utagharimu **Shilingi bilioni 130.** |
| 41(f) | Kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea kuboresha huduma za uchukuzi katika bandari za mwambao kwa kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Nyamisati ili kuboresha usafirishaji wa kwenda na kutoka Mafia. | Upembuzi yakinifu wa mradi huu umekamilika. Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Bandari hii unatarajiwa kusainiwa Novemba 2017. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika Juni, 2019. |
| 41(g) | Kushirikiana na Sekta Binafsi, kuendelea kuboresha huduma za uchukuzi katika bandari za mwambao kwa kuendelea kuboresha Bandari ya Mwanza, upanuzi wa Bandari ya Musoma na ujenzi wa magati ya Ntama, Lushamba na Kyamkwikwi. | (i) Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa uboreshaji wa miundombinu ya bandari iliyopo Ziwa Victoria ulikamilika Aprili 2017 na hatua za kuwatafuta wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa bandari hizo unaendelea.<br>(ii) Ujenzi wa gati la Ntama katika Ziwa Victoria ulikamilika Agosti, 2016.<br>(iii) Ujenzi wa gati la Lushamba ulikamilika Julai 2016.<br>(iv) Kazi ya kukarabati gati la Kyamkwikwi ilikamilika Agosti, 2016. |

| | | |
|---|---|---|
| 41(h) | Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya bandari za Ziwa Nyasa na Tanganyika ili kuimarisha huduma zitolewazo kwa kujenga magati ya Kagunga, Kasanga, Kibirizi, Itungi na Kiwira. | (i) Kazi ya ujenzi wa gati la Sibwesa katika Ziwa Tanganyika ilianza Desemba, 2015 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2017.<br>(ii) Ujenzi wa gati la Kibirizi katika ziwa Tanganyika umeanza Juni, 2017 na unatarajiwa kukamilika Julai, 2018.<br>(iii) Ujenzi wa gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika ulikamilika Januari, 2017 |
| 41(I) | Kuboresha Mfumo wa Uondoshaji Mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza kiwango cha utendaji kwa kuweka Mfumo wa "Electronic Single Window System" na kufunga mita za kupima mafuta. | Mshauri Mwelekezi wa kuwezesha Mfumo wa TANCIS kutoa huduma za *Electronic Single Window* anaendelea na kazi chini ya usimamizi wa TRA. Kazi hii ilianza kutekelezwa Agosti, 2016 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2017 na zabuni za ununuzi wa Mita ya kupima mafuta zimefunguliwa Septemba, 2017. |
| 41(j) | Kujenga na kukamilisha meli mbili (2) za abiria na mizigo. Meli moja ya abiria na mizigo katika Ziwa Victoria na meli nyingine ya abiria na mizigo katika Ziwa Nyasa. | Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) inatarajia kuingia mkataba na mkandarasi aliyeshinda zabuni ya ujenzi wa meli katika Ziwa Victoria (Kampuni ya M/S STX Engine Co. LTD kwa ubia na STX Offshore & Shipbuilding Co. Ltd) baada ya kukamilisha majadiliano. Mkataba huo unatarajiwa kusainiwa Oktoba, 2017 |
| | | Ujenzi wa matishari mawili (2) (Self Propelled Barges) yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja katika Ziwa Nyasa ulikamilika Februari, 2017. Aidha, ujenzi wa Meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa ulianza Juni, 2016 na unatarajiwa kukamilika Oktoba 2017. |

## 2.8 Nishati




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akikagua ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi, Kinyerezi Jijini Dar es Salaam




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi mkubwa wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga Tanzania.



Serikali imeendelea na kazi ya kusambaza umeme vijijini. Mafundi umeme wakisimika nguzo za umeme katika wilaya ya Itilima, mkoani Simiyu chini ya mradi unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akioneshwa moja ya mifuniko ya transfoma za umeme na Meneja Mkuu wa kampuni ya kutengeneza transfoma za umeme ya TANELEC, Bw. Zahir Saleh (kulia).

Serikali inaimarisha na kuboresha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini na vijijini kwa kuzingatia Sera ya Nishati ya Taifa na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme wa mwaka 2009 – 2033. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na 9.

Bangokitita 9: Mafanikio Katika Sekta ya Nishati

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 43(a) | Kuongeza uzalishaji wa Umeme ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma hii, kulingana na Sera ya Nishati ya Taifa, kwa kutekeleza miradi iliyoainishwa kwenye Mpango Kabambe wa kuendeleza sekta ya Umeme *(Power System Master Plan 2009 – 2033)* ili kukidhi mahitaji ya umeme nchini; kipaumbele kitatolewa katika rasilimali za makaa ya mawe, maji *(hydro),* gesi asilia na Nishati jadidifu *(renewable energy)* ambapo lengo ni kufikia MW. 4,915 mwaka 2020 kutoka MW.1,308 mwaka 2015 | Serikali inatekeleza Miradi mikubwa ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I na II ambayo kwa pamoja inatarajiwa kuzalisha Megawati 565 kwa kutumia gesi asilia kwa gharama ya **Shilingi trilioni 1.2** na maandalizi kwa ajili ya miradi ya Kinyerezi III na IV ambayo itazalisha takribani Megawati 600 inaendelea. Vilevile, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa maji wa Staglier's Gorge ambao utazalisha Megawati 2,100. |
| 43(b)(i) | Kukamilisha Mradi wa Backbone wa kV 400 unaounganisha mikoa ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga wenye urefu wa Km.670 | Mradi huo Umekamilika tarehe 28 Desemba 2016 kwa asilimia 100. |
| 43(b)(ii) | Mradi wa Makambako – Songea wa kV 220, ambao unaunganisha mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma Km.205. | Malipo ya fidia yamekamilika na malipo ya awali kwa mkandarasi wa *lot A*. Usambazaji wa umeme kutoka Tulila wenye kV 33 umejengwa na unaingiza takribani MW.1.8 kutoka Tulila kwenda Songea. |
| 43(b)(iii) | Mradi wa Kaskazini (North-East) unaounganisha Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, mradi mwingine ni ule wa | Serikali imeanza majadiliano kwa ajili ya kulipa wananchi watakaoathirika kwa kuendelezwa kwa mradi huu na tathmini ya kijamii na ya kimazingira imekamilika. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | North-West, ambapo unaunganisha Mikoa ya Mbeya, Katavi, Rukwa na Kigoma. | |
| 43(c)(i) | Kuendelea kuongeza bajeti ya Wakala wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA) ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wenye uhakika. | Mwaka 2017/18, Serikali imetenga Shilingi bilioni 667.48 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 587.61 zilizotengwa katika Mwaka wa fedha 2016/17. |
| 43(c) (ii) | Kukamilisha utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini (*REA Turnkey Projects Phase* II) yenye lengo la kuunganisha wateja 250,000 utakapokamilika. | Mradi wa Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA Turn-key Projects phase II) umekamilika kwa asilimia 98. Jumla ya wateja 172,000 kati ya wateja 250,000 wameunganishwa na kazi inaendelea. |
| 43(c) (iii) | Kuanzisha REA (III) ambayo ina lengo la kuongeza wigo wa usambazaji umeme kutoka REA I na II zilipoishia; kufikisha umeme kwenye shule zote za sekondari, hospitali na vyanzo vya maji; kuongeza idadi ya vijiji ambavyo vinafikiwa na umeme; na maeneo yote ambayo si tija kwa TANESCO kuwekeza. | Duru ya kwanza ya Awamu ya Tatu ya Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme ambayo imeanza itahusisha kupatiwa umeme kwa vijiji 3,559 na vijiji vitakavyosalia vinavyofikia 4,314 vitapatiwa umeme katika duru ya pili ya Awamu ya Tatu ikihusisha maeneo yaliyopo nje ya gridi. Pia, umeme utapelekwa katika maeneo ambayo hayakupatiwa katika awamu mbili za mwanzo pamoja na taasisi za elimu, afya na pampu za maji katika maeneo ya vijijini. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 44 (a) | Kuwezesha na kusimamia ujenzi wa miundombinu muhimu ya gesi asilia na mafuta nchini pamoja na kukamilisha Mpango Kabambe wa matumizi ya gesi asilia *(Natural Gas Utilization Master Plan).* | Serikali imekamilisha ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na zoezi la usambaziji gesi asilia kwa matumizi ya viwandani na majumbani linaendelea kutekelezwa ambapo viwanda zaidi ya 36 vimeshaunganishwa na huduma hiyo Jijini Dar es Salaam. Pia, Serikali imeridhia ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi bandari ya Tanga -Tanzania. Aidha, Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia Awamu ya Kwanza imekamilika na maandalizi ya awamu ya Pili yanaendelea. |
| 44(b) | Kuhakikisha wananchi wanaopakana na miundombinu ya gesi na ambako bomba la gesi linapita wanashiriki na kunufaika na gesi. | Kampuni za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi zinalipa tozo ya asilimia 0.3 ya mapato kwa ajili ya maendeleo ya maeneo ambayo gesi inazalishwa. |
| 44(c) | Kuwawezesha wananchi kwa ujumla washiriki na wanufaike na fursa zinazotokana na uchumi wa gesi. | Maandalizi ya Kanuni mahsusi kwa ajili ya kusimamia ushiriki wa Watanzania katika sekta ya mafuta na gesi zimeanza kutumika tangu Mei, 2017. |
| 44(g) | Kuendelea kusomesha vijana wa kitanzania katika ngazi mbalimbali za vyuo vikuu, VETA kulingana na mahitaji ya rasilimali watu katika sekta ya mafuta na gesi. | Serikali kwa kushirikiana na nchi rafiki ikiwemo China imeendelea kutoa fursa za mafunzo kwa Watanzania kusoma shahada ya pili na ya uzamivu katika tasnia ya mafuta na gesi asilia. |
| 45(a) | Kuzalisha umeme wa jua usiopungua MW. 180; Jotoardhi MW. 200 kwa kuzingatia uwezo uliopo wa | Uhamasishaji wa wazalishaji wadogo wa umeme wa jua kwa kutumia gridi ndogo katika maeneo ambayo hayafikiwi na gridi ya taifa umeendelea ambapo hadi sasa kuna takribani MW. 10 zinazalishwa. Pia |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kuzalisha hadi MW. 5,000. | kuna miradi mikubwa ya Kishapu – Shinyanga MW. 150 unaotarajiwa kukamilika mwaka 2020 na Chuo Kikuu cha Dodoma MW. 55 unaotarajiwa kukamilika mwaka 2019 ambapo zote zipo katika hatua za utafiti wa awali. |
| 45(c) | Kufanya tafiti ili kubaini na kupanga vyanzo mbadala kwa miaka ijayo ili kuepusha Taifa kukosa nishati ya umeme. | Tafiti zimeendelea ambapo maeneo yenye fursa na rasilimali za nishati jadidifu yamebainishwa. TANESCO imetengeneza Ramani za maeneo yanayofaa kwa uwekezaji. |

## 2.9 Mawasiliano



*Moja ya minara wa mawasiliano ya Kampuni ya Simu mkoani Katavi.*



*Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Prof. Makame Mbarawa, akipewa maelezo juu ya mnara wa mawasiliano wa Kampuni ya Simu ya Halotel*

Serikali imeweka mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuinua sekta ya mawasilano ili kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.10

Bangokitita 10: Mafanikio Katika Sekta ya Mawasiliano

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 47 (d) | Kuunganisha katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano baadhi ya shule za msingi, shule zote za Sekondari, Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya/Polisi (OCD), Hospitali zote za Wilaya, Vyuo Vikuu vyote na Vituo vya Posta 65 ili kuweza kutumia fursa za TEHAMA hususan Elimu Mtandao, Maktaba Mtandao na Afya | Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya VIETTEL hadi kufikia mwezi Septemba, 2017 imefikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo yafuatayo:-<br>i) Ofisi za Halmashauri 117;<br>ii) Vituo vya Posta 71;<br>iii) Vituo vya Polisi 129;<br>iv) Hospitali za Wilaya 90;<br>v) Mahakama 27; na<br>vi) Huduma ya intaneti bure kwa miaka mitatu katika Shule 425. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Mtandao. | |
| 47 (f) | Kufikisha huduma za mawasiliano ya Simu za viganjani kwa wananchi wote kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) katika vijiji vyote vya Tanzania Bara na Zanzibar. | (i) Kata 443 zenye uhitaji wa huduma za mawasiliano zimepata wazabuni wa kupeleka mawasiliano husika. Kati ya kata hizo 443, upelekaji wa mawasiliano umekamilika katika kata 391. Aidha, Kata 52 zilizobaki zinategemewa kufikishiwa huduma hiyo kabla ya mwisho wa mwaka 2017.<br><br>(ii) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote pia umetoa zabuni ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata 75 zenye vijiji 154 ambazo zinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2018. Kutokana na mkataba ambao Serikali iliingia na Kampuni ya Viettel yakufikisha huduma ya mawasiliano katika vijiji 4,000, Kampuni hiyo imeweza kujenga minara na kufikisha huduma ya mawasiliano katika vijiji 3,069 ambapo vijiji 931 vilivyosalia vinatarajiwa kupata huduma mwaka 2017/18. |
| 47 (g) | Kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye Sekta ya Mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu gharama za mawasiliano ya simu. | (i) Serikali imenunua hisa zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya *Bhart Airtel* katika TTCL ili TTCL iweze kusimamia miundombinu ya kimkakati, kuhakikisha usalama wa mtandao, kujiendesha kibiashara na kumudu soko la ushindani. Hatua hii itaiwezesha TTCL kutoa huduma bora na kwa gharama nafuu.<br><br>(ii) Gharama za huduma za mawasiliano hapa nchini zinapungua kadri Mkongo |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | wa Taifa unavyotandazwa katika maeneo mbalimbali hususani vijijini. Aidha, Serikali imeweka bei elekezi/ukomo ya huduma za mawasiliano ya mwingiliano (Inteconnection) ambayo inatakiwa izingatiwe na watoa huduma wote wa mawasiliano kati ya mtandao mmoja na mwingine. |
| 47 (i) | Kuwalinda watumiaji wa simu za mkononi dhidi ya dhuluma, wizi na uhalifu wa mitandao. | (i) Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na Mkakati wake wa utekelezaji vinaelekeza kudhibiti dhuluma, wizi na uhalifu katika mtandao;<br><br>(ii) Usimamizi wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Huduma za ziada za mwaka 2015 umewezesha kwa kiasi kikubwa kudhibiti uhalifu wa mtandao.<br><br>(iii) Maboresho ya Mfumo wa Rajisi ya namba kwa kuunganisha katika mfumo wa Vitambulisho vya Taifa na usajili wa Vifaa vya Mawasiliano vya Mkononi (Central Equipment Identity Register – CEIR) vimesaidia kupunguza matumizi ya uhalifu kupitia mitandao; na<br><br>(iv) Elimu inatolewa kwa wananchi kuhusu uhalifu katika mtandao na namna ya kubaini uhalifu katika mtandao, kuchukua tahadhari na kutoa malalamiko au taarifa; |
| 47(j) | Kuongeza Idadi ya watumiaji mitandao (internet) kutoka **milioni 9.0** mwaka 2015 hadi kufikia | Kutokana na Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kuunganishwa kwenye maeneo mengi nchini, leseni kutolewa kwa kampuni zilizokidhi vigezo ili kutoa huduma |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | **milioni 20.0** mwaka 2020. | za Intaneti, na miundombinu ya kuwezesha upatikanaji wa huduma Intaneti ya kasi kote nchini kuboreshwa, matumizi ya intaneti yameongezeka kutoka **watumiaji 9,000,000** mwaka 2015 na hadi watumiaji **19,862,525** mwaka 2016. |

## *2.10 Huduma za Afya*



*Muonekano wa mbele wa jengo la hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi shirikishi Muhimbili (MUHAS) lililopo kampasi ya Mloganzila. lililofunguliwa rasmi na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akipata maelezo kuhusu mashine ya kufanya uchunguzi (MRI) wakati wa ufunguzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi shirikishi Muhimbili iliyopo kampasi ya Mloganzila.*

Serikali imeendelea kutekeleza dhamira ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa na wananchi wenye afya bora watakaoweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kuwapatia huduma bora za afya. Aidha, Serikali inaendelea kuongeza bajeti ya afya pamoja na kuhamasisha wananchi wajiunge na Mfuko wa Bima ya Afya ili waweze kupata huduma za afya wakati wote. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na. 11.

Bangokitita Na. 11: Mafanikio Katika Utoaji wa Huduma za Afya

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 50(a)(i) | Lengo la kila kijiji kuwa na Zahanati, Kata kuwa na Kituo | Vituo vya kutolea huduma za Afya vimeongezeka kutoka vituo 7,014 mwaka |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | cha Afya na Wilaya kuwa na Hospitali linaendelea kutekelezwa katika maeneo ambayo huduma hizi hazijakamilika pamoja na kujenga hospitali za wilaya katika wilaya zote mpya. | 2014/2015 hadi 7,284 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la **vituo 269.** Aidha, Halmashauri mpya na zile za zamani ambazo hazikuwa na hospitali zake za Wilaya sasa zimeanza kujenga hospitali za wilaya na ujenzi umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-<br><br>(i) **Halmashauri ambazo tayari zimeanza ujenzi;**<br>Buchosa DC, Mbinga TC, Ilemela DC, Nanyumbu DC, Busokelo DC, Kaliua DC, Tabora MC, Uyui DC, Mvomero DC, Momba DC, Ruangwa DC, Shinyanga DC, Buhigwe DC, Morogoro MC na Tunduma DC.<br><br>(ii) **Halmashauri ambazo ujenzi upo katika hatua za kupandisha hadhi Vituo vya Afya kuwa hospitali za Wilaya ni:-**<br>Ifakara TC (Kibaoni HC), Chalinze DC (Chalince HC), Nyang'wale DC (Khalumwa DC), Geita DC (Nzela HC), Kibaha DC (Mlandizi HC), Mtwara MC, Milele DC (Inyonga Disp), Madaba DC (Madaba HC), Musoma DC (Mrangi HC), Bunda TC (Manyamanyama HC), Nanyumbu DC (Dinyecha Disp.), Tarime DC (Nyamwaga Disp.), Mtwara DC na Nanguruwe (HC).<br><br>(iii) **Halmashauri ambazo zimetenga maeneo na kuanza maandalizi ya ujenzi;**<br>Kigamboni MC**,** Nyasa DC, Bumbuli DC, Ushetu DC, Rorya DC, Tanganyika DC, Chemba DC, MC, Kalambo D, Buchosa DC, Moshi MC, Njombe DC na Longido.<br><br>(iv) **Halmashauri ambazo tayari zina hospitali zenye hadhi ya wilaya;** |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Ubungo MC (Kituo cha Sinza (Palestina) kilipandishwa hadhi), Makambako DC (Hospitali ya Makambako inaendelea kupanuliwa), Busokelo DC (wanatumia Itete Lutheran CDH), Butiama DC wanaendelea na upanuzi wa miundombinu na Songwe DC (wanatumia Mwambaniu DDH). |
| 50(a)(ii) | Hospitali za Rufaa za Mikoa zinaendelea kuimarishwa na kukamilisha ujenzi kwa mikoa mipya na ile ambayo haina hospitali hizo. | Mikoa mipya ya Simiyu, Geita, Njombe, Katavi na Songwe ilianzisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa. Ujenzi upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-<br><br>(i) **Mkoa wa Simiyu;**<br>Jumla ya ekari 100 zimetengwa na jengo la OPD limefikia hatua ya kuezeka.<br>(ii) **Mkoa wa Katavi;**<br>Eneo lenye jumla ya ekari 243 limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa na tayari Mkandarasi yupo eneo la ujenzi kwa ajili ya hatua za mwanzo za ujenzi.<br>(iii) **Mkoa wa Geita;**<br>Eneo la ekari 103 limetengwa na ujenzi umeanza.<br>(iv) **Mkoa wa Njombe;**<br>Eneo la ekari 70 limetengwa na ujenzi wa Hospital ya Mkoa uko katika hatua ya kukamilika.<br>(v) **Mkoa wa Songwe;**<br>Eneo la ujenzi linaandaliwa na ramani ya jengo la OPD inaendelea kuandaliwa. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 50 (a)(iii) | Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Afya kwa kupitia Sera ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). | Serikali iliingia Mkataba na watoa huduma binafsi (Service Level Agreement) ili kupunguza ulazima wa Halmashauri kujenga vituo vipya vya huduma za afya sehemu ambapo kuna vituo vya Sekta Binafsi. Katika makubaliano hayo, ya Halmashauri 39 zinatumia Hospitali teule kama Hospitali za Wilaya. |
| 50(a)(iv) | Hospitali za Rufaa za Kanda zitaendelea kuimarishwa na kujenga hospitali nyingine tatu kwa ajili ya Kanda ya Kusini, Kati na Magharibi. | Awamu ya Kwanza ya jengo la Wagonjwa wa nje na Mapokezi pamoja na uzio wenye urefu wa Km. 2.7 la Hospitali ya Mtwara kwa ajili ya Kanda ya Kusini limekamilika. Kwa upande wa hospitali ya kanda ya magharibi ambayo itajengwa Tabora, **Shilingi milioni 100** zimetengwa kwenye bajeti ya 2017/18 kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi wa hospital hiyo. |
| 50(a)(v) | Kudahili **wanafunzi 15,000** katika Vyuo vya Afya na Ustawi wa Jamii ifikapo mwaka 2020 ikiwa ni jitihada za kutosheleza mahitaji ya rasilimali watu katika sekta hii. | Udahili wa wanafunzi tarajali wanaodahiliwa katika vyuo vya afya umeongezeka kutoka **wanafunzi 13,002** mwaka 2015/16 hadi **wanafunzi 13,632** mwaka 2016/2017. Aidha, katika mwaka 2016/2017, jumla ya **wanafunzi 1,277** walidahiliwa kwenye Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambapo **wanafunzi 428** walidahiliwa katika ngazi ya **Cheti, 375** ngazi ya Diploma, 422 ngazi ya Shahada na 52 ngazi ya Shahada ya Juu. |
| 50(a)(vi) | Kukarabati, kujenga na kupanua miundombinu katika vyuo vya mafunzo ya afya na kushirikisha Sekta Binafsi katika uendeshaji wa vyuo. | Katika mwaka 2016/17, vyuo 14 vimeboreshewa miundombinu yake na kati ya hivyo, vyuo 12 vimekamilika na kukabidhiwa kwa watumiaji. Serikali pia imenunua vifaa vya Maabara za vitendo kwa ajili ya kufundishia kwa vyuo 10 vya utabibu, uuguzi na ukunga. |
| 50(a)(vii) | Kuajiri wataalamu zaidi wa afya kutoka ndani na nje ya | Kati ya mwaka 2015/16 hadi 2016/17, jumla ya vibali vya **ajira 3,408** vimetolewa kwa |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | nchi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma za afya. Aidha, hospitali za wilaya zitaendelea kuimarishwa kwa kuzipatia madaktari, wauguzi, dawa na vifaa tiba vya kutosha. | awamu mbili vikihusisha vibali vya **madaktari 258** awamu ya kwanza na Awamu ya Pili **vibali 3,150.** Aidha, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka **Shilingi bilioni 31** mwaka 2015/16 hadi kufikia **Shilingi bilioni 260** mwaka 2017/18. Hadi mwezi Juni, 2017, **asilimia 83** ya dawa muhimu zaidi (essential medical items) zinapatikana katika Bohari ya Dawa na hali ya upatikanaji wa dawa kwenye vituo kufikia mwishoni mwa mwezi Julai 2017 ni **asilimia 86.3.** |
| 50(a)(ix) | Kujenga nyumba za watumishi karibu na vituo vya kutolea huduma. | Serikali kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Taasisi ya Benjamini Mkapa kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa **nyumba 200** za watumishi katika **Mikoa 9** ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Tanga, Manyara, Pwani na Simiyu. Ujenzi wa **nyumba 132** umekamilika na ujenzi wa **nyumba 68** unaendelea. Kukamilika kwa nyumba hizo kutaongeza idadi ya nyumba za watumishi zilizojengwa kupitia mradi huu na kufikia **nyumba 480** katika maeneo yenye mazingira magumu. |
| 50(b)(i) | Kuwagawia **wananchi 22,360,386** vyandarua vyenye viuatilifu bila malipo. | Katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2016/17, Serikali ilisambaza **vyandarua 27,189,572** (sawa na asilimia 122 ya lengo) vyenye viuatilifu na kuvigawa bure kwa wananchi katika mikoa 23. |
| 50(b)(ii) | Kutekeleza mpango wa upuliziaji wa viuatilifu ukoko katika kuta za nyumba ili kuua mbu wanaoeneza malaria katika Mikoa ya Kigoma na Lindi. | Upuliziaji wa dawa yenye viatilifu ukoko ndani ya nyumba ulifanyika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo ina maambukizi makubwa zaidi ya malaria hapa nchini ambayo ni (Kagera, Mwanza, Mara na Geita). |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 50(b)(iv) | Kununua na kusambaza dawa za malaria katika vituo vyote vya kutolea huduma nchini. | Katika mwaka 2015/16 hadi 2016/17, dozi **37, 181,550** za dawa mseto na vitepe vya **mRDT milioni 33** vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. |
| 50(c) | Kuimarisha upatikanaji wa huduma za dharura na za kawaida kwa wagonjwa kupitia vituo vya huduma za afya nchini. Huduma hizo ni pamoja na magonjwa ya saratani, mishipa ya fahamu, mapafu, figo, huduma za magonjwa ya moyo, upasuaji mbalilmbali ikiwamo upasuaji wa mifupa. | **Huduma za Dharura**<br>Watoa huduma wamepewa mafunzo ya kutoa huduma wakati wa dharura na maafa pamoja na kuandaliwa Mwongozo wa kufundushia timu za dharura, Mwongozo wa kufanya mazoezi ya dharura katika sekta ya afya, Mpango wa Sekta ya Afya wa kukabiliana na maafa na dharura za aina zote, Mpango wa kudhibiti kipindupindu, Mpango wa kukabiliana na sumukuvu na Mwongozo wa kufundisha utoaji huduma kwa majeruhi wengi. Uratibu wa utoaji huduma za afya wakati wa dharura na maafa katika sekta ya afya umeboreshwa kwa kuanzishwa Public Health Emergence Operation Centres (PHEOC).<br><br>**Upatikanaji wa huduma nyingine za Afya wakati wa Kawaida (Pamoja na huduma za Kibingwa)**<br>Upatikanaji wa huduma zitolewazo katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili imeimarishwa kama ifuatavyo:<br><br>(i) Wodi 5 za ICU zinafanyiwa ukarabati utakaoongeza vitanda vya ICU kutoka 21 na kufikia 75.<br><br>(ii) Mashine **14** za upasuaji (Diathermy Machines) na Mashine kubwa mbili **(2)** za utakasishaji vifaa zimenunuliwa. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (iii) Mashine ya **CT-Scan** mpya yenye uwezo wa "slice" **128** imenunuliwa.<br><br>(iv) Mashine za *ventilators, monitors na anaesthesia* zimefanyiwa ukarabati.<br><br>(v) Jengo kuu la upasuaji kwa mama wajawazito na jengo la upasuaji wa watoto linakarabatiwa. Ukarabati huo utaongeza vyumba vya upasuaji **6** na kufanya Hospitali iwe na jumla ya vyumba **19**.<br><br>(vi) Upanuzi wa jengo la kusafisha figo umefanyika ambao utaongeza vitanda **27** na kufikia jumla ya vitanda **42**<br><br>(vii) Wataalamu saba (7) wamepelekwa nchini India kwa ajili ya mafunzo ya upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia (Cochlear Implants) kwa wagonjwa wenye matatizo ya kusikia. |
| 50(e) | Kuunganisha hospitali za rufaa za Mikoa na Wilaya na hospitali nyinginezo kwenye mfumo wa matibabu mtandao (telemedicine). | (i) Serikali kwa kushirikiana na wadau imeanzisha kituo kinachotumia huduma ya tiba mtandao (telemedicine) kwenye Kijiji cha Ololosokwani kilichopo Wilaya ya Ngorongoro. Kituo hicho kimeunganishwa na Hospitali ya Muhimbili na KCMC hivyo mgonjwa anaweza kutibiwa na daktari bingwa kutoka hospitali hizo.<br><br>(ii) Serikali pia, imeziunganisha hospitali za Rufaa za Mikoa ya Morogoro, Lindi na Hospitali za Rufaa za Wilaya za Kilosa, Turiani (DDH), Nachingwea, Mafia, Nyangao (DDH) na Hospitali ya Taifa |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Muhimbili kwenye Mfumo wa Tiba Mtandao. |
| 50(f) | Halmashauri za Wilaya zitaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kununua vifaa vya kujimudu kwa lengo la kuwawezesha watu wenye ulemavu. | Katika mwaka 2016/2017, Halmashauri zilitenga na kutumia **Shillingi milioni 68.7** kuwezesha **watoto 3,535** wenye ulemavu wa ngozi kwa kuwapatia chakula, matibabu na uchunguzi wa kiafya. Katika mwaka 2017/2018, Halmashauri zimetenga **Shilingi milioni 247** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kujimudu kwa walemavu. |
| 50(g) | Bohari ya Dawa itakamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika Mikoa ya Tanga, Tabora. Mtwara na Dar es Salaam. Serikali itaendelea kushirikisha Sekta Binafsi kuwezesha upatikanaji wa dawa pale zinapokosekana katika Bohari ya Dawa kwa kuongeza Washitiri Binafsi 17 katika mikoa tisa kwa ajili ya ununuzi wa dawa pale ambapo hazipo Bohari ya Dawa. | Bohari ya Dawa (MSD) imekamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika Mikoa ya Tanga na Tabora.. |
| 50(I) | Kuunganisha mifumo ya ukusanyaji na utoaji taarifa za afya ili kufikia lengo la kuwa na mfumo mmoja unaokusanya na kutoa taarifa za afya nchini. Aidha, mfumo wa ukusanyaji taarifa kwa njia ya simu za mkononi utasambazwa nchi nzima. | (i) Serikali inatumia mfumo wa Kielektroniki wa "District Health Information System (DHIS2)" kupokea takwimu za huduma za Afya kutoka vituo vyote vya Serikali, Mashirika ya Dini na Binafsi. Kwa sasa mfumo huu umeunganisha zaidi ya program 35 ambazo taarifa zake zinapatikana kwenye mfumo.<br><br>(ii) Serikali pia, imeanzisha matumizi ya mifumo ya Kielektroniki katika |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | kukusanya Takwimu kwa kutumia mfumo wa *Government of Tanzania Hospital Management Information System* (GoT- HoMIS) na *electronic Medical Records* (eMR) ambayo inasaidia watumishi kukusanya takwimu katika vituo vya kutolea huduma na kuziwasilisha kielektroniki ili kuziingiza katika mfumo wa DHIS2 kwa uchambuzi na matumizi katika ngazi mbalimbali. Aidha, mfumo wa matumizi ya simu za mkononi umeanza kutumika kutolea taarifa magonjwa ya milipuko. |
| 50(j) | Kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi kuwa na Bima ya Afya ili kumudu gharama za matibabu. | Serikali inaandaa Mkakati wa Ugharamiaji wa Huduma za Afya ambao utawezesha kuwepo kwa Mfumo wa Bima Moja ya Afya kwa wananchi wote, ili kufikia lengo la Serikali la afya kwa watu wote (universal health coverage).<br><br>Hadi kufikia mwezi Juni 2017, idadi ya watanzania waliokuwa wamejiunga na mfuko wa Bima ya Afya imeongezeka kufikia **asilimia 34** kutoka **asilimia 19** ya mwaka 2015. Uhamasishaji kwa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi kujiunga na Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) unaendelea katika mikoa mbalimbali nchini. Pia, Waheshimiwa Wabunge wameingizwa katika utaratibu utakaowawezesha kupata huduma za afya kwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. |
| 50(k) (i) | Kununua mashine za mionzi (LINAC machine) kwa ajili ya tiba ya Saratani. | (i) Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la “bunker” katika Taasisi ya Saratani ya Ocen Road ambapo mashine za |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | mionzi za LINAC pamoja na CT Simulator zitasimikwa. Usimikaji wa mashine hizo utakamilika Februari 2018.<br><br>(ii) Ujenzi wa kituo cha tiba za saratani awamu ya kwanza kati ya nne katika Hospitali ya KCMC inayojumuisha jengo la kliniki kwa ajili ya wagonjwa wa saratani na jengo la tiba ya dawa (Chemotherapy) imekamilika. Aidha, hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za juu Kusini – Mbeya imefanywa kituo cha tiba ili kuwezesha huduma hizo kutolewa katika kiwango kikubwa zaidi. |
| 50(k)(iv) | Kuimarisha mtandao wa Hospitali za Taifa pamoja na Huduma za Ubingwa wa Juu zikiwemo zile za upasuaji wa moyo; huduma kwa wagonjwa wa saratani; upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu na upasuaji kupitia tundu dogo kwa kutumia kifaa maalumu ikiwa ni pamoja na kuchuja damu na kupandikiza figo kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo. | Masuala makubwa yafuatayo yamefanyika:<br><br>(i) **Huduma za matibabu ya moyo - JKCI**<br>Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKC) imewahudumia jumla ya wagonjwa wa moyo wanaotibiwa na kurudi nyumbani **37,199** mwaka 2016/17 ikilinganishwa na **wagonjwa 24,570** waliopatiwa huduma hiyo mwaka 2015/2016; kufanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa **236; wagonjwa 608** kupatiwa matibabu maalum kupitia **tundu dogo kwa kutumia mtambo wa kisasa** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 190** ikilinganishwa na **wagonjwa 290 waliohudumiwa katika mwaka wa fedha 2015/16.** Vilevile, JKCI ilifanya kambi 3 za upasuaji kwa kushirikiana na wataalam kutoka |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Israel, Ujerumani na Australia) na Serikali imewapeleka **madaktari 9** wa JKCI kwenye masomo ya juu katika fani ya moyo.<br>(ii) **Huduma za tiba ya mifupa na mishipa ya fahamu - MOI**<br>Taasisi ya MOI imeongezwa uwezo, ikiwemo **Shilingi bilioni 13** katika mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Jengo la MOI Awamu ya Tano na ununuzi wa vifaa Tiba. Kutokana na uwezeshaji huo, Taasisi imewahudumia jumla ya **wagonjwa 126,410;** imeanza kutoa huduma ya upasuaji wa migongo ya watoto iliyopinda (paediatric scoliotic spine correction); kufanya upasuaji mkubwa kwa wagonjwa 496, ikijumuisha **wagonjwa 67** waliofanyiwa upasuaji wa **nyonga, 62 mgongo, 55 Ubongo, 262** watoto wenye vichwa vikubwa na watoto **50** wenye mgongo wazi; na watoto **2,200 walifanyiwa uchunguzi ambapo watoto 250** walifanyiwa **upasuaji kwa** mafanikio na kutoa mafunzo kwa Madaktari wa upasuaji wa kawaida katika hospitali za rufaa za mikoa/kanda nchini katika kambi tiba zilizofanyika katika **Mikoa 18.** |
| 50(m) | Kukamilisha ujenzi wa hospitali za Mloganzila, Mtwara na Benjamini Mkapa – Dodoma. | Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa – DODOMA imekamilika na kuanza kazi na kufunga mitambo ya uchunguzi wa magonjwa ikiwemo MRI, CT Scan, Mammgrapgh, General purpose X-ray, Flluroscopy, Utrasound, Dental unit na Dental X-ray machine. Vilevile, Hospitali ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Mloganzila imekamilika na kufunguliwa mwezi Novemba, 2017. |
| 50(Q)(i) | Kuzijengea uwezo Hospitali na Vituo vya Afya ili kutoa huduma kamili ya Afya ya Uzazi na Mtoto pamoja na upasuaji kwa mama wajawazito. | Hadi sasa jumla ya **vituo 106** kati ya **vituo 535** vya Serikali sawa na **asilimia 20** vimejengewa uwezo wa kutoa huduma kamili ya Afya ya Uzazi na Mtoto. Aidha, Serikali inaendelea kujenga uwezo kwa **vituo 172** kwa kukarabati na kununua vifaa. Ukarabati wa vituo hivyo utawezesha jumla ya **vituo 278** sawa na **asilimia 52** ya **vituo vyote 535** vya Serikali kutoa huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji wa kutoa mtoto tumboni. |
| 50(Q)(ii) | Kuanzisha Benki za Damu katika Mikoa itakayoanza kutekeleza mpango wa kutoa huduma kamili ya afya ya Uzazi na Mtoto. Vilevile, huduma za uzazi wa mpango zitapewa kipaumbele. | Hadi sasa benki za damu za mikoa saba zimeanzishwa katika mikoa ya Dar es salaam, Lindi, Morogoro, Dodoma, Iringa, Kigoma na Shinyanga. Aidha, uanzishwaji wa benki hizo katika mikoa ya Mara na Kagera upo katika hatua za mwisho. |
| 50(Q)(iii) | Kuzijengea uwezo zahanati na vituo vya afya katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Kigoma kutoa huduma ya msingi ya dharura ya Afya ya Uzazi na Mtoto. | Jumla ya watoa huduma za **afya 1,061** walipewa mafunzo ya huduma muhimu za dharura kwa matatizo yatokanayo na uzazi na watoto wachanga kutoka katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Dar es Salaam, Mtwara, Kagera, Lindi, Mara, Tabora, Morogoro, Iringa, Geita, Rukwa, Ruvuma, Njombe, Kigoma, Singida. |
| 50(Q)(v) | Kuendelea kutekeleza mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto. | (i) Serikali inatekeleza Mpango wa kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) lengo likiwa ni kupunguza hadi asilimia 4 ifikapo 2021. Hadi kufikia Mwaka 2016, maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua hadi kufikia **asilimia 7.6** kutoka **asilimia 26** ya mwaka 2011.<br><br>(ii) vituo vinavyotoa huduma za afya ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | uzazi na mtoto vimeongezeka kufikia **vituo 5,806,** sawa na **asilimia 94** mwaka 2016 kutoka vituo **vituo 5,063** ambayo ni **asilimia 86** mwaka 2015.<br><br>(iii) Idadi ya akina mama waliokutwa na maambukizi walioanzishiwa dawa ARVs imeongezeka kutoka **asilimia 90** ya mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 98** kwa mwaka 2016.<br><br>(iv) Mfumo maalum (Mother Child Cohort Monitoring System) wa kuwafuatilia kina mama na watoto wao kwa pamoja wanapoanza dawa za ARVs hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka miwili umeanzishwa. Mfumo umeanza kutumika katika mikoa ya Tabora, Tanga, Pwani, Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam. Mafunzo kwa ajili ya watumishi kuwajengea uwezo wa kutumia mfumo huu katika mikoa yote yanaendelea.<br><br>(v) Kati ya 2015 hadi Desemba 2016 jumla ya **wahudumu 660** ngazi ya Jamii na wasimamizi **147** kutoka mikoa 14 yenye asilimia kubwa ya maambukizo ya VVU ya Dar es Salaam, Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Simiyu, Dodoma, Rukwa, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Njombe Simiyu Ruvuma wamepata mafunzo ya kuboresha utendaji kazi wao. |

## 2.11 Elimu, Sayansi na Teknolojia



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akiongozana na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam Prof. Rwekaza Mukandala wakati akiwasili kuzindua majengo mapya ya mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam eneo la Mlimani jijini Dar es Salaam.*



*Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimuangalia mwanafunzi wa Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko mara baada ya kuzindua zoezi la usambazaji wa vifaa vya elimu maalum nchini vilivyonunuliwa na Serikali.*

Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza Mpango wa Elimu Bila Malipo kuanzia shule za msingi hadi sekondari. Hatua hiyo imesaidia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa. Serikali pia imeongeza juhudi katika kujenga maabara, kusambaza vifaa vya maabara na kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Masomo ya Sayansi. Vilevile, bajeti ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeongezwa na idadi ya Wanafunzi wanaopata Mkopo wa Elimu ya Juu imeongezeka. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.12.

Bangokitita Na.12: Mafanikio Katika Sekta za Elimu, Sayansi na Teknolojia

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 47(a) | Kuanzisha vituo vya ubunifu ili kukuza makampuni ya TEHAMA yanayoibukia kwa lengo la kuongeza ajira kwa vijana. | (i) Mfuko Maalum wa Kuendeleza Ubunifu katika Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia umeanzishwa. Vituo saba (7) vya ubunifu, sawa na **asilimia 17.5** vimeanzishwa katika taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka 2016/17.<br>(ii) Serikali imeendesha mafunzo ya jinsi ya kuanzisha vituo vya ubunifu |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | kwa Taasisi saba (7) za Elimu ya Juu. Mafunzo haya yamewezesha kuanzishwa kwa atamizi (incubators) katika Vyuo Vikuu vya Tumaini (Kiota Hub), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Sokoine (SUGECO), Dodoma na Zanzibar (SUZA). Katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali imeanza kuendesha mafunzo ya kufungua atamizi zijulikanazo kama *Virtual incubator* katika Serikali za Mitaa, Manispaa na Majiji. Kazi hii imeanza katika mkoa wa Mwanza.<br>(iii) Serikali imetoa mafunzo kwa wahariri 40 wa vyombo vya habari kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi wa kuandaa taarifa za sayansi na utafiti katika namna ambayo watumiaji wa taarifa hizo wataelewa kirahisi. |
| 47(c) | Kuendeleza matumizi ya teknolojia ya nyuklia katika tiba ya saratani na kuongeza vituo kutoka vituo viwili vya sasa (OCRI na BMC) hadi sita vitakavyohudumia kanda mbalimbali nchini. Vituo vinne vitakavyoongezwa ni: Hospitali ya Rufaa Mbeya, Mnazi Mmoja (Zanzibar), KCMC pamoja na Dodoma. | (i) Mashine za kuchunguza na kutibu ugonjwa wa saratani zimeshasimikwa katika Hospitali ya Bugando (BMC) na Mafunzo kwa wataalamu katika Hospitali ya Bugando (BMC) yanatolewa.<br>(ii) Kutokana na uhamasishaji wa Serikali kwa Sekta Binafsi, vituo viwili vya binafsi vinavyotoa huduma ya matibabu ya saratani kwa kutumia mionzi vimekaguliwa, kusajiliwa na kupewa leseni. Vituo hivyo ni "*Besta Specialized Polyclinic"* pamoja na Hospitali ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | Agha Khan vilivyopo Dar es Salaam. |
| 52 | Serikali inasimamia Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa kuandaa mfumo, muundo na taratibu nyumbufu za kutoa Elimu ya Awali na Elimumsingi (1+6+4) bila malipo. | Serikali ya Awamu ya Tano ilianza kutoa elimu bila malipo kuanzia shule za msingi hadi sekondari tangu Januari, 2016. Serikali ilianza kwa kutenga Shilingi bilioni 18.77 kila mwezi kwa ajili ya kugharama elimu bila malipo. Mwezi Julai 2016, kiasi hicho kiliongezwa hadi kufikia **Shilingi bilioni 23.868,** na hivyo kufanya Serikali kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 465.6** kugharamia elimu bila malipo hadi mwezi Agosti, 2017. |
| 52 (a)(i) | Uandikishwaji rika lengwa la watoto wa Darasa la Elimu ya Awali unaongezeka kutoka asilimia 45 mwaka 2015 hadi 100 mwaka 2020. | Kwa kuanzia, walimu 16,129 wanaofundisha Elimu ya Awali wamepatiwa mafunzo kazini yaliyolenga kuimarisha ufundishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). |
| 52(a)(ii) | Uandikishwaji rika lengwa la watoto wa Darasa la Kwanza unaongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2015 hadi 100 mwaka 2020. | (i) Idadi ya wanafunzi walioandikishwa Darasa la I imeongezeka kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 2,120,667 mwaka 2016.<br>(ii) Kwa mwaka 2016/2017, Serikali imefanya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya madarasa na vyoo katika shule za msingi 142 kwa lengo la kuongeza uandikishwaji wa |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | wanafunzi wa elimu ya awali na msingi. |
| 52(a)(iii) | Uandikishwaji rika lengwa la Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza unaongezeka kutoka asilimia 60 mwaka 2015 hadi asilimia 80 mwaka 2020. | Wanafunzi waliofaulu Mtihani wa Elimu ya Msingi na kujiunga Kidato cha Kwanza wameongezeka kutoka 518,038 mwaka 2015 hadi 538,826 mwaka 2016. |
| 52(b)(i) | Asilimia 20 ya wahitimu wa Elimumsingi wanaendelea na masomo katika ngazi za Sekondari ya Juu na asilimia 80 kuendelea na elimu au mafunzo ya ufundi katika ngazi ya Cheti, Stashahada au Shahada kulingana na sifa, vipaji au vipawa. | (i) Shule zenye kidato cha tano zimeongezeka kutoka shule 276 mwaka 2015 hadi shule 345 mwaka 2017. Asilimia 15.4 ya wanafunzi waliohitimu Kidato cha Nne mwaka 2015 walijiunga na Kidato cha Tano mwaka 2016.<br>(ii) Idadi ya wanafunzi waliojiunga na mafunzo ya ufundi katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada iliongezeka kutoka 117,067 mwaka 2014/2015 hadi 125,004 mwaka 2015/2016. |
| 52(b)(ii) | Asilimia 80 ya wahitimu wa Elimu ya Sekondari ya Juu kujiunga na Elimu ya Juu ya Taaluma na asilimia 20 kuendelea na Elimu ya Ufundi, katika ngazi ya cheti, stashahada au shahada kulingana na sifa. | (i) Usajili wa Vyuo vipya binafsi vya Ufundi Stadi vipatavyo 30 umefanyika. Hatua hii itaongeza uwezo wa Vyuo vya Ufundi kudahili wanafunzi wengi zaidi<br>(ii) Chuo cha Ufundi Arusha, katika mwaka wa masomo 2016/17 kimedahili jumla ya wanafunzi 1,111. Kati ya hao wanafunzi 952 ni wa Ufundi Sanifu (Technicians), wanafunzi 119 ni wa Uhandisi (Engineers), na Astashahada 40. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 52(b)(iii) | Asilimia 70 ya wahitimu wa Elimu au Mafunzo ya Ufundi na Taaluma wanapata ajira kwa kujiajiri au kuajiriwa. | Serikali imeanza kutekeleza Programu ya Kuongeza Ujuzi wa Kuweza Kuajiriwa au Kujiajiri (ISTEP) kuanzia Novemba 2015 itakayowanufaisha watanzania 1,200 kwa kuanzisha Mashirikiano saba (7) (Institutional Partnership) kati ya Taasisi na Vyuo vya Canada pamoja na Taasisi na Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Tanzania ili kujenga uwezo wa kufundisha kwa umahiri stadi zinazohitajika katika Sekta za Uchimbaji wa Madini, Mafuta, Gesi na Sekta ya Utalii. |
| 52 (c ) | Kudurusu na kuhuisha muundo wa mitaala ili elimu katika ngazi mbalimbali ikamilike kwa muda wenye tija na itilie maanani matokeo ya kusoma yenye kujenga ujuzi, maarifa ya kujitegemea, weledi na kuwawezesha wahitimu kumudu na kufanya kazi mbalimbali za kuajiriwa au kujiajiri. | Serikali imepitia Mtaala na Mihtasari ya Elimu ya Awali, Darasa la I –VI kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kuandaa Miongozo ya walimu wa Elimu ya Awali, Darasa la I –VI kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili kuhakikisha kuwa wahitimu wa ngazi hizo wanapata ujuzi na maarifa stahiki. Mihtasari ya Elimu ya Awali, Darasa la I na II na Darasa la II na IV imehuishwa kuendana na mtaala ulioboreshwa katika ngazi hizo. |
| | | (i) Jumla ya mitaala 87 ya kada za Sayansi (Science and Allied Technology - SAT), Elimu (Teaching and learning facilitation - TLF), Afya (Health and Allied Science - HAS) na Biashara, Mipango na Utalii (Business Tourism and Planning - BTP) imehuishwa.<br><br>(ii) Serikali imefanya uhakiki wa Mitaala 15 ya Programu za mafunzo kutoka Vyuo vinne (4); imefanya uidhinishaji wa baadaye (post validation) mitaala |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | 16 kutoka vyuo vitano (5) na kufanya uhakiki wa awali (pre-validation) wa mitaala 45 ya programu mbalimbali za mafunzo. Aidha, ufuatiliaji na tathmini katika vyuo 103 umefanyika ili kuangalia kiwango cha ubora wa elimu. |
| 52(d)i | Kuhakikisha kuwa ufaulu wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi unaongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi asilimia 90 mwaka 2020 na asilimia ya wanafunzi wanaoendelea na Kidato cha Kwanza kuongezeka kutoka asilimia 55.5 hadi asilimia 100. | (i) Serikali imeimarisha Mfumo wa Udhibiti Ubora ndani ya Shule kwa kutoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na mafunzo kuhusu usimamizi wa elimu katika ngazi ya shule kwa wajumbe 129,609 wa Kamati za Shule za Msingi zipatazo 11,647. Aidha, Walimu wa Elimu ya Awali 16,129, Walimu 33,180 wa Darasa la I – II pamoja na Walimu 32,053 wa Darasa la III na IV wamepewa mafunzo kuhusu ufundishaji wa KKK kati ya walimu 205,166 wa elimu za msingi.<br>(ii) Ufaulu katika Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 70.3 mwaka 2016. |
| 52(e)(ii) | Programu tatu (3) au zaidi za mafunzo zinaanzishwa zenye kukidhi mahitaji na kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kulingana na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa. | Katika mwaka 2016/2017, Maombi ya kuidhinisha programu mpya na kuhuisha 106 yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya programu hizo, programu 75 zimekidhi vigezo vya kuanza kufundishwa katika vyuo vikuu. Kwa mwaka 2016/17 uanzishwaji wa programu mpya za mafunzo umeongezeka kwa asilimia 29.24. |
| 52(e)(iii) | Kuhakikisha kuwa asilimia 70 ya wahitimu katika ngazi zote | (i) Serikali inaendelea na mkakati wa kukamilisha maabara tatu (3) za |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | wanakuwa katika mrengo wa Sayansi, Ufundi, Hisabati na Teknolojia. | Sayansi katika kila shule. Kwa sasa shule za Serikali zenye maabara ni 2,141 kati ya 3,614 na zisizo za Serikali zenye maabara ni 1,075 kati ya 1,145. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya maabara vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 16.9** kwa Shule za Sekondari 1,696 kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Masomo ya Sayansi kwa nadharia na vitendo.<br>(ii) Mafunzo ya walimu 5,920 wa Sayansi na Hisabati ngazi ya Stashahada yanaendelea katika Vyuo vya Ualimu.<br>(iii) Serikali ilitoa nafasi 219 za ajira kwa Mafundi Sanifu Maabara mwaka 2017. Hadi kufikia Juni, 2017 wameshaajiriwa Mafundi Sanifu Maabara 137. |
| | | (iv) Chuo cha Ufundi na Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo cha Ufundi cha Karume Zanzibar (KIST) na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) vimeanzisha kozi mpya za fani ya Mafuta na Gesi, na Teknolojia ya mashine nzito za viwandani (Heavy Duty Equipment Engineering) zitakazosaidia ukuzaji wa viwanda. |
| 52(f)(i) | Kuhakikisha kuwa uwiano wa kitabu cha kiada kwa mwanafunzi katika Elimumsingi unaongezeka kutoka 1:3 mwaka 2015 hadi 1:1 mwaka 2020. | Serikali imeandaa na kuchapisha vitabu vya kiada vya Sekondari Kidato 1 hadi 4 vya Sayansi Jamii na Lugha nakala 1,958,628; Vitabu vya Sekondari Kidato cha 5 – 6 nakala 151,055; Vitabu vya Darasa la I – II nakala 6,862,800; na |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 52(f)(ii) | Asilimia 50 ya fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule zinatumika kuchapisha na kusambaza vitabu vya kiada. | Vitabu vya Darasa la III nakala 6,818,181. |
| 52(g)(i) | Asilimia 100 ya wahitaji wa mikopo kwa ajili ya kusomea fani ya udaktari wanapata mikopo. | Kwa 2016/17, jumla ya wanafunzi 1,940 waliodahiliwa katika fani za Udaktari na Sayansi za Afya walipatiwa mikopo. Nafasi zisizopungua 2,500 za mikopo zimetengwa kwa ajili ya wanafunzi watakaodahiliwa katika fani za Tiba na Afya katika mwaka wa masomo wa 2017/18. Kwa mwaka 2016/2017 hadi mwaka 2017/18, kuna ongezeko la mkopo kwa asilimia 22.4 kwa ajili ya wanafunzi wanaosomea fani ya Udaktari. |
| 52(g)(ii) | Ufadhili wa Nafasi 500 za masomo ya fani ya udaktari zinapatikana kila mwaka ili kupunguza pengo la uhaba wa madaktari nchini. | |
| 52(g)(iii) | Asilimia 100 ya wale wenye mahitaji maalumu, vipaji na vipawa watakaotambulika watapata fursa za kuendelea na masomo katika ngazi mbalimbali. | (i) Jumla ya wanafunzi 44,546 wenye ulemavu wa aina mbalimbali walitambuliwa na kuendelezwa. Kati ya hao, wanafunzi 37,034 ni wa shule za msingi na 7,512, katika shule za sekondari. Aidha, Vifaa vya kielimu na visaidizi kwa ajili ya viziwi na wasioona vimesambazwa katika shule 213 za msingi na shule 22 za sekondari za wanafunzi wenye mahitaji maalum.<br><br>(ii) Katika mwaka wa masomo 2016/17, idadi ya wanafunzi 2,756 wenye mahitaji maalum walipatiwa mikopo. Kati yao, wanafunzi 1,269 ni yatima, 604 wenye mzazi mmoja, 660 waliofadhiliwa na Taasisi mbalimbali katika elimu ya Sekondari na 223 walikuwa wanafunzi walemavu. |
| 52(g)(iv) | Shule moja maalumu ya Ufundi (Specialized Technical | Shule za Sekondari za Serikali saba (7) za Ufundi zilizopo (Ifunda, Iyunga, Tanga, |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Schools) au zaidi inaanzishwa kila Mkoa ambayo itadahili wanafunzi wenye vipaji mbalimbali na kuwaendeleza kwenye fani mbalimbali zenye tija kwa maendeleo ya Taifa. | Mtwara, Moshi, Musoma na Bwiru Boys) ni miongoni mwa shule kongwe zinazofanyiwa ukarabati na Serikali, ambapo ukarabati katika shule ya Sekondari Iyunga umekamilika. Asilimia 14 ya ukarabati kwa Shule 7 za ufundi umekamilika. |
| 52(h)(i) | Asilimia 80 ya walimu wanaandaliwa na kutumia TEHAMA kufundishia katika ngazi zote. | (i) Mafunzo kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji yametolewa kwa walimu 2,229 wa Shule za Sekondari. Aidha, Shule za Serikali 50 ambazo ni vituo vya mafunzo kazini kwa walimu zina maabara ya kompyuta, TV Set na Projector kwa ajili ya kuwezesha ufundishaji kwa kutumia TEHAMA. Wakufunzi 70 walipatiwa mafunzo kupitia mradi wa majaribio ya kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza kwa kutumia TEHAMA katika shule 21 za sekondari na Mkataba kwa ajili ya ununuzi wa Kompyuta 400 kwa ajili ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi umetiwa saini.<br><br>(ii) Katika mwaka 2016/2017, Vyuo 40 vya Elimu ya Ufundi vimepatiwa jumla ya kompyuta 400 kwa lengo la kuandaa walimu kutumia TEHAMA katika ufundishaji. |
| 52(h)(ii) | Asilimia 70 ya taasisi zote zinazotoa elimu na mafunzo zinaunganishwa katika Mkongo wa Taifa. | Vyuo vya Ualimu vyote 35 vimeunganishwa na Mkongo wa Taifa. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 52(j)(i) | Uondokaji wa walimu, wakufunzi na wahadhiri unapungua kutoka wastani wa asilimia 0.8 mwaka 2015 hadi asilimia 0.2 mwaka 2020. | (i) Shule za Sekondari 40 zimejengewa nyumba za walimu zinazojitegemea na Shule 183 zimejengewa nyumba sita (6) katika moja (6 in One) kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kuishi walimu.<br><br>(ii) Serikali kupitia MMES II imeweka miundombinu ya maji na umeme katika shule 792. Jumla ya shule za msingi 3,818 kati ya 17,174 na za sekondari 2,246 kati 4,759 zimeunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa. |
| 52(j)(ii) | Tatizo la uhaba wa walimu wapatao 24,000 wa masomo ya sayansi na hisabati kwa shule za Sekondari linapungua kwa kutoa mafunzo kwa walimu 5,000 wa masomo hayo kila mwaka. | Mwaka 2017, nafasi za ajira zimetolewa kwa walimu 4,129. Hadi kufikia Juni 2017 walimu 3,463 waliohitimu mwaka 2015 wameajiriwa. Asilimia 69.3 ya walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati wameajiriwa kwa mwaka 2016/17. |
| 52(j)(iii) | Idadi ya Wahadhiri wanaongezeka kutoka Wahadhiri 6,880 mwaka 2015 hadi Wahadhiri 10,000 mwaka 2020. | Katika mwaka 2017/18, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya kusomesha Wahadhiri 100 kwa ngazi ya uzamili na uzamivu. Serikali imewezesha upatikanaji wa ufadhili wa wahadhiri 122 kusoma nchi za nje. |
| 52(k)(ii) | Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha Mkoa wa Kagera utafanyika. | Ardhi ya kujenga Chuo hicho imepatikana katika eneo la Burugo, Wilaya ya Bukoba Vijijini. Utafiti wa stadi mbalimbali zitakazofundishwa chuoni umeshafanyika. |
| 52(k)(iv) | Udahili katika vyuo vya Ufundi vya Kati unaongezeka kutoka wastani wa wanafunzi 30,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi | Udahili katika vyuo vya kati umeongezeka kutoka wanafunzi 96,694 mwaka 2015/16 hadi wanafunzi 111,958 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 3.7 |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | 285,600 mwaka 2020. | |
| 52(k)(v) | Udahili katika ngazi ya Shahada unaongezeka katika Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka wastani wa wanafunzi 60,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 117,000 mwaka 2020. | (i) Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa iliongezeka kutoka 65,064 (Wanaume 42,839 na wanawake 22,225) mwaka 2015/2016 hadi kufikia wanafunzi 69,539 (wanaume 42,180 na wanawake 27,359) ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 4,475.<br><br>(ii) Serikali imeongeza Bajeti ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka **Shilingi bilioni 365** mwka 2015 hadi **Shilingi bilioni 483** mwaka 2017 na kuwezesha idadi ya Wanafunzi wanaopata Mkopo wa Elimu ya Juu kuongezeka kutoka 98,300 mwaka 2015 hadi wanafunzi 125,000 mwaka 2017. |
| 52(n)(i) | Mchango wa Sekta Binafsi katika kudahili wanafunzi katika Vyuo vya Ufundi ngazi ya kati unaongezeka kutoka asilimia 21 mwaka 2015 hadi asilimia 25 mwaka 2020. | Vyuo vya elimu ya ufundi katika sekta binafsi vinavyotoa mafunzo ngazi ya kati kwa mwaka 2016 vimedahili jumla ya wanafunzi 39,024 kati ya Wanafunzi wote 111, 958 katika Vyuo vya Elimu ya Kati. Udahili huo ni asilimia 34.8 ya udahili wote katika vyuo hivyo. |

## *2.12 Maji*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, akimtwisha ndoo ya maji mkazi wa kijiji cha Mabama, wilayani Uyui, Tabora wakati akizindua mradi wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 29.*



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akimtwisha ndoo ya maji Bi. Leonara Kibuno wa Kijiji cha Magingo, kata ya Mkongotema wilayani Songea mara baada ya kuzindua mradi maji.*

Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wote hususan wale wanaoishi maeneo ya vjijini pamoja na usafi wa mazingira. Aidha, Serikali inajenga na kukarabati skimu za umwagiliaji za wakulima ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali maji. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.13.

Bangokitita Na. 13: Mafanikio Katika Sekta ya Maji

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 54(a) | **2.12.1 Maji Safi**<br><br>Kuboresha huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 67.7 mwaka 2015 hadi asilimia 85 mwaka 2020. | Hadi Septemba 2017, jumla ya miradi 1,423 imekamilika na kufanya jumla ya vituo vya maji vilivyojengwa kwenye miradi kufikia 117,190. Vituo hivyo vina uwezo wa kuhudumia watu 29,297,500, sawa na asilimia 79. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| 54(b) | Kuboresha huduma ya Maji Mijini. | Serikali imeboresha huduma ya maji katika maeneo ya mijini kama ifuatavyo;<br><br>(i) Kukamilisha miradi ya maji katika Miji ya Bukoba, Dodoma, Sengerema na Nansio<br>(ii) Upanuzi wa Mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini, Ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa bomba kuu kutoka Ruvu Chini hadi matanki ya Chuo cha Ardhi kwa Jiji la Dar es Salaam umekamilka Agosti, 2017.<br>(iii) Ujenzi wa miradi katika Miji ya Sumbawanga, Lindi, Kigoma na Musoma inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;<br>(iv) Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe, Katavi na Songwe inaendelea kutekelezwa.<br>(v) Miradi ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya ya Simanjiro, Longido, Kilosa, Turiani, Mvomero, Gairo, Mafinga, Bunda, Chunya ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.<br><br>(vi) Serikali imekamilisha upanuzi na ukarabati wa mtambo wa kuchuja na kutibu maji, Manispaa ya Tabora. |
| 54(c) | Kukamilisha miradi mikubwa ya maji na kuhakikisha vijiji vyote vilivyopo kandokando ya miradi hiyo mikubwa vinanufaika. | (i) **Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Igunga, Nzega, Sikonge na Tabora**<br><br>Ujenzi wa mradi huu umeanza Agosti, 2017 ambapo Wakandarasi watatu (3) wanaendelea na kazi. Mradi unatarajiwa kukamilika baada ya miezi 30. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (ii) **Mradi wa kutoa maji kutoka mto Malagarasi kwa Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka**<br><br>Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya Upembuzi wa awali ambapo na sasa anaendelea na usanifu wa kina. Mradi ukikamilika utanufaisha wakazi wapatao **607,086.**<br><br>(iii) **Mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Mkoa wa Simiyu**<br><br>Upembuzi yakinifu wa mradi huu utakaonufaisha wakazi **wapatao 834,204** umekamilika na Mtaalamu Mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa mradi.<br><br>(iv) **Mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Isaka na Kagongwa**<br><br>Serikali inatekeleza mradi wa maji kwenda katika Miji ya Isaka na Kagongwa kwa kutumia chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria kupitia bomba kuu la **Kashwasa.** Kwa sasa Wakandarasi wapo katika hatua za matayarisho ya kuanza ujenzi (*mobilisation*).<br><br>(v) **Mradi wa Maji Same-Mwanga-Korogwe**<br>Mradi unatarajiwa kunufaisha jumla ya watu 438,931. Hadi sasa ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa mitambo ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | kuchuja maji, ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji na ujenzi wa matangi ya kuhifadhi maji kabla ya kuyasambaza kwa watumiaji umefikia asilimia 43 na utakamilika Mei, 2018. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika Mji wa Same wenye wakazi wapatao 97,400 umeanza tarehe 1 Juni, 2017 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2019. |
| 54(d) | Kupanua na kuboresha miradi ya maji ya kitaifa. | (i) **Mradi wa Kitaifa Chalinze:** Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji Chalinze ambao unatoa huduma ya majisafi katika vijiji **47** vilivyopo katika Mkoa wa Pwani **(vijiji 42)** na Morogoro **(vijiji 5)** imekamilika. Mradi huo unawanufaisha wakazi **197,648** wa Wilaya za Morogoro Vijijini, Bagamoyo na Kibaha.<br><br>(ii) **Mradi wa Maji Makonde:** Serikali imekamilisha ukarabati wa visima virefu sita (6) eneo la Mitema na kufunga pampu katika visima hivyo. Kukamilika kwa kazi hizo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 7.4** hadi **lita milioni 14.8** kwa siku na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo yanayohudumiwa na mradi huo.<br><br>(iii) **Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga chini ya KASHWASA,** Serikali imekamilisha kupeleka maji katika Miji ya Maganzo, Mwadui, Kolandoto na Kishapu. Ujenzi wa miundombinu |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | ya maji kwenda Miji ya Nzega, Igunga, Uyui na Tabora na vijiji vilivyopo kando kando ya bomba kuu kwa umbali wa kilomita 12 unaendelea.<br><br>(iv) **Mradi wa Maji Maswa,** Serikali inatekeleza mradi wa kujenga chujio la maji katika Mji wa Maswa litakaloweza kuchuja maji kiasi cha mita za ujazo 10,368 kwa siku, ambapo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 75. Jumla ya watu **111,669** wa Mji wa Maswa na **Vijiji 11** watanufaika na mradi huo unaotegemewa kukamilika Desemba 2017. |
| 54(e) | Kuanzisha miradi ya ujenzi wa mabwawa katika mikoa yenye ukame. | Serikali imefanya utafiti katika maeneo yenye ukame nchini na kubaini maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa katika Halmashauri za Mlele, Bahi, Mpwapwa, Chemba na Sumbawanga. Usanifu wa Bwawa la Nsekwa umekamilika, na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. |
| 55(d) | Kuendelea kuhamasisha wananchi kuunda Jumuiya za Watumia Maji Vijijini katika Mabonde yote ya maji nchini ifikapo mwaka 2020 ili kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji. | (i) Serikali imeendelea kuelimisha, kuunda na kuimarisha Jumuiya za Watumia Maji ili ziweze kusimamia rasilimali za maji katika ngazi ya chini. Hadi sasa zipo jumla ya Jumuiya za Watumia Maji 103 kwa mabonde yote tisa (9).<br><br>(ii) Serikali imetoa miongozo kwa watekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji kuhusu namna bora ya kuunda, kusajili na kuvijengea uwezo Vyombo vya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | Kijamii vya Watumiaji maji Vijijini (*Community Owned Water Supply Organizations – COWSOs*). Hadi kufikia Septemba 2017 jumla ya *COWSO* **2,285** zilikuwa zimeundwa na kusajiliwa. |
| 55(e) | Kujenga na kukarabati Maabara za Maji kwa ajili ya kusimamia ubora wa maji nchini na kutoa taarifa za hali ya ubora wa maji kila mwaka. | (i) Ujenzi wa Maabara ya maji Kigoma umekamilika na ukarabati wa jengo la Maabara Kuu ya Maji Dar-es-Salaam kazi imefikia asilimia **98.**<br>(ii) Ujenzi wa Maabara katika ofisi za Bonde la Mto Ruvuma umefikia asilimia **80** na kwa Ofisi za Mtwara na Songea ujenzi umefikia asilimia **40.**<br>(iii) Ujenzi wa Maabara katika Ofisi za Bonde la Ziwa Rukwa, Sumbawanga ni asilimia **60** na Mbeya ni asilimia **70**.<br>(iv) Ujenzi wa Maabara za Mwanza, Bukoba na Musoma umefikia asilimia **90.**<br>(v) Kwa kipindi cha miaka miwili, jumla ya sampuli 14,776 zilikusanywa kutoka maeneo mbalimbali nchini na kuhakikiwa ubora wake kulingana na viwango vilivyowekwa kwa ajili ya kulinda afya za wananchi, ambapo sampuli 14,179 zilihakikiwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na matokeo yalionesha kuwa asilimia 81 ya sampuli hizo zilikidhi viwango vinavyokubalika. Vilevile, sampuli 901 za majitaka zilihakikiwa ubora wake kabla ya kumwagwa kwenye mazingira ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na matokeo yalionesha kuwa asilimia 46 ya sampuli hizo hazikukidhi viwango vinavyokubalika na ushauri stahiki ulitolewa. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 55(f) | Kuziongezea uwezo wa kiutendaji taasisi zinazoshughulika na Sekta ya Maji ambazo ni Chuo cha Maji, Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na Bohari Kuu ya Maji ili kuongeza ufanisi wa taasisi hizo. | Taasisi za Sekta ya Maji zimeongezewa uwezo wa kiutendaji kama ifuatavyo:<br><br>(i) Madarasa manne na viti **401** vimeongezwa katika Chuo cha Maji na Mtandao wa TEHAMA (*Local Area Network*) umewekwa katika majengo yote ya chuo hicho na kimeunganishwa na Mkongo wa Taifa (*Government Optic Fibre network*). Pia vitabu **822** vilinunuliwa kwa ajili ya maktaba.<br><br>(ii) Katika mwaka 2017/2018, jumla ya **Shilingi 690,669,000** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa *Earth Moving Machines*; **Shilingi 300,000,000** kwa ajili ya kununua *Geophysical Equipment* na **Shilingi 600,000,000** kwa ajili ya Ukarabati wa *Mechanical Workshop*.<br><br>(iii) Serikali imejenga ukuta kuzunguka eneo lote la Bohari Kuu ya maji na imekarabati ghala moja kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vya maji. |
| 55(g) | Kuendelea kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika matumizi endelevu na usimamizi bora wa rasilimali za majishirikishi. | (i) Nchi za Tanzania na Malawi zimeanza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe.<br><br>(ii) Awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria *(Lake Victoria Environmental Management Project – LVEMP II)* inatekelezwa na Serikali kwa pamoja na nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda. Hadi Agosti 2017, miradi 284 ya jamii yenye thamani ya **Dola za Marekani 4,659,633.94** imekamilika na kati ya hiyo, miradi |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | **253** imefanyiwa tathmini na kukabidhiwa kwa Halmashauri **23** zinazotekeleza miradi hiyo ambayo ipo katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita, Kagera na Mara kwa ajili ya uendelezaji. |
| 55(h) | Kuweka mfumo madhubuti na endelevu wa utunzaji wa vyanzo vya maji na udhibiti wa uchafunzi wa vyanzo hivyo. | Serikali inatekeleza Mpango Maalum wa Utunzaji na Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji nchini katika Mabonde Madogo ya Ruvu Mkoani Morogoro na Zigi Mkoani Tanga. Jumla ya vyanzo vya maji 258 vimeainishwa katika Mpango wa utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji ambapo vyanzo tisa (9) vimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji; vyanzo vya maji 43 vimewekewa mipaka; na vyanzo 16 vipo katika hatua mbalimbali za kuwekewa mipaka. |
| 55(i) | Kufanya tafiti za upatikanaji maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuendeleza rasilimali hiyo kwa matumizi mbalimbali. | Utafiti wa kubaini maeneo ya maji chini ya ardhi umefanyika katika maeneo 211 yakiwemo maeneo 15 katika Bonde la Kati, maeneo matatu (3) katika Bonde la Ziwa Nyasa, maeneo 22 Bonde la Ziwa Rukwa, maeneo 26 katika Bonde la Mto Rufiji na maeneo 145 katika Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini. |
| 55(j) | Kuimarisha mtandao wa ukusanyaji takwimu za rasilimali za maji kwa ajili ya kupata taarifa sahihi za hali ya rasilimali za maji nchini ili kuwezesha mgawanyo mzuri wa maji na kupunguza migogoro baina ya watumia maji. | Serikali imeimarisha mtandao wa ukusanyaji takwimu kwa kukarabati vituo 36 na kujenga vituo 12 vya hali ya hewa sehemu mbalimbali nchini. |
| 55(k) | Kuanzisha Mfuko wa Maji wa Taifa *(National Water Investment Fund)* kwa ajili ya | Mfuko wa Maji wa Taifa (NWIF) umeanzishwa kwa mujibu wa kifungu 44 cha Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kuharakisha ujenzi wa miradi nchini. | Mazingira Na. 12 ya Mwaka 2009. Mfuko ulianza rasmi kutekeleza majukumu yake Februari 2016. Chanzo cha fedha kwa ajili ya Mfuko huo ni tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita moja ya mafuta ya petroli na dizeli inayouzwa nchini. Fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji nchini. |
| | **2.12.2 Majitaka** | |
| 55(a) | Kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya uondoaji majitaka nchini. | Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji mbalimbali nchini kama ifuatavyo:-<br>(i) Imekamilisha usanifu wa mradi wa Majitaka katika Mji wa Musoma na mkandarasi wa kutekeleza mradi huo amepatikana.<br>(ii) Imekamilisha usanifu wa mradi katika Mji wa **Bukoba** ambapo maandalizi ya kumpata mkandarasi wa kutekeleza mradi pamoja na Mtaalam Mshauri atakayesimamia kazi za ujenzi yanaendelea. Ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza Desemba 2017.<br>(iii) Serikali imekamilisha Mradi wa Uondoaji Majitaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la wastani wa hekta 108.<br>(iv) Serikali imekamilisha usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa uondoaji majitaka katika Mji wa Singida.<br>(v) Jiji la Dar es Salaam linatekeleza mradi wa uondoaji majitaka kwa gharama ya **Dola za Marekeni milioni 89** ili kuongeza wastani wa huduma ya uondoaji majitaka kutoka |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | asilimia 10 hadi asilimia 30 mwishoni mwa mwaka 2017. Mradi huo utahusu upanuzi wa miundombinu ya majitaka kwenye maeneo ya katikati ya Jiji na ujenzi wa miundombinu mipya katika maeneo mbalimbali ya Jiji. Vilevile, mradi huo utahusisha ujenzi wa mitambo mitatu (3) ya kisasa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Jangwani, Kurasini na Mbezi Beach.<br><br>(vi) Serikali imekamilisha usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi ya miradi wa uondoaji majitaka katika Miji ya Tanga, Tabora na Iringa.<br><br>(vii) Mkandarasi anaendelea kukamilisha upanuzi wa mtandao wa Majitaka katika Manispaa ya Morogoro kwa gharama ya **Shilingi milioni 494** na atakamilisha kazi hiyo Juni 2018. |
| **2.12.3 Umwagiliaji** | | |
| 22(c)(v) | Kujenga, kukarabati na kuboresha skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo na wa kati ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali maji. | (i) Ujenzi wa makinga maji matatu (3), usakafiaji wa mifereji yenye urefu wa mita 100 na ujenzi wa kivuko cha mifugo, katika skimu yenye hekta 290 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2016/2017 umekamilika Julai 2017.<br><br>(ii) Uchimbaji na usakafiaji wa mfereji mkuu wenye urefu wa mita 740 ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2016/2017 umekamilika Julai |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | 2017 katika skimu ya **Hangangadinda** yenye hekta 250 katika Halmashauri ya Mji Mdogo wa Madaba.<br><br>(iii) Usakafiaji wa mfereji mkuu wenye urefu wa mita 115 na ujenzi wa vigawa maji saba (7) katika skimu ya **Igongwa** yenye hekta 300 katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2016/2017 umekamilika August 2017.<br><br>(iv) Uchimbaji wa utoro wa maji (spilway) katika bwawa la Usoke Mlimani yenye hekta 200 katika Halmashauri ya Urambo ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2016/2017 umekamilika Julai 2017.<br><br>(v) Serikali imeingia mkataba na Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa (DDCA) wa kukamilisha ujenzi wa utoro wa maji (spilway) katika bwawa la Dongobesh katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu. |
| | 22(C)(viii) Kuijengea uwezo Tume ya Umwagiliaji ili iongeze kasi ya ujenzi wa miundombinu. | Wataalamu saba wa umwagiliaji kutoka Kanda za Morogoro, Dodoma (Kati) na Mbeya walipata mafunzo juu ya ubainishaji, uandaaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya umwagiliaji. Vilevile, vitendea kazi kama vile magari, kompyuta *na GPS* vilinunuliwa. |

## *2.13 Kuimarisha Muungano*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kuhusu masuala ya Muungano mjini Zanzibar.*

Katika jitihada za kuimarisha Muungano wetu, Serikali imetafutia ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoukabili kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na maendeleo. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.14.

Bangokitita Na. 14: Kuimarika kwa Muungano

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| 143(a) | Kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. | (i) Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa Vikao vya Kisekta vya Ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano ili kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu. Katika kipindi cha Novemba, 2015 hadi Septemba, 2017, Sekta za Nishati, Maji, Utumishi na Utawala Bora, Viwanda na Biashara, Maliasili na Utalii, Afya na Mazingira zilikutana.<br><br>(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ilitembelea Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar; Miradi mbalimbali inayotekelezwa na SMZ pamoja na Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar.<br><br>(iii) Kamati ya Mawasiliano na Ardhi ya Baraza la Wawakilishi ilifanya ziara kwenye Taasisi za Muungano na zisizo za Muungano zilizopo Tanzania Bara kwa lengo la kujua utendaji kazi wa taasisi hizo. |
| 143(b) | Kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizokuwepo kwa kuweka utaratibu wa kikatiba na kisheria wa kutatua changamoto zitakazojitokeza. | Katika kipindi hiki kimefanyika kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ tarehe 5 Januari 2017, Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ tarehe 13 Januari 2017 na kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ chini ya Uongozi wa Makamu wa Rais tarehe 13 Januari, 2017. Kupitia vikao hivyo changamoto zimejadiliwa na ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya changamoto zinatafutiwa ufumbuzi ni za masuala ya fedha; masuala |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | ya ajira katika taasisi za Muungano na hoja ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. |
| 143(c) | Kuendelea kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha uchumi katika pande mbili za Muungano hususan katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa manuafaa ya pande zote. | (i) Serikali imefuatilia utekelezaji wa miradi na programu za pamoja zinazotekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi hiyo ni pamoja na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund-TASAF III); Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini – MIVARF; na Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth-(SWIOFISH).<br><br>(ii) Programu ya TASAF III imekuwa na mafanikio kwa wananchi wa pande mbili za Muungano ambapo ruzuku zinazotolewa kwa walengwa zimewasaidia kupata mahitaji ya msingi yakiwemo ya chakula, mahitaji ya shule kwa watoto na miradi midogomidogo ya kujiongezea kipato.<br><br>(iii) Programu ya MIVARF imetekelezwa kwa mafanikio kwa wananchi wa pande mbili za Muungano kwa kujenga |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | miundombinu muhimu ya masoko kuongezewa thamani ya mazao yao, kuwajengea uwezo na kuwaunganisha na masoko na huduma za fedha vijijini. Aidha, kwa maeneo yanayopitiwa na barabara zilizojengwa na programu hii, shughuli za kiuchumi zimeongezeka na hivyo kuongeza kipato kwa jamii.<br><br>(iv) Mpango wa MKURABITA umeendelea na shughuli za kuandaa, kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Umiliki Rasilimali na Uendeshaji Biashara utakaoboresha sheria, kanuni na taratibu za kijamii. Mpango huu umekuwa na faida kwa wananchi kwani wameweza kurasimisha rasilimali na biashara wanazomiliki na kuzitumia kupata mitaji na kuongeza kipato.<br><br>(v) Mradi wa SWIOFish umeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi kwa lengo la kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi. |

## 2.14 Utawala Bora na Demokrasia



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akiwaaga marais wastaafu wakati wa sherehe ya Uhuru wa Tanzania Bara tarehe 9 Desemba 2017 katika uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma.*

Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuimarisha utawala bora na demokrasia kwa kupambana kwa dhati dhidi ya vitendo vya rushwa, ufisadi na uhujumu uchumi ili kutoa haki na huduma bora kwa wananchi na kutokomeza umaskini katika jamii yetu. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.15.

Bangokitita Na. 15: Kuimarika kwa Utawala Bora na Demokrasia

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 145(a) | Kuendeleza jitihada za kukuza, kulinda na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala wa Sheria katika ngazi zote za uongozi. | Kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na:<br>(i) Kukamilisha tafiti juu ya Sheria zinazolinda Haki za Wazee, Haki za Walaji na Sheria zinazosimamia |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu;<br><br>(ii) Kupokea malalamiko yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ambapo jumla ya malalamiko 5,994 yalichunguzwa yakiwemo malalamiko mapya 336 na 5,658 ya zamani. Malalamiko 618 yamefungwa na 5,376 yanaendelea na uchunguzi;<br><br>(iii) Kugawa nakala 7,114 za machapisho yanayohusu, haki za binadamu na utawala bora kwa wananchi pamoja na kuendesha vipindi tisa (09) vya redio na televisheni vya elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora. |

| | | |
|---|---|---|
| 145(c) | Kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na pia kuanzisha Mahakama Maalumu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa lengo la kuharakisha uchunguzi na utoaji hukumu kwa makosa hayo. | Mahakama Maalumu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imeanzishwa. Hadi Juni 2017, jumla ya mashauri thelathini (30) yalipokelewa ambapo mashauri nane (8) yamesikilizwa kwenye masjala ya Dar Es Salaam na Mashauri 22 yamesikilizwa katika masjala ndogo zilizopo kwenye kanda mbalimbali za Mahakama Kuu ya Tanzania. |
| 145(d) | Kuimarisha mfumo wa utoaji haki kwa kufanya maboresho katika utendaji wa vyombo vya maamuzi ikiwemo Mahakama, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. | Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:<br><br>(i) Kufanya Mapitio ya Sheria ya Ushahidi (Evidence Act), Sheria ya Usuluhishi (Arbitration), Sheria zinazohusiana na Ufilisi (*The Legal Framework Relating to Insolvency*), Mfumo wa Sheria Zinazosimamia Utoaji wa Mikopo na Usajili wa Dhamana (*Establishment of Secured Credit Transactions and Collateral Registry*) na Sheria Zinazosimamia Mfumo wa Haki Jinai (Criminal Justice). Kazi hii inatakamilika Juni, 2018;<br><br>(ii) Kufuatilia na kufanya tathmini ya Usimamizi na Ukaguzi wa shughuli za kimahakama katika mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Pwani, Singida, Tabora, Mwanza na Mara zikiwemo Mahakama za Mwanzo 26; Mahakama za Wilaya 18 na Mahakama za Hakimu Mkazi 6; |

| | | |
|---|---|---|
| | | (iii) Kusambazwa nakala 2,600 za Kitabu cha Mwongozo wa Ukaguzi wa Shughuli za Kimahakama katika ngazi zote za Mahakama nchini;<br>(iv) Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga na Mahakama ya Mwanzo Kawe;<br>(v) Kukamilisha ukarabati mkubwa wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Watoto Mkoa wa Mbeya. |

## *2.15 Vyombo vya Ulinzi na Usalama*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akiwapungia mkono wananchi wakati akiingia uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma, kwenye sherehe ya Uhuru wa Tanzania Bara zilizofanyika tarehe 9 Desemba 2017.*



*Viongozi wa vyombo vya Ulinzi na Usalama wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara zilizofanyika katika uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma, tarehe 9 Desemba 2017.*

Serikali inaendelea kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kutekeleza mikakati mbalimbali: Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.16.

Bangokitita Na. 16: Kuimarika kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **2.15.1 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** | | |
| 146 | Kuimarisha uwezo wa vikosi vya Zimamoto na Uokoaji kwa kuvipatia mafunzo na zana za kisasa za kupambana na matukio ya | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepatiwaa magari 18 ya kuzima moto, magari mawili ya uokozi, gari moja la kubebea wagonjwa pamoja na vifaa vya kuzima moto na maokozi. Vilevile, Maafisa na Askari 106 |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | moto na pia vifaa vya kuokoa maisha ya watu kutokana na majanga ya asili na ajali | wamepatiwa mafunzo ya kuzima moto na maokozi ndani ya nchi, na Maafisa na Askari 17 wmepatiwa mafunzo hayo nje ya nchi. |
| 146 (i) | Kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu. | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeongezewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo limepewa **Shilingi bilioni 3.5** katika mwaka 2016/17 na 2017/18. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pia limeajiri askari wapya 481 tangu awamu ya tano imeingia madarakani na katika mwaka huu wa fedha (2017/18), Jeshi linataraji kuajiri askari wapya 600. |

## 2.15.2 Jeshi la Polisi

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 146 (i) | Kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu. | (i) Jeshi la Polisi limeongezewa bajeti kama ifuatavyo: Mwaka 2015/16, jumla ya **Shilingi 489,627,345,000.00** zilitengwa; mwaka 2016/17 **Shhilingi 535,211,306,105.00** na 2017/18 **Shilingi 598,466,220,000.00** zimetengwa.<br>(ii) Katika mwaka 2015/16 hadi 2016/17 askari wapya 3,164 waliajiriwa kwa ajili ya kuongeza ufanisi. |
| 146 (ii) | Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo makazi, mafunzo na zana za kazi za kisasa. | Serikali imeboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya ulinzi na usalama kwa kufanya yafuatayo:<br>(i) Kulipa posho ya fidia ya msamaha wa kodi kwa askari kwa kiasi cha **Shilingi 100,000** kwa mwezi; |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (ii) Kuwapatia Askari **1,150** mafunzo mbalimbali ya kutoa huduma bora kwa jamii, mbinu za upelelezi na mafunzo ya mbinu za kijeshi nchini, na askari **173** walipata mafunzo nje ya nchi;<br><br>(iii) Askari **4,137** Wamepandishwa vyeo katika mwaka 2016/2017;<br><br>(iv) Jumla ya **Shilingi 12,534,856,056.14** ambazo ni madeni zimelipwa kwa askari/watumishi hadi sasa;<br><br>(v) Magari 231 yamenunuliwa;<br><br>(vi) Nyumba 353 za makazi ya askari Mkoa wa Kipolisi Kinondoni zipo hatua ya umaliziaji;<br><br>(vii) Upanuzi wa Chuo cha Polisi Moshi umeanza;<br><br>(viii) Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa Helkopta ya Jeshi la Polisi kwa gharama ya Shilingi bilioni moja;<br><br>(ix) Kituo cha Kisasa cha Mawasiliano (**Call Centre**) kimejengwa katika Mkoa wa Dar-es-Salaam kinawezesha wananchi kutoa taarifa ya matukio kwa urahisi na ndani ya dakika 15 Askari wanakuwa tayari wako katika eneo la tukio;<br><br>(x) Vifaa maalumu (Global Positioning System (GPS) vimefungwa katika magari ya Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni kwa ajili ya kudhibiti na kufuatilia wahalifu na uhalifu.<br><br>(xi) Magari 26 yaliyokuwa mabovu katika Mkoa wa Dar es Salaam yamefanyiwa ukarabati mkubwa. |
| 146 (v) | Kuendeleza na kuimarisha | Katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | mpango wa ulinzi shirikishi na kuwashirikisha wadau mbalimbali nchini kutoa elimu kwa umma dhidi ya imani potofu zinazosababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi (albino). Aidha, hatua kali za haraka na za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kujihusisha na uhalifu wa aina hii, ujambazi na vitendo vyovyote vyenye mwelekeo wa ugaidi. | ya Awamu Tano hakuna vitendo vya ukatili au mauaji dhidi ya wenye ulemevu wa ngozi ambavyo vimeripotiwa nchini.<br><br>Mkoa wa Kipolisi Rufiji umeanzishwa ili kudhibiti matukio ya ujambazi mkoa wa Pwani. |
| 146 (vi) | Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka hasa ugaidi, uharamia, Utakatishaji wa Fedha haramu (Money Laundering), biashara Haramu ya Dawa za kulevya na usafirishaji wa binadamu. | Jeshi la Polisi lilianzisha Kikosi Kazi *Transnational Organized Crime Unit* (TOCU) kinachokusanya na kuchambua taarifa za uhalifu na wahalifu wa kimataifa kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi. Kupitia Kikosi hicho, jumla ya kilogramu 12 na gramu 732.5 za dawa za viwandani zilikamatwa na watuhumiwa 462 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Aidha, makosa 852 ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliripotiwa na watuhumiwa 96 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. |
| **2.15.3 Jeshi la Magereza** | | |
| 146 (i) | Kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu. | (i) Maofisa/Askari na watumishi raia 2,886 walipata mafunzo mbalimbali katika kipindi husika. Kati ya hao 1,540 walihudhuria mafunzo ndani ya Jeshi na maofisa/askari na |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | watumishi raia 1,346 walihudhuria mafunzo yanayohusu taaluma mbalimbali nje ya Jeshi.<br><br>(ii) Jumla ya Shilingi bilioni 20.53 zililipwa zikiwa ni madeni watumishi, wazabuni na huduma ya umeme.<br><br>(iii) Serikali imelipatia Jeshi la Magereza matrekta 50 aina ya yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.01 na matengenzo ya zana za kilimo ya Shilingi 22,130,000 yamefanyika.<br><br>(iv) Ujenzi wa majengo 12 ya ghorofa katika eneo la gereza la Ukonga ambao ukikamilika utakuwa na uwezo wa kutoa huduma ya makazi kwa familia 320 umeanza.<br><br>(v) Ununuzi wa vitendea kazi na malighafi za viwanda vidogovidogo vinavyotumika kwa ajili ya shughuli za urekebishaji umefanyika. Viwanda hivyo ni vya ufumaji-Gereza Butimba- Mwanza, KPF-Morogoro na Isanga- Dodoma. Vingine ni viwanda vya utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mianzi - Gereza la Njombe - Iringa na vifaa vya Henzerani Gereza Bangwe na Ukonga -Dar es Salaam.<br><br>(vi) Jumla ya hekta 235 zimelimwa kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **2.15.4 Idara ya Uhamiaji** | | |
| 146 (i) | Kuviwezesha Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu. | (i) Ununuzi wa magari 16 kwa viongozi wa Idara ya uhamiaji umefanyika.<br>(ii) Idara ya Uhamiaji iliajiri askari wapya 297 ambao wamepangiwa kufanya kazi katika mikoa mbalimbali hapa nchini.<br>(iii) Vitabu vya kuchapa Pasipoti 150,000 vimenunuliwa pamoja na malighafi zake. |
| 146 (ii) | Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo makazi, mafunzo na zana za kazi za kisasa. | (i) Serikali imekamilisha ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Pwani na Singida pamoja na Ngudukitu-Pemba na inaendelea kukamilisha ujenzi katika Mikoa ya Geita, Mtwara, Lindi na Mtwara. Aidha, Nyumba tano (5) za makazi kwa Makamishna na nyumba za maafisa wa Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Ruvuma zimekamilika.<br>(ii) Ukarabati wa Chuo cha Uhamiaji Cha Kikanda Moshi umekamilika.<br>(iii) Maafisa **223** walipata mafunzo kwa ajili ya kupandishwa vyeo, na askari **35** walihudhuria mafunzo nje ya nchi.<br>(iv) Maafisa na askari 2,583 wanaendelea kulipwa posho ya chakula, likizo na uhamisho. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| **2.15.5 Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa** | | |
| 146(I) | Kuviwezesha vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu. | (i) Serikali imetangaza ajira mpya kwa vijana 3,000 waliopo katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).<br><br>(ii) Jumla ya Maafisa Wanafunzi 783 walitunukiwa kamisheni baada ya kukamilisha mafunzo na hivyo kuongeza wataalam katika Jeshi ambapo Wanaume walikuwa 704 wanawake 79.<br><br>(iii) Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kulipia meli kubwa na boti za doria za Jeshi la Wanamaji na hivyo kuongeza uwezo wa Jeshi kufanya doria katika Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone- EEZ) na Operesheni za Kupambana na Uharamia na Uharibifu wa Mazingira. |
| 146(ii) | Kuendelea kuboresha maslahi ya Watendaji katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama Ikiwemo Makazi, Mafunzo na zana za kazi za Kisasa. | Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya Wanajeshi wake kama ifuatavyo:<br><br>(i) Kuwapatia wanajeshi mishahara na posho mbalimbali kwa wakati kila mwezi.<br><br>(ii) Kuwapatia Wanajeshi wote posho ya ushuru (duty free allowance) ambayo inawezesha kila Mwanajeshi kunufaika badala ya wale waliopo katika maeneo ya mijini kwenye maduka hayo.<br><br>(iii) Mpango bora zaidi wa tiba kwa wanajeshi wote na familia zao unaandaliwa. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (iv) Kukamilisha ujenzi wa nyumba 6,064 zikiwa na huduma za maji na umeme kwa ajili ya makazi ya Wanajeshi katika vikosi vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Pemba, Kigoma na Kagera. Nyumba hizo tayari zinatumika. |
| 146 (iii) | Kuendelea kuweka mazingira mazuri yanayoliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha Mafunzo kwa vijana Wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa mujibu wa Sheria. | (i) Katika mwaka 2016/17, jumla ya vijana 24,596 walipatiwa mafunzo katika Kambi mbalimbali hapa nchini. Kati yao, vijana 14,748 ni wa mujibu wa sheria na vijana 9,848 ni wa kujitolea.<br><br>(ii) Katika mwaka 2016/17, Serikali lilikarabati na kufungua Kambi mpya tano (5) za Milundikwa na Luwa zilizopo katika Mkoa wa Rukwa; Itaka Mkoani Songwe; Mpwapwa Mkoani Dodoma; na Makuyuni Mkoani Arusha.<br><br>(iii) Katika Mwaka 2017, mafunzo yalitolewa kwa maafisa vijana 66 wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuwajengea maadili mema, ukakamavu na moyo wa uzalendo kwa nchi yao. |
| 146(iv) | Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika kupeleka askari wetu kushiriki majukumu ya Ulinzi wa Amani kwenye Nchi mbalimbali duniani ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za Kisasa za Ulinzi wa Amani. | (i) Jeshi limeendelea kushiriki katika shughuli za ulinzi wa amani Barani Afrika katika Jimbo la Darfur nchini Sudani, Sudani ya Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Aidha, JWTZ limetuma kikosi kwa ajili ya Kulinda Amani katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (Central African Republic –CAR).<br><br>(ii) JWTZ limeendelea kushiriki katika shughuli za ulinzi wa amani nchini Lebanon. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (iii) Jeshi limeendelea kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki kwa kufanya mazoezi mbalimbali ya ushirikiano ikiwemo Zoezi Ushirikiano Imara – 2016 (Kenya) na “Command Post Exercise Utulivu Africa II- 2017” (Rwanda) katika mpango wa African Capacity for Immediate Response to Crises. Aidha, JWTZ lilishiriki Michezo ya Majeshi kwa mwaka 2017 ambayo yalifanyika nchini Burundi katika kuendeleza ushirikiano wa majeshi.<br><br>(iv) JWTZ limeendelea kushirikiana na nchi za SADC kwa kufanya mazoezi ya pamoja. Katika mwaka 2017 JWTZ lilikuwa mwenyeji wa Zoezi Matumbawe 2017 yaliyofanyikia mkoani Tanga. Zoezi hilol a “SADC Special Forces” limeongeza uwezo wa Jeshi katika kupambana na wahalifu wa ndani ya nchi na wahalifu wa kimataifa.<br><br>(v) Jeshi linashirikiana na nchi za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Australia, Bangladesh, China, Hispania, India, Iran, Italia, Pakistan, Sierra Leone, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Urusi kuzuia matishio ya utekaji meli katika Bahari ya Hindi. |

## 2.16 Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki




*Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwa katika kikao cha 17 kilichofanyika Jijini Arusha tarehe 2 Machi 2017.*

Serikali inaimarisha uhusiano mzuri baina ya nchi yetu na nchi nyingine duniani ili kuimarisha na kukuza diplomasia ya uchumi. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.17.

Bangokitita Na. 17: Mafanikio Katika Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 149(a) | Kuendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda na kuendeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuzingatia maslahi muhimu ya nchi yetu ili kunufaisha Watanzania wote. | (i) Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ili kuendana na mahitaji ya sasa ya Tanzania kwenye Jumuiya mbalimbali za Kikanda. Hatua za awali za mapitio ya Sera hiyo zimeanza kufanyika na taarifa ya kwanza ya tathmini ya Sera imeshaandaliwa.<br><br>(ii) Serikali inazishawishi Taasisi Binafsi na mashirika makubwa kuendeleza kuisaidia Tanzania kwenye maeneo |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | ya afya, elimu, maji, utalii na maeneo mengine muhimu. Aidha, Serikali imeratibu mazungumzo ya upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu kati ya Tanzania na Poland na kufanikisha mkopo wa Dola za Marekani milioni 110 ambazo zitatumika kuanzisha kiwanda cha kuunganisha matrekta nchini. |
| 149(e) | Kuendelea kupigania Diplomasia ya Uchumi na Siasa. | Serikali imeratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa, (United Nations Development Assistance Programme – UNDP II) unaotekelezwa kuanzia Julai 2016 hadi Juni, 2021. Kupitia mpango huo, Tanzania itanufaika na miradi yenye thamani ya **Dola za Marekani bilioni 1.3** ambapo asilimia 8 ya fedha hizo zinatumika kwa miradi ya Zanzibar. |
| 150(c) | Kuendelea na utekelezaji wa hatua za awali za mtangamano wa Afrika Mashariki za Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja ili kuhakikisha Watanzania wanaendelea kunufaika na fursa za kibiashara, uwekezaji na ajira zitokanazo na utekelezaji wa hatua hizo. | (i) Serikali imeratibu ukusanyaji na usambazaji wa taarifa stahiki zilizosaidia Serikali ya Uganda kuamua kupitisha Bomba la Mafuta kutoka Hoima hadi Bandari ya Tanga. Aidha, Serikali inaratibu ushiriki wa Tanzania katika vikao vya majadiliano vya Wataalamu wa nchi za Tanzania na Uganda na wale wa Kampuni ya TOTAL kuhusu utekelezaji wa mradi huo.<br><br>(ii) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) Serikali inaratibu maandalizi ya majukwaa ya kibiashara na uwekezaji kama moja ya njia za kufungua fursa za kiuchumi kwa wafanyabiashara wa Kitanzania na kuimarisha mahusiano ya kibiashara na kuvutia uwekezaji nchini husasan katika sekta ya viwanda. |

## 2.17 Kuhamia Makao Makuu Dodoma



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, akiwa katika picha pamoja na wazee wa mkoa Dodoma wakati alipohamia rasmi Makao Makuu tarehe 30 Septemba 2016.*




*Aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Angellah Kairuki (wa pili kushoto), akizindua awamu ya kwanza ya ofisi yake kuhamia Dodoma, Januari 2017.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, tarehe 23 Julai, 2016 alitangaza uamuzi wa kuhamisha shughuli za Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.18.

Bangokitita Na. 18: Mafanikio Katika Kutekeleza Mpango wa Serikali Kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **151 (a)** | Kutunga Sheria itakayoutambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. | Mapendekezo ya kutunga Sheria mpya itakayoutambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi yameandaliwa. |
| **151(b)** | Kusimamia azma ya Serikali ya kuhakikisha majengo yote ya Wizara za Serikali yanajengwa Dodoma badala ya Dar es salaam. | Kufuatia uamuzi uliofanywa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 23 Julai, 2016 kuwa shughuli za Serikali zinahamishwa kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, majengo yote ya Serikali sasa yatajengwa Dodoma. Eneo lenye ukubwa wa **ekari 700** limepatikana Ihumwa, Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 200** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo mapya ya Serikali Dodoma. Hadi sasa, jumla ya **Watumishi 2,069** wamehamishiwa Dodoma wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Watumishi wengine **wapatao 5,136** watahamia katika mwaka wa fedha 2017/ 2018. |
| 151 (C) | Kuongeza kasi ya kupima viwanja kwa ajili ya Makazi, Viwanda na Taasisi na kuendelea kuboresha miundombinu ikiwemo maji umeme na barabara**.** | Baada ya kuvunjwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA), shughuli za upimaji wa viwanja zinafanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kwa kushirikiana Wizara ya Ardhi Nyumba Maendeleo ya Makazi kwa kasi zaidi na pia kuishirikisha Sekta Binafsi. |

## 2.18 *Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Majanga*

Majanga ni matukio yanayojitokeza na yenye uwezo mkubwa wa kuleta maafa yanayohatarisha maisha ya watu na mali zao, miundombinu na huduma mbalimbali za jamii. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.19.

Bangokitita Na. 19: Mafanikio Katika Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Majanga

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **153(a)** | Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria mpya ya kukabliana na maafa katika ngazi zote kuanzia Taifa hadi Vijijini. | Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na.7 ya Mwaka 2015 zimeandaliwa, kusainiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Vilevile, Mwongozo wa Utekelezaji wa Sheria Na.7 ya mwaka 2015, uliandaliwa. |
| **153(b)** | Kujenga kituo cha menejimenti ya maafa na mawasiliano ili kuongeza uwezo wa nchi katika kukabiliana na maafa. | Maandalizi ya awali ya eneo la ujenzi wa Kituo cha Menejimenti ya Maafa na Mawasiliano nchini kitakachojengwa Dodoma yanaendelea. |

## *2.19 Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) ramani inayoonyesha kiwango cha maambukizo ya ugonjwa wa UKIMWI ambayo yameainishwa kwenye taarifa mpya ya Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania (THIS 2016) wakati wa Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani ambayo Kitaifa yamefanyika Jijini Dar es Salaam, tarehe 1/12/2017.*

Serikali inatekeleza Mkakati wa kupunguza maambukizi ya UKIMWI katika jamiii yetu na kuimarisha huduma za elimu ya kujikinga na UKIMWI pamoja na kuanzisha Mfuko maalum wa UKIMWI kwa lengo la kupata rasilimali za kutosha. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.20.

Bangokitita Na. 20: Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **154(a)** | Kupunguza au kuondokana kabisa na utegemezi wa wafadhili kwa kuanzisha Mfuko maalumu wa UKIMWI (AIDS TRUST FUND) ukiwa na lengo la kuongeza rasilimali kwa ajili ya kuboresha huduma za UKIMWI zinazotolewa. | Mfuko Maalumu wa UKIMWI (AIDS TRUST FUND) ulianzishwa rasmi katika mwaka wa fedha 2015/16 na Serikali imekwishachangia **Shilingi bilioni 1.32** kutoka kwenye bajeti yake. Aidha, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi billioni 3** katika mwaka wa fedha 2017/18 kwa ajili ya Mfuko huo. Vilevile, Serikali imekusanya jumla ya **Shilingi 345,750,000** kupitia harambee mbalimbali. |
| **154(b)** | Kufanya jitihada za kupunguza kasi ya maambukizi katika jamiii kutoka 5.1% mwaka 2015 hadi 3% ifikapo 2020 | Makisio ya kimahesabu ya kukadiria kiwango cha maambukizi ya UKIMWI nchini yanaonesha kuwa idadi ya watu wanaopata maambukizi mapya ya UKIMWI imepungua kutoka asilimia 0.32 mwaka 2013 hadi asilimia 0.22 mwaka 2017. |
| **154(c)** | Kuimarisha huduma za elimu ya UKIMWI kwa njia ya mawasiliano baina ya watu mashuhuri, program za mahali pa kazi na viongozi wa dini. | Serikali imeendelea kuwezesha sekta mbalimbali kifedha na kitaalamu katika kupanga na kutekeleza afua za kudhibiti UKIMWI mahala pa kazi. Wizara, Wakala na Taasisi za Serikali 23 zimeandaa mikakati ya kudhibiti UKIMWI na kutengeneza mipango ya utekelezaji inayotokana na Mikakati hiyo. |
| **154(d)** | Kuongeza usambazaji wa taarifa zinazohusu kubadili tabia hatarishi na upatikanaji | Mwongozo wa kitaifa wa mawasiliano ya mabadiliko ya tabia umesambazwa kwa wadau kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | wa huduma bora kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kupitia vyombo vya Habari. | wa afua za kinga dhidi ya VVU miongoni mwa makundi ya vijana. Aidha, Kampeni kupitia kwenye redio za kitaifa na kijamii zinaendelea kufanyika ili kuelimisha vijana kujikinga na UKIMWI. Vilevile, Serikali imejenga vituo tisa (9) vya maarifa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Songwe, Mbeya, Iringa na Singida. |
| **154(e**) | Kuendeleza tafiti za UKIMWI na kutathimini vipaumbele kwa ajili ya kufanya maamuzi na kuandaa program za UKIMWI. | Katika mwaka 2016/2017, Serikali ilianzisha utafiti wa kubainisha viwango vya maambukizi ya UKIMWI. Utafiti huo utaiwezesha Serikali kujua ukubwa wa maambukizo, ufahamu wa jamii kuhusu kinga, tiba na vichocheo vya maambukizi kwa kila Mkoa Tanzania Bara na Zanzibar. |

## 2.20 Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya



*Waziri Mkuu Mhe.Kassim Majaliwa akizungumza na Mawaziri na Wajumbe wa Baraza la Taifa la Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nchini wakati akifungua kikao cha Baraza hilo Jijini Dar es Salaam.*

Madhara ya matumizi ya dawa za kulevya ni makubwa hususan kwa vijana kwani yana madhara kwa nguvu kazi ya taifa. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.21.

Bangokitita Na. 21: **Mapambano Dhidi ya** Dawa za Kulevya

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **155(a)** | Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeanzishwa rasmi Februari, 2017 na inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake. |
| **155(b)** | Kuongeza utoaji wa dawa na matibabu pamoja na kuanzisha vituo vya kuhudumia wananchi walioathirika na matumizi ya | Idadi ya vituo vinavyotoa huduma za matibabu imeongezeka kutoka vituo vitatu (3) hadi vituo vinne (4). Vituo Vitatu (3) vipo jijini Dar es Salaam na kituo kimoja |

| | | |
|---|---|---|
| | dawa za kulevya. | (1) kimeanzishwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya. Aidha, Serikali inasimamia uanzishwaji wa Nyumba za upataji nafuu (sober houses) ambazo hadi sasa idadi yake ni 22. |
| **155 (c)** | Kushirikiana na asasi za kijamii na kuziwezesha ili kuinua uwezo wa kushiriki katika kutoa elimu juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii zinazowazunguka. | Serikali imefanya tathmini ya Asasi 36 zilizopo katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa lengo la kufahamu mahitaji yake na ziweze kusaidiwa. |
| **155(d)** | Kusimamia kwa ukamilifu Sheria Mpya ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya. | Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 (kama ilivyorekebisha 2017) imeendelea kutumika na imefanikisha ukamataji wa watuhumiwa na uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya nchini. |

## *2.21 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo*




*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akionyesha Kamusi Kuu ya Kiswahili baada ya kuizindua kwenye ukumbi wa Bunge mjini Dodoma.*




*Mwanariadha wa Tanzania, Alphonce Simbu akimaliza mbio za Marathon Mumbai Januari 2017 ambako alishimda medali ya dhahabu.*

Serikali imeboresha mazingira ya uhuru wa vyombo vya habari na kuendeleza sekta ya utamaduni na michezo. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.21.

Bangokitita Na. 21: Mafanikio Katika Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **157(a)** | Kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa kwa urahisi na kwa wakati kwa mujibu wa Sheria. | (i) Jumla ya habari 864 na makala 540 zimechapishwa katika magazeti mbalimbali ya Serikali na Kampuni binafsi. Kipindi maalumu cha "TUNATEKELEZA" kinachorushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kila Jumatatu saa 1:00 usiku hadi saa 2:00 usiku, na Alhamisi saa 3:30 usiku hadi saa 4:30 usiku kinatoa fursa kwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali kuelezea na kutoa ufafanuzi kwa Umma kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya maendeleo.<br><br>(ii) Serikali imeanzisha Maelezo TV; Blog ya Maelezo pamoja na Blog ya Magazeti ya Serikali (TSN) na kuziunganisha na mitandao ya kijamii kama vile facebook, twitter na instagram ili kupitia mitandao hii kutoa habari kwa Wananchi kuhusu utendaji wa Serikali. |
| **157(b)** | Kuharakisha mchakato wa kupitisha na kuanza kutekeleza Sheria kuhusu uhuru wa Wananchi kupata habari na uhuru wa Vyombo vya Habari kupata na kutoa habari. | Muswada wa Huduma ya Habari Na 12 ya mwaka 2016 ulipitishwa na Bunge tarehe 16 Novemba, 2016 na kuwa Sheria. Aidha, Kanuni zimeandaliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Toleo Na. 18 la tarehe 3 Februari, 2017. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, vyombo vyote vya Habari vikiwemo Magazeti na Majarida vinatakiwa kujisajili upya ambapo hadi kufika Septemba, 2017 magazeti 18 yalikuwa yamesajiliwa. |
| **157(c)** | Kuhakikisha kwamba matangazo ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) | Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) limeunganishwa na Mkongo wa Taifa na hivyo kurahisisha utumaji wa habari kwenda |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | yanasikika nchini kote kwa kulipatia uwezo wa rasilimali watu, fedha na vifaa vya kisasa. | sehemu mbalimbali. Aidha, Mradi wa Upanuzi wa usikivu wa Redio katika Wilaya/maeneo ya mipakani mwa nchi unatarajiwa kukamilika hivi karibuni. Vilevile, utekelezaji wa awamu mbili za Mradi wa kufunga vifaa vipya vya mtambo wa kurushia matangazo ya redio na televisheni kwa njia ya satelaiti (satellite up-link) umeanza na unatarajia kukamilika mwisho wa mwaka 2017. |
| **157(d)** | Kuimarisha uwezo wa Idara ya Habari (Maelezo) kama Msemaji Mkuu wa Serikali. | Serikali imeimarisha Idara ya Habari-Maelezo kwa kuipatia vifaa mbalimbali. |
| **159(a)** | Kuhakikisha lugha ya Kiswahili inaendelezwa ndani na nje ya nchi na kutumika kama bidhaa ya soko na chanzo cha ajira kwa wataalamu na wapenzi wa Kiswahili. Aidha, kupanua wigo wa misamiati na istilahi za lugha ya Kiswahili kwa kufanya utafiti wa Lugha za Kijamii. | (i) Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limetoa huduma za tafsiri kwa Asasi za Serikali, Mashirika ya Umma na ya binafsi, na imetoa pia huduma ya ukalimani katika mikutano ya Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika iliyofanyika mwezi Julai, 2016 Kigali-Rwanda na mwezi Januari, 2017 Addis Ababa Ethiopia pamoja na mkutano wa Bunge la Afrika uliofanyika Sharm el Sheikh – Misri, mwezi Oktoba 2016.<br><br>(ii) Serikali imekamilisha maandalizi ya mafunzo ya Kiswahili kwa wageni, miswada mitano ya Kamusi ndogo ya lugha tatu kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki na Afrika pamoja na maneno ya Kiswahili milioni moja na nusu kwa ajili ya Kanzi Kuu ya Kiswahili. Lengo ni kukifanya Kiswahili kuwa bidhaa. |
| **159(c)** | Kusimamia Utekelezaji wa Sheria zinazohusu shughuli | (i) Serikali imehakiki na kutolea vibali *(Certificates of Approval)* kazi |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | za Filamu, Michezo ya Kuigiza, Muziki, Ubunifu kwa lengo la kulinda haki na Maslahi ya Makundi hayo. | mbalimbali za sanaa ambapo jumla ya kazi za picha jongevu 2,797 zilifanyiwa kazi zikijumuisha filamu 2,568 za kitanzania na filamu 229 kutoka nje ya nchi;<br>(ii) Serikali imepitia na kutoa vibali vya utengenezaji filamu 445 pamoja na kufanya operesheni kubwa mbili za kazi za filamu zinazoingia sokoni bila kufuata utaratibu ambapo hadi kufikia Machi 2017, jumla ya kazi 2,394,059 zilikamatwa zikiwemo kazi za nje ya nchi 2,393,529 zenye thamani ya zaidi ya Shilingi 3,590,293,500 na za ndani 530 zenye thamani ya Shilingi 1,590,000. |
| **161(a)** | Kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo nchini. | Serikali imewezesha kukamilishwa kwa ukarabati wa Uwanja wa Uhuru na kukabidhiwa tarehe 22 Agosti, 2016. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kama FIFA na TFF inaendelea kuboresha viwanja vya michezo vya Kaitaba Mkoani Kagera na Nyamagana Mkoani Mwanza;<br><br>Serikali imeanza ujenzi wa eneo changamani la michezo Mkoani Dodoma ambapo Serikali imetenga Shilingi Bilioni 1.82 katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya mradi huo unaotekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Morocco. |
| **163(k)** | Kuhifadhi kumbukumbu ya ushiriki na mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika | (i) Serikali imefanya majadiliano na Serikali ya Afrika ya Kusini na kufikia makubaliano ya kusaini *Communique* ya utekelezaji wa Programu ya |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kwa kuendeleza utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi. | Ukombozi wa Bara la Afrika. Makubaliano hayo ni kwa ajili ya kutambua, kuhifadhi na kuendeleza Urithi wa Ukombozi na Utamaduni wa bara la Afrika.<br><br>(ii) Serikali imebainisha na kuhifadhi kumbumbuku mbalimbali za harakati za ukombozi kwa kutembelea maeneo yote ya urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na kupata kumbukumbu zikiwemo picha zipatazo 2,000. |

## *2.22 Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, akizundua rasmi Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya mwaka 2017 na Mkakati wa Utekelezaji wake mjini Dodoma.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua huduma ya TTCL Pesa Jijini Dar es Salaam.*

Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wananchi Kiuchumi kwa kuanzisha na kuendesha program za kukabiliana na changamoto za umaskini kwa wananchi. Maelezo ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.22.

Bangokitita Na. 22: Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **57(a)** | Kuhakikisha kuwa shughuli zote zenye mwelekeo wa ushirika zinapewa msukumo stahiki kwa kuhamasisha na kusimamia kwa nguvu uanzishaji wa vikundi vya ushirika kama vile SACCOS na VICOBA; Vyama vya Mazao, Ufugaji na Uvuvi hasa ikizingatiwa kuwa ushirika ndiyo silaha kuu ya wanyonge na nguzo kuu ya ujenzi wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. | Uhamasishaji kuhusu uanzishwaji na uendelezaji wa vyama vya ushirika umefanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Hadi kufikia Juni 2017, Vyama vya Ushirika vimeongezeka kufikia 10,596 zikiwemo SACCOs 5,640. Vyama hivyo vimesajiliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na vina jumla ya wanachama 1,312,145. Kati ya hao wanawake ni 407,772 na wanaume ni 904,373. Vyama hivyo kwa ujumla vina hisa zenye thamani ya Shilingi 52,948,735,020. |
| **57(b)** | Kuweka mfumo wa kuvitambua, kuvisajili na kuviwezesha vikundi vyote vyenye mwelekeo wa ushirika na ujasiriamali. | Mwongozo wa Kusajili na Kuandaa Taarifa za Vikundi vya kifedha vya kijamii umeandaliwa. Mwongozo huo unaelekeza jinsi ya kusajili, kufuatilia na kutoa taarifa za maendeleo ya vikundi vya kifedha katika ngazi husika. Aidha, waratibu wa uwezeshaji katika mikoa na halmashauri, wamejengewa uwezo kutambua wajibu wao katika kusimamia, kuhamasisha, kufuatilia na kutoa taarifa za maendeleo ya vikundi hivyo. |
| **57( c )** | Kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuhakikisha kwamba fursa ya mikopo kwa ajili ya mitaji inapatikana bila ya urasimu na kwa masharti nafuu na kuwafikia wananchi wengi mijini na vijijini. | Hadi kufikia Aprili 2017, Serikali kupitia mifuko ya MEF, NEDF, CAF, AGITF, YDF, WDF, SME-CGS, ECGS, SELF MF, UTT Microfinance Fund, KKCF na PTF iliwezesha watanzania zaidi ya 750,500 kupata mikopo yenye thamani ya **Shilingi trilioni1.4.** |
| **57(e)(i)** | Kusaidia wafanyabiashara wadogo kwa kutenga maeneo mahsusi katika kila Halmashauri kwa ajili ya | Hadi kufikia Juni 2017, mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ilikuwa imetenga maeneo maalumu ya uwekezaji katika Halmashauri zao. Viongozi wa Mikoa na Halmashauri |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | biashara ndogo ndogo. | nchini wanaboresha maeneo hayo kwa kuyapima na kuyawekea miundombinu muhimu. |
| **57(e)(ii)** | Kusaidia kwa kuondoa kero na malalamiko kuhusu ushuru na kodi zinazotozwa na Halmashauri ambazo zinakwamisha jitihada za wafanyabiashara wadogo kujikwamua kimaisha. | Katika bajeti ya Mwaka 2017/2018, jumla ya tozo 92 ambazo zilikuwa kero kwa makundi mbalimbali ya wazalishaji na wafanyabiashara zimefutwa. Kati ya tozo hizo, tozo 80 ni kwa wakulima, tozo saba (7) kwa wafugaji na tozo 5 kwa wavuvi. |
| **57(e) (vi)** | Kusaidia wafanyabiashara wadogo kwa kuweka utaratibu utakaozitaka Halmashauri kutenga asilimia 30 ya thamani ya manunuzi yake kwa ajili ya biashara, kampuni au vikundi vinavyomilikiwa na vijana/wanawake. | Sheria ya Ununuzi wa umma ya mwaka 2013 imefanyiwa mapitio mwaka 2016 ili kuhakikisha kuwa asilmia 30 ya ununuzi wa Serikali unafanywa na Makundi Maalumu (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu). Serikali inaandaa mwongozo wa utekelezaji wa Sheria hii hususan kwenye eneo la asilimia 30 ya ununuzi kwenye makundi maalumu. |
| **60(a)** | Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga, kurasimisha, kupima na kuyawekea miundombinu maeneo maalumu ya vijana kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo, ufugaji, madini, viwanda vidogo, uvuvi, mawasiliano na biashara. | Halmashauri 81 zimetenga jumla ya kilomita za mraba zipatazo 2,438 kama maeneo maalumu ya uwekezaji ili kuwezesha wananchi pamoja na wawekezaji wengine kufanya shughuli za uwekezaji. Maeneo haya yamewawezesha vijana na jamii kwa ujumla kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuinua vipato vyao. |
| **60(b)** | Kuziwezesha SACCOS za vijana katika Halmashauri zote nchini kupata mikopo kutoka kwenye benki na taasisi nyingine za fedha. | Serikali imetoa dhamana za mikopo kwa SACCOS za Halmashauri katika Mikoa ya Iringa, Kigoma, Tanga, Ruvuma na Kagera. Mfuko huo umedhamini mikopo yenye thamani ya **Shilingi Milioni 457.9** na Geita, Mwanza, Simiyu, Lindi na Mtwara. |
| **60(i)** | Kuhakikisha kwamba | Katika Mwaka 2016/17, Halmashauri |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Halmashauri zote nchini zinatenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu. | zilitenga **Shilingi bilioni 28.4** kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo hadi Juni, 2017 **Shilingi bilioni 8** zilikopeshwa kwenye vikundi 6,076 vya vijana vyenye wanachama 30,380. |
| **63(a)** | Kuendelea kuwapatia vijana mikopo yenye masharti nafuu, elimu ya ujasiriamali na biashara ili kuwawezesha kuongeza ajira, ujuzi wa kujiajiri, fursa za kipato na kujikimu. | Mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 2.1** imetolewa katika mikoa 10 ambayo ni Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Dodoma, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Kigoma, Tabora na Kagera. Utoaji wa mikopo hii ulitanguliwa na elimu ya ujasiriamali na biashara. |
| **63(b)** | Kuwahamasisha kuanziha na kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali, vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS na VICOBA) na kuwawezesha kimtaji ili kupanua shughuli zao za uzalishaji mali. | Uhamishaji kwa wananchi kujiunga katika vikundi vya kiuchumi na ujasiriamali umefanywa katika miko ya Tanga, Geita, Simiyu, Mwanza Pwani, Dar es Salaam, Dodoma, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Kigoma, Tabora na kagera. Aidha, Serikali imetoa dhaman za mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.1 kwa vikundi 113 katika mikoa iliyohamasishwa. |
| **63(d)** | Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu. | Hadi kufikia Juni 2017, watu 22,409 kutoka Halmashauri 81 walinufaika na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Kati ya wanafaaka hao, wanufaika 14,825 ni wanawake 7,584 ni wanaume. Jumla ya **Shilingi bilioni 2,505,891,000** zilitolewa katika kipindi hicho. |

## *2.25 Kuendeleza Makundi Maalumu*

Hatua zimeendelea kuchukuliwa na Serikali kwa kutunga Sera, Sheria na Programu mbalimbali zenye lengo la kuongeza fursa za kiuchumi kwa makundi maalum. Maelezo

ya kina juu ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yanavyobainishwa katika Bangokitita Na.23.

Bangokitita Na. 23: Kuendeleza Makundi Maalumu

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **2.25.1 KUWEZESHA VIJANA KUJIAJIRI** | | |
| 60(d) | Kuwawezesha vijana wanaohitimu Elimu ya Juu na Vyuo vya Ufundi kuunda makampuni kulingana na fani zao kwa lengo la kuwapatia mitaji na nyenzo kupitia taasisi za fedha na mifuko mingine ya uwezeshaji. | (i) Serikali katika Mwaka 2016/2017, imetekeleza Program ya Kukuza Ujuzi ambapo jumla ya **vijana 11,340** (wakiwemo wa elimu ya juu) wamepewa mafunzo ya stadi za kazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa wana ujuzi wa kuajirika au kujiajiri.<br>(ii) Katika mwaka 2017/2018, **Shilingi 1,075,000,000/=** zimetengwa kwa ajili ya kutoa nyenzo za kazi kwa vijana walio katika vikundi kupitia programu ya kukuza ujuzi. |
| 60(e) | Kuhamasisha na kuweka mazingira yatakayowezesha Vijana Wajasiriamali wadogo kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuweza kupata mikopo na kunufaika na mafao mengineyo yatolewayo na Mifuko hiyo. | Mifuko ya GEPF, NSSF, PPF, LAPF na PSPF imeanzisha utaratibu maalum wa kuandikisha wanachama kutoka sekta isiyo rasmi ili waweze kunufaika na mafao yatolewayo na mifuko hiyo. Wanachama hao ni pamoja na vijana waendesha boda boda, wafanyabiashara wadogo, Mama Lishe na Wanamuziki. |
| 60(h) | Kuwawezesha Vijana wanaohitimu Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati kufanya kazi kwa kujitolea katika asasi mbalimbali kwa lengo la kuwapatia uzoefu na maadili ya kazi ili waweze kuajiriwa au kujiajiri wenyewe. | Serikali imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo kwa Vitendo Kazini kwa Wahitimu wa Vyuo Vikuu (National Internship Guidelines). Mwongozo huo unaweka namna bora ya kuandaa, kutekeleza, kusimamia na kuratibu programu za mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu kwa kushirikiana na waajiri. Mwongozo huo umeanza kutumika rasmi tarehe 16.09.2017. Katika mwaka 2017/18, Serikali kupitia |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | progamu ya kukuza ujuzi nchini, imetenga jumla ya **Shilingi 7,237,000,000** kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo kazini kwa **wahitimu 4,000** kwa kushirikiana na waajiri.<br><br>Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya Uanagenzi kwa vijana 140 yanaendelea.<br><br>Vijana 5,000 wanaendela na mafunzo ya kurasimisha Ujuzi uliopatikana wa Mfumo usio rasmi.<br><br>Vijana 60 wamepata mafunzo katika Sekta ya ngozi kupitia mfumo wa mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu. |
| ***2.25.2 Watu Wenye Ulemavu*** | | |
| 166(a) | Watu Wenye Ulemavu wote nchini wanaendelea kutambuliwa na kulindwa na vitendo vinavyoshusha utu vikiwemo ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu. | (i) Serikali inahakikisha kuwa watumiaji wa lugha ya alama wanapata haki yao ya kikatiba ya kupata habari kwa kuviagiza vyombo vya habari nchini kutumia wakalimani wa lugha ya alama ikiwa ni takwa la Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na. 9 ya 2010;<br><br>(ii) Serikali imezindua Baraza la Watu wenye Ulemavu na Baraza hilo linatekeleza majukumu yake ipasavyo kama ilivyoainishwa katika sheria;<br><br>(iii) Serikali imeanza utekelezaji wa mkakati wa kutengeneza vifaa saidizi nchini kwa kupitia SIDO na wadau wengine;<br><br>(iv) Serikali inatoa Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Watu Wenye Ulemavu nchini ili kutoa fursa kwa watu wengi wenye |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | ulemavu kupata ujuzi na stadi za ufundi zitakazowawezesha kujiajiri wao wenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa; na<br><br>(v) Serikali inawaunganisha Wadau wa Kitaifa na Kimataifa katika kushughulikia masuala yanayohusu haki, usawa na usalama kwa watu wenye ualbino nchini. |
| 166(b) | Kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu wa ngozi wanalindwa dhidi ya ukatili na ubaguzi wa aina yoyote. | Rasimu ya Mkakakati wa Kuwalinda Watu Wenye Ualbino dhidi ya Ukatili na Mauaji imeandaliwa na kampeni ya kupinga unyanyapaa na ukatili dhidi ya Watu Wenye Ualbino katika mikoa sita ya Kanda ya Ziwa imezinduliwa. |
| 166(c) | Kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapata elimu kwa kutumia vifaa maalum na kushiriki katika nafasi za uwakilishi na shughuli za kijamii. | (i) Mwaka 2016/2017, Serikali ilisambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule za Watoto wenye Ulemavu nchini, vifaa hivyo ni pamoja na mashine **932** za kuandikia maandishi ya nukta nundu; wasioona **1,495** walipatiwa kivunge chenye vifaa vya kujifunzia kwa (kila kivunge kina fimbo nyeupe, kibao na kalamu zake, futi kamba ya vipimo na vifaa vya kufanya hisabati); shime sikio **1,100**; rimu **2,548** za karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu; pamoja na rimu **1,100** za karatasi za kudurufu maandishi ya nukta nundu.<br><br>(ii) Serikali imeondoa kodi kwa nyenzo zote za kujimudu kwa Watu Wenye Ulemavu zinazotengenezwa ndani na nje ya nchi. |
| 166(f) | Kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata ajira na kufanya kazi. | (i) Serikali imetoa maelekezo kwa Serikali za Mitaa kutenga maeneo maalum kwa Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (ii) Watu wenye Ulemavu hususan vijana wanapatiwa fursa sawa na Vijana wengine katika kujiunga na mafunzo ya kukuza ujuzi kupitia Program ya miaka mitano (5) ya kukuza ujuzi kwa makundi mbalimbali ya wafanyakazi walioajiriwa na waliojiajiri. |
| **2.25.3 Wafanyakazi** | | |
| 174(c) | Kuboresha na kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wakiwa sehemu ya kazi. | a) Serikali imefanya yafuatayo:<br>(i) Kaguzi 25,750 za kawaida, Kaguzi maalum 16,010 na Upimaji Afya Wafanyakazi 76,587 zilifanyika.<br>(ii) Sehemu za Kazi 11,253 zilisajiliwa na Sehemu 524 zilipewa leseni za kukidhi vigezo vya Usalama na Afya;<br>(iii) Wafanyakazi 27,518 walipewa mafunzo ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi;<br>(iv) Kanuni ya Mazingira ya kufanyia kazi ziliandaliwa na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji katika maeneo yao ya kazi;<br>(v) Wajasiriamali wadogo wapatao 2,887 walipewa mafunzo ya Afya na Usalama mahali pa Kazi katika mikoa ya Tabora, Ruvuma, Dodoma, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mwanza, Singida, Mbeya, Mtwara, Shinyanga na Geita; na |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | (vi) Mishahara na stahili za kiutumishi kwa Wafanyakazi wote imelipwa kulingana na taratibu za kiutumishi na kiutawala. |
| 174(d) | Kuridhia Mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) yenye maslahi kwa wafanyakazi. | Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Saba uliofanyika kuanzia tarehe 4 April hadi 5 Julai, 2017 liliridhia Mkataba wa Kimataifa wa ILO wa Kazi za Ubaharia wa Mwaka 2006 (Labour Maritime Convention, 2006) na Mkataba wa Kimataifa wa ILO wa Vitambulisho vya Mabaharia Na.185 wa Mwaka 2003 (Seafarers' Identity Documents (Revised) Convention No. 185 of 2003). |
| **2.25.4 Kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii** | | |
| 174(i) | Kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuimarisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili iendelee kutoa huduma bora na endelevu kwa wanachama wao. | Mpango wa kuimarisha na kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii ikiwa ni pamoja na (i) kuunganisha mifuko iliyopo, (ii) kutoa fao mbadala la "Upotevu wa Ajira"(iii) na kuanzisha mpango wa Pensheni kwa Wazee umekamilika. |
| 174(ii) | Kuhamasisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuanzisha mfuko mkubwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi na wajasiriamali wadogo kwa masharti nafuu. | Utaratibu wa Kisheria umeandaliwa ambapo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii itatoa mikopo kwa Wafanyakazi na Wajasiriamali wadogo wadogo kwa masharti nafuu kupitia SACCOS za wanachama. |

# SURA YA TATU

## *3.0 Matarajio*

Sura ya Pili ya Taarifa hii, imebainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha takriban miaka miwili ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho kifupi, wananchi wana matajario makubwa kwa Serikali yao. Uchumi unatarajiwa kukua kwa kasi zaidi kutokana na kuimarishwa kwa miundombinu ya usafirishaji wa barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege pamoja na kuwekwa kwa misingi imara na mazingira bora ya uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini na kutoa ajira kwa watanzania wengi.

Katika kipindi kilichobakia, Serikali itaendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge),* kukamilisha uletaji wa ndege za ATCL zilizoagizwa, kukamilisha ujenzi wa jengo la tatu (3) la abiria, katika uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam, ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na kuboresha mfumo wa uondoshaji mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam. Vilevile, ujenzi wa meli katika ziwa Victoria na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mwanza, Kigoma, Sumbawanga na Shinyanga utafanyika. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo muhimu na kuimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi kutaiwezesha nchi yetu kutumia kikamilifu nafasi yake ya kijiografia kukuza uchumi.

Usimamiaji makini wa Rasilimali za Taifa zikiwemo utalii na maliasili, madini, mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2017 unatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya madini kwa kiasi kikubwa.

Benki ya Kilimo inatarajia kukua zaidi kwa kuongezewa mtaji na hivyo kuwawezesha wakulima kupata mikopo ili kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara yenye ubora unaotakiwa kukidhi masoko ya Ndani na Nje. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali itafufua mazao matano makuu ya biashara ya Pamba, Kahawa, Tumbaku, Korosho na Chai ili kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa na tija, kinachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kipato cha wakulima na kinachochea ukuaji wa uchumi wa Viwanda na kuongeza fursa za ajira. Pamoja na kuongeza upatikanaji wa fedha za kilimo kupitia Benki ya Kilimo, Serikali itaimarisha upatikanaji wa pembejeo muhimu za kilimo, kuimarisha miundombinu ya masoko ya kilimo, kuongeza maafisa ugani na kuhakikisha

wanasimamia wakulima Vijijini. Serikali pia, itaimarisha tafiti katika Sekta ya Kilimo kwa kutumia Vyuo vyake vya Kilimo.

Huduma za Mawasiliano nchini zitaendela kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kuunganisha Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya/Polisi (OCD), Hospitali zote za Wilaya, Vyuo Vikuu vyote na Vituo vya Posta katika mtandao wa pamoja ili kuboresha huduma mtandao (e-services). Vilevile, huduma za mawasiliano zitafikishwa katika **kata 274** zenye Vijiji zaidi ya 800. Kuongezeka kwa ushindani, katika Sekta ya Mawasiliano na kufikishwa kwa huduma hizo muhimu kutawezesha kushuka kwa gharama za huduma za Mawasiliano na hivyo, kuwawezesha wananchi kupata habari zikiwemo taarifa za masoko ya mazao na bidhaa nyingine muhimu.

Serikali pia itakamilisha miradi mingi ya uzalishaji na usambazaji wa umeme ili kuwepo kwa nishati ya uhakika itakayowezesha kuongezeka kwa uzalishaji viwandani na pia matumizi ya umeme nyumbani yakiwemo maeneo ya vijijini. Upimaji wa ardhi, na mashamba na kuwapatia wananchi hati za umiliki ardhi unatarajiwa kuwezesha wananchi wengi kupata mikopo itakayowasaidia kufanya shughuli za uzalishaji mali na biashara na hivyo kuongeza kipato na kupunguza umaskini.

Kutokana na kazi nzuri iliyofanyika ya kudhibiti mianya ya rushwa, na kuimarisha usimamizi wa fedha za umma pamoja na matarajio ya ukuaji mzuri wa uchumi, mapato ya ndani ya Serikali yataendelea kuongezeka. Kuongezeka kwa mapato kutawezesha huduma za jamii zikiwemo za jfya, maji na elimu kutolewa kwa wingi na kwa ufanisi zaidi na hivyo, kuchangia kupungua kwa umaskini. Upatikanaji wa chakula cha kutosha kutokana na kuimarika Sekta ya kilimo na miundombinu ya masoko vitawezesha Mfumuko wa Bei kuendelea kubaki katika tarakimu moja na hivyo kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi wa hali ya chini.

Matarajio makubwa waliyo nayo wananchi kwa Serikali yao ni chachu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ili kwa pamoja kusukuma gurudumu la maendeleo mbele na kwa kasi kubwa.

# SURA YA NNE

## *4.0 Hitimisho*

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani Novemba2015, imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015-2020 pamoja na ahadi za mgombea urais wake kwa juhudi kubwa. Wananchi wameshuhudia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi kifupi cha takriban miaka miwili ya Uongozi wa Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hali ya uchumi imeendelea kuimarika kwa ukuaji wa wastani wa asilimia 7. Aidha, Mfumuko wa Bei umeendelea kudhibitiwa na kubaki katika wigo wa tarakimu moja kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na za fedha pamoja na upatikanaji wa chakula na kuimarisha miundombinu ya masoko. Vilevile, Serikali imeendelea kuchukua hatua murua za kuongeza uwezo wa Serikali katika kugharamia Bajeti na kupunguza utegemezi wa kibajeti ikiwa ni pamoja na kudhibiti na kusimamia makusanyo, kupunguza misamaha ya kodi na kuboresha Mifumo ya Kieletroniki ya ukusanyaji wa mapato. Kutokana na kuongezeka kwa mapato, uwezo wa Serikali kugharamaia miradi muhimu ya maendeleo umeongezeka na imeweza kulipa kwa wakati madeni yote ya ndani na ya nje yanayoiva.

Ujenzi wa miundombinu muhimu ikiwemo reli, barabara, madaraja, viwanja vya ndege na bandari unaendelea. Vilevile, uzalishaji na usambazaji wa nishati ya uhakika na upimaji ardhi kwa ajili ya mashamba, viwanda na makazi unafanyika kwa kasi. Miundombinu hii itasaidia kuweka mazingira mazuri kwenye uwekezaji wa viwanda na pia kuvutia utalii ambao unaliongezea Taifa fedha nyingi za kigeni.

Juhudi zote ambazo Serikali inazifanya, zinalenga kuongeza vipato vya Watanzania na kutoa huduma muhimu za jamii ikiwepo elimu bila malipo, afya na maji ili kupunguza umaskini miongoni mwa watu wetu.

Ni dhahiri kwamba, miaka miwili ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi imeonesha mwelekeo mzuri wenye mafanikio makubwa jambo linalotoa matumaini kwamba yale yaliyolengwa kutekelezwa ndani ya miaka mitano (5) yatakamilika ifikapo mwaka 2020 na pia kutekeleza masuala mengine ya ziada. Jukumu la wananchi ni kuunga mkono jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa. Vilevile, kila anayestahili kulipa kodi ni lazima alipe na kila mmoja awajibike kutoa taarifa zitakazosaidia kubaini wote wasiolipa kodi ili zipatikane fedha za kuwekeza kwenye miundombinu itakayosaidia ukuaji wa haraka wa uchumi na utoaji wa huduma muhimu za jamii.